AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

**BARAZA LA UTENDAJI**
**Kikao cha Kawaida cha Arobaini na Nne**
**Tarehe 15 Januari - 15 Februari 2024**
**Addis Ababa, ETHIOPIA**

**EX.CL/1505(XLIV)**
Matini Chanzi: Kiingereza

# RIPOTI YA MWAKA KUHUSU SHUGHULI ZA UMOJA WA AFRIKA NA VYOMBO VYAKE KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI DESEMBA 2023

***ORODHA YA VIFUPISHO*** ***..............................................*** *Error! Bookmark not defined.*

***NENO LA UTANGULIZI LA MHE. MWENYEKITI*** ***............*** *Error! Bookmark not defined.*

***MUHTASARI MKUU*** ***......................................................*** *Error! Bookmark not defined.*

***1. UTANGULIZI: Mwaka wenye Changamoto Lakini Wenye Mafanikio ya Kutia Moyo*** ***..........................................................................*** *Error! Bookmark not defined.*

***2. MATOKEO MUHIMU YA UTEKELEZAJI WA AJENDA 2063 VIPAUMBELE VYA MKAKATI.*** ***..............................................................*** *Error! Bookmark not defined.*

**2.1. UCHANGANUZI WA KIMATAIFA WA MPANGO WA KWANZA WA MIAKA KUMI YA UTEKELEZAJI WA AJENDA 2063 NA MAANDALIZI YA MPANGO WA PILI WA UTEKELEZAJI WA MIAKA KUMI.** **.........................................................................................**Error! Bookmark not defined.

2.1.1. Mbinu Bunifu na Jumuishi ........................................................................................................ 6

2.1.2. Uchanganuzi wa Kimataifa wa Mpango wa Kwanza wa Utekelezaji wa Miaka Kumi wa Ajenda 2063 : Muongo wa Maendeleo na Dira ya Baadaye, Kuoanisha Umuhimu, Uwiano, Ufanisi na Uendelevu. ........................................................................**Error! Bookmark not defined.**

2.1.3. Maandalizi ya Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi : Kuweka Mwongozo**Error! Bookmark no**

**2.2. AMANI, USALAMA, UTAWALA NA DEMOKRASIA: NGUZO MUHIMU KWA BARA.**Error! Bookmark not d

2.2.1. Uhimilivu wa Bara: Juhudi za UA katika Kudumisha Amani na Usalama**Error! Bookmark not defined.**

2.2.2. Kuimarisha Ushirikiano na Umoja wa Mataifa kuhusu Amani na Usalama**Error! Bookmark not defined**

2.2.3. Kuongeza Ubora wa Utawala: Mipango Muhimu na Mafanikio ya Umoja wa Afrika**Error! Bookmark not**

2.2.4. Kudumisha Usalama: Kuendeleza Amani kupitia Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika (AUPF)……………. ............................................................................**Error! Bookmark not defined.**

**2.3. MAENDELEO YA KIUCHUMI NA UTANGAMANO WA KANDA: VIPAUMBELE MUHIMU**Error! Bookmark n

2.3.1. Mazingira ya Kiuchumi ya Afrika: Maendeleo katika Uchumi wa Dunia na Athari zake kwa Bara ………………………………………………………………………………………………**Er ror! Bookmark not defined.**

2.3.2. Kaulimbiu ya Mwaka ya UA: “Kuharakisha utekelezaji wa AfCFTA”**Error! Bookmark not defined.**

2.3.3. Mageuzi ya Kiuchumi: Maendeleo, Biashara, Viwanda na Madini**Error! Bookmark not defined.**

**2.4 KUCHOCHEA MAENDELEO: MIUNDOMBINU, NISHATI NA DIGITALI…………………………34**

2.4.1 Vichocheo vya Mabadiliko: Mageuzi ya sekta y Anga, Usafiri, Reli, Bahari na Miundombinu barani Afrika………………………………………………………………………………………….34

2.4.2 Kuonyesha Mwelekeo: Maendeleo ya Nishati Endelevu barani Afrika…………………………..36

2.4.3 Kuvuka Mipaka ya Kidijitali: Kupiga hatua kwa Afrika katika AI, Usalama wa Mtandao, na Ustawi Unaoendeshwa na Data………………………………………………………………………………….38

**2.5. HUDUMA ZA KIBINADAMU, AFYA, HIFADHI YA JAMII NA UHAMIAJI: MAENDELEO YA KIJAMII MSINGI WA AJENDA YA UA.** **...............................................**Error! Bookmark not defined.

2.5.1. Uhimilivu wa Huduma za Kibinadamu: Njia za kutatua Changamoto za Afrika**Error! Bookmark not defi**

2.5.2. Kuimarisha Usimamizi wa Uhamiaji: Mkakati Unaoongozwa na Data wa AUC**Error! Bookmark not defi**

2.5.3. Kuwezesha Wafanyakazi wa Afrika: Kuimarisha Hifadhi ya Jamii & Kuchochea Maendeleo ya Kijamii barani Afrika.....................................................**Error! Bookmark not defined.**

2.5.4. Kuimarisha Michezo barani Afrika : Safari ya Kuelekea Maendeleo Shirikishi na Ubora wa Kimataifa.............................................................................**Error! Bookmark not defined.**

2.5.5. Kuimarisha Afya ya Umma na Utawala Barani Afrika: Mkakati wa Jumla wa AUC wa Kuzuia Magonjwa na Ushirikiano wa Kanda.......................................**Error! Bookmark not defined.**

**2.6. MAENDELEO ENDELEVU NA USALAMA WA CHAKULA: KUIMARISHA USTAWI WA BARA LA AFRIKA KWA AJILI YA WAKATI UJAO** **..................................**Error! Bookmark not defined.

2.6.1. Kuongeza Uhimilivu dhidi ya tabianchi: Uongozi wa AUC na Mwitikio wa Kimkakati kwa Changamoto za Kimazingira za Afrika. ......................................**Error! Bookmark not defined.**

2.6.2. Usalama Endelevu wa Chakula: Mipango ya Urutubishaji na Kilimo ya CAADP**Error! Bookmark not de**
2.6.3. Kuimarisha Kilimo Endelevu: Dhamira ya AUC ya Kuimarisha Usalama wa Chakula Barani Afrika.......................................................................................**Error! Bookmark not defined.**

**2.7. UTAMADUNI, ELIMU, WANAWAKE NA VIJANA: MKAKATI UNAOLENGA WATU.**Error! Bookmark not de
2.7.1. Kufungua fursa: Mkataba wa AUC wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Habari Barani Afrika.
…………………………………………………………………………………………………**Error! Bookmark not defined.**
2.7.2. Kujenga uwezo kwa ajili ya Wakati Ujao: Dira ya AUC ya Mipango ya Jinsia na Vijana**Error! Bookmark**
2.7.3. Kuimarisha Ushirikiano: Mikakati ya AUC kwa Diaspora ya Afrika**Error! Bookmark not defined.**

***3. MUHTASARI WA SHUGHULI ZA VYOMBO VINGINE NA TAASISI ZA UA***Error! Bookmark no

***4. UTAWALA WA TAASISI NA MABORESHO YA KITAASISI: MAENDELEO KUELEKEA UMOJA WA AFRIKA UNAOENDELEA, BORA NA WENYE UFANISI... 71***

**4.1 KUIMARISHA MATOKEO YA USHIRIKIANO, URATIBU NA USHIRIKIANO**
4.1.1. Kuelekea Kukamilika kwa Mchakato wa Mageuzi………………………………………………… 70
4.1.2. Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maamuzi ya Vyombo vya Kisera…………………………………….
4.1.3. Kujenga Uwiano wa Kimkakati………………………………………………………………………...
4.1.4. Kuanzisha Mfumo wa RBM wa UA……………………………………………………………………
4.1.5. Nyenzo Bunifu za Uratibu wa Uendeshaji……………………………………………………………
4.1.6. Kuimarisha Uhusiano na AU RECS/RMS na AUDA-NEPAD…………………………………...76
4.2. UFADHILI WA UMOJA WA AFRIKA…………………………………………………………………
4.2.1. Hali ya Bajeti ya UA…………………………………………………………………………………….
4.2.2. Ushirikiano na F15………………………………………………………………………………………
4.2.3. Utekelezaji wa Tozo ya 0,2%...........................................................................................,,,,,,,,,,,,,,,,,,
4.2.4. Kuelekea Vyanzo Bunifu vya Ufadhili……………………………………………………………….
4.2.5. Kuboresha Hali ya Ukaguzi wa UA…………………………………………………………
4.3. UFANISI WA UENDESHAJI………………………………………………………………………..
4.3.1. Uwajibikaji katika Utoaji Huduma …………………………………………………………..80
4.3.2. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano……………………………………………………………..
4.3.3. Nyaraka na Mikutano………………………………………………………………………………
4.3.4. Usimamizi wa Mali Zinazoshikika…………………………………………………………………
4.3.5. Ulinzi na Usalama……………………………………………………………………………………
4.3.6. Afya na Ustawi wa Wafanyakazi……………………………………………………………………
4.3.7. Protokali………………………………………………………………………………………………..
4.3.8. Vyombo vya habari na Kujenga Chapa ya UA…………………………………………………
4.3.9. Mahakama ya Utawala ya IES…………………………………………………………………
**4.4. USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU……………………………………………………………**
4.4.1. Maendeleo katika Utekelezaji wa Muundo wa Idara za AUC - Mwongozo wa Kuajiri………
4.4.2. Maendeleo katika Utekelezaji wa Muundo wa Idara za AUC Kupitia SACA…………

***5. AFRIKA KATIKA NGAZI YA KIMATAIFA........................................................... 75***

**5.1. KUELEKEA MUSTAKABALI MPYA: KUTENGENEZA MUSTAKABALI WA BAADAYE WA USHIRIKIANO WA UA ................................................................................................90**

**5.2. KUTOKA KUTAMBULIWA HADI USHAWISHI: UANACHAMA WA UMOJA WA AFRIKA KWENYE G20..............................................................................................................91**

**5.3. KUJENGA USHIRIKIANO: MFUMO WA URATIBU WA NGAZI TATU KATIKA UHUSIANO WA AU-UN ....................................................................................................92**

**5.4 KUTENGENEZA NJIA BUNIFU KWA AJILI YA UTAFUTAJI WA RASILIMALI .....................94**

***6. RIPOTI YA VINARA (Muhtasari Mkuu) ......................*** *Error! Bookmark not defined.*

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ACERWC** | Kamati ya Wataalamu wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto |
| **ACHPR** | AUC kuhusu Haki za Binadamu |
| **AFCFTA** | Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika |
| **AFCHPR** | Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu |
| **AFTCOR** | Kikosi Kazi cha Afrika kwenye mapambano dhidi ya UVIKO-19 |
| **AFRICA CDC** | Vituo vya Afrika vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa |
| **AGA** | Taasisi ya Utawala Afrika |
| **AMA** | Taasisi ya Madawa Afrika |
| **AMERT** | Mfumo wa Afrika wa Ufuatiliaji, Tathmini na Ripoti |
| **AMISOM** | Ujumbe wa Umoja wa Afrika nchini Somalia |
| **APSA** | Taasisi ya Amani na Usalama Afrika |
| **AU** | Umoja wa Afrika |
| **AUC** | Kamisheni ya Umoja wa Afrika |
| **AUDA** | Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika |
| **AUEOM** | Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Afrika |
| **AUFIS** | Taasisi za Kifedha za Umoja wa Afrika |
| **AUHR** | Mwakilishi wa Ngazi ya Juu wa Umoja wa Afrika |
| **AWLF** | Mfuko wa Afrika wa Uongozi wa Wanawake |
| **CIEFFA** | Kituo cha Kimataifa cha Elimu ya Wasichana na Wanawake barani Afrika |
| **CSO** | Asasi ya Kiraia |
| **CSV/RA** | Tathmini ya Athari za Kimuundo/Uhimilivu wa Nchi |
| **EMBS** | Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi |
| **EU** | Umoja wa Ulaya |
| **GDP** | Pato la taifa |
| **GEWE** | Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa wanawake |
| **MAPUTO PROTOCOL** | Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Haki za Wanawake barani Afrika |
| **MPFA** | Mfumo wa Sera ya Uhamiaji barani Afrika |
| **MPSI** | Kadi ya takwimu ya Protokali ya Maputo na Fahirisi |
| **MS** | Nchi Wanachama |

| | |
|---|---|
| **NGO** | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| **ODA** | Msaada wa Maendeleo kutoka Nje |
| **PANVAC** | Kituo cha Afrika cha Chanjo ya Mifugo |
| **PAP** | Bunge la Afrika |
| **PAVEU** | Chuo Kikuu cha Afrika cha elimu kwa njia ya mtamdao |
| **PBFA** | Kupanga, Bajeti, Fedha na Uhasibu |
| **PIDA** | Mpango wa Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika |
| **PRC** | Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu |
| **PSC** | Baraza la Amani na Usalama |
| **PSO** | Operesheni za Msaada wa Amani |
| **RECS** | Jumuiya za Kiuchumi za Kanda |
| **SAATM** | Soko la Pamoja la Usafiri wa Anga la Afrika |
| **SACA** | Tathmini ya Ujuzi na Umahiri |
| **SDGs** | Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| **SDGEA** | Azimio Rasmi la Usawa wa Kijinsia Barani Afrika |
| **SEZS** | Maeneo Maalumu ya Kiuchumi |
| **SRR** | Maboresho ya Sekta ya Usalama |
| **STC** | Kamati Maalumu ya Kitaalamu |
| **UN** | Umoja wa Mataifa |

## NENO LA UTANGULIZI LA MHE. MWENYEKITI

Kwa kuwasilisha ripoti ya shughuli za Kamisheni ya Umoja wa Afrika na vyombo vingine vya Umoja wetu kwa mwaka 2023, ni wajibu wangu kutimiza matamanio mawili muhimu.

Kwanza, ni suala la kuandaa orodha sahihi ya programu na miradi yetu, kubainisha changamoto ambazo tumekumbana nazo, kubainisha maendeleo yaliyopatikana, na changamoto na vikwazo ambavyo bado vinatusumbua.

Pili, tujiandae kupokea miongozo, mitazamo na maagizo kutoka kwa viongozi wetu, kwa nia ya kuboresha utekelezaji wa mipango na ahadi zetu za siku zijazo.

Kuwasilisha ripoti hii ni zaidi ya utaratibu wa kawaiad wa kiutawala. Inawakilisha wakati muhimu wa kubadilisha maarifa na zoezi makini la kimkakati.

Mabadiliko ya haraka na makubwa ambayo yanaelezea mazingira mapya ya kimataifa ya kijiografia, kiuchumi, kiutamaduni na kiteknolojia yanatuhitaji tuchunguze kila mara nafasi yetu ulimwenguni, katika safari yetu ya pamoja na njia bora zaidi ya kuendeleza uhusiano wetu na wengine. Ni muhimu kulinda urithi wetu wa kiutamaduni na kisiasa huku tukiendelea kulinda hadhi ya Umoja thabiti, wenye nguvui, kisayansi na kiteknolojia. Ni hapo tu ndipo tunaweza kufikia mabadiliko ya kimuundo ya uchumi wetu, msingi wa maendeleo jumuishi ya kweli.

Napenda kutoa shukurani zangu kwa kila Mkuu wa Nchi na Serikali, vinara wa masuala mbalimbali ya kimkakati kwa ajili ya Umoja wa Afrika, nawashukuru kwa mchango wao mkubwa kwenye kazi za Umoja wa Afrika .

Napenda kuhitimisha dibaji hii kwa kupongeza juhudi zisizo na kuchoka zinazofanywa na Wakuu wa Nchi na Serikali zetu zote kwa ajili ya ujio wa Afrika yenye misingi mipya inayowapatia wananchi wake wote mazingira bora ya kuishi. Napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi kubwa kwa wafanyakazi waliojitolea na wenye vipaji wa AUC na mfum wote wa kitaasisi wa UA.

Naomba ripoti hii iwe chachu ya mijadala yenye tija, yenye, msukumo wa mapendekezo yenye kujenga na chimbuko la mapendekezo ya kiubunifu kwa Afrika iliyoungana na yenye ustawi.

Mhe. Moussa Faki Mahamat, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika

**MUHTASARI MKUU**

Ripoti hii inatoa uchanganuzi wa jumla wa mipango ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC) pamoja na ile ya vyombo mbalimbali vya Umoja wa Afrika (UA) kwa mwaka 2023, ikionyesha mwelekeo mkuu wa kimkakati unaojumuisha juhudi za Umoja huo na ndio kiini cha shughuli zake. Inaanza na dibaji, ikifuatiwa na uchanganuzi wa muktadha wa kijiografia na kisiasa duniani, unaozingatia vikwazo vya nje na changamoto za ndani zinazoikabili Afrika. Kisha inaendelea kwa muongo wa kwanza wa utekelezaji wa Ajenda 2063, kubainisha maendeleo ambayo, ingawa ni mazuri kiasi, bado yana upungufu kwenye matarajio ya kimsingi, kutokuwa na mgawo wa kutosha, changamoto za kifedha na usimamizi wa majanga kama vile Uviko-19. Na mgogoro wa Urusi-Ukraine. Kulingana na tathmini hii, mapendekezo ya kimkakati yanatolewa ili kuongeza mafanikio ya Ajenda 2063 kwa kipindi cha 2024-2033. Katika uga wa amani na usalama, ripoti hiyo inaelezea kuwasilishwa kwa muundo mpya wa kitaasisi wa Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama, uimarishaji wa mfumo wa tahadhari ya haraka, utaratibu wa upatanishi, utatuzi wa migogoro, mapambano dhidi ya ugaidi, kuunga mkono utawala wa kidemokrasia, na ujumuishaji wa vipimo vya usalama wa binadamu. Inaonyesha umakini mkubwa wa kuzuia, unaodhihirishwa katika ujumbe wa waangalizi wa uchaguzi na mchango wa Kundi la Wenye hekima katika kuleta amani nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati na Chad. Mataifa ambayo yalifanya mabadiliko ya serikali kinyume na katiba yalisimamishwa kwenye shughuli za Umoja wa Afrika. Wakati huo huo, Umoja wa Afrika ulimarisha ushirikiano wake na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda ili kuoanisha mipango mingi ya amani, hasa mashariki mwa DRC, na kuunga mkono mchakato wa amani nchini Ethiopia.

Ukiendelea kuwekeza kikamilifu katika kutafuta amani nchini Sudan na maridhiano nchini Libya, Umoja wa Afrika umeimarisha ahadi yake ya kuzuia, hasa kupitia mapambano dhidi ya usambazaji wa silaha ndogo ndogo, na umetoa msaada wa kitaalamu na kifedha kwa Nchi Wanachama kwenye kipindi cha mpito wa kisiasa. Pia ilitoa msaada kwa michakato ya haki ya mpito na kuongeza kwa kiasi kikubwa ushiriki wa wanawake na vijana katika midahalo na mazungumzo ya amani, na hivyo kutambua jukumu lao muhimu katika kujenga amani ya kudumu katika bara. Kwa upande wa uchumi, ripoti imejikita kwenye azma ya mabadiliko ya kimuundo ya uchumi wa Afrika, inayoungwa mkono na utafutaji wa ufadhili kwa kuzingatia rasilimali za ndani, ukuaji wa sekta ya binafsi na ujasiriamali, na vile vile kuharakisha ukuaji wa viwanda, kutumia fursa ya utalii na rasilimali za madini, kupitia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotokana na Mkutano maalumu wa Niamey ambao ulifanyika mwaka 2022. Ili kuondokana na vikwazo vya kifedha na kukuza mafanikio ya mabadiliko ya kimuundo yanayotarajiwa na Ajenda 2063, UA imeongeza jitihada zake za kutekeleza maamuzi yanayohusiana na taasisi za fedha za Afrika, kupambana na mtiririko wa fedha haramu, na kukuza mageuzi ya kodi yanayolenga kuongeza mapato ya Nchi Wanachama. Kufadhili maendeleo ya Afrika, hata hivyo, bado ni mchakato mgumu ambao matokeo yake ni ya muda mrefu. Kwa muda mfupi, UA inafanya kazi ya kuongeza mvuto wa uchumi wa Afrika kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, huku ikiimarisha ushirikiano na wabia wa kimataifa na taasisi za kifedha, kwa lengo la kupunguza madeni ya mizigo na kurekebisha usanifu wa fedha wa kimataifa ili kuweka haki zaidi na usawa kwa nchi za Afrika. Ushirikiano wa kanda, ambao tayari umeanzishwa kama kipaumbele ili kukabiliana na changamoto ya kuzalisha mali na kuboresha ustawi wa watu wa Afrika, umepata msukumo mpya na utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara ya Bara la Afrika. Mkutano wa nne wa uratibu, uliofanyika Nairobi, ulijikita kwenye maendeleo yaliyopatikana katika kanda mbalimbali na kuainisha namna ya kusonga mbele. Azimio la Nairobi limetakiwa kuimarisha utendaji kazi wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, ambalo lilikuwa kaulimbiu ya mwaka wa 2023. Katika muktadha huu, maendeleo yanayohusiana na ZlecAf yanapaswa kuangaziwa, hasa mazungumzo kuhusu kipengele cha biashara, na hasa kanuni

zinazohusiana na sheria za asili, ambazo zinakaribia mwisho wake. Hivyo, kupitishwa kwa protokali zinazohusiana na uwekezaji, ushindani na hakimiliki, iliyopitishwa wakati wa mkutano wa thelathini na tano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, itaonyesha mwelekeo mzuri kuhusiana na mzunguko wa mtiririko wa uwekezaji na uhamiaji wa watu, mambo muhimu kwa mabadiliko ya kiuchumi wa Afrika na mafanikio ya ushirikiano wa kiuchumi wa bara. Ili kukabiliana na hitaji kubwa la kujaza nakisi ya miundombinu barani Afrika, Umoja wa Afrika umejitolea kuhusiana na uamuzi wa kutimiza maono yake, hasa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Miundombinu Afrika (PIDA) awamu ya II na mipango mingine mikubwa. Hili lilidhihirishwa na kuanzishwa kwa soko moja la usafiri wa anga, na kujiunga na Nchi Wanachama 37 ambazo zinawakilisha asilimia 90 ya usafiri wa anga ndani ya Afrika na ambazo zilijitolea kwa dhati kujiunga na Soko la Pamoja la Usafiri wa Anga la Afrika (SAATM), kwa sasa katika awamu ya majaribio katika nchi kadhaa. Juhudi za ziada zimefanyika ili kuboresha masuala mbalimbali ya usafiri wa aina nyingi, ikiwa ni pamoja na barabara, reli na njia za baharini. Katika suala la mabadiliko ya nishati, Umoja wa Afrika umejikita kwenye umuhimu wa nishati ya jotoardhi, huku ukitafuta kupunguza hatari zinazohusiana nazo, na umechukua msimamo wa kukuza haidrojeni inayozingatia mazingira. Hivyo, soko moja la umeme, lililozinduliwa mwezi Juni 2021, lilikuwa ishara ya uchanganuzi wa kina wa mifumo yake ya uendeshaji katika mwaka 2023 na athari za janga la Uviko-19 baada ya kuweka kipaumbele kwenye masuala ya afya ya UA. Mkakati wa Afya 2016-2030 umeonyesha maendeleo makubwa, kuboresha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za afya. Maendeleo haya ni pamoja na kuzuia na kudhibiti magonjwa, uchumi wa afya na ufadhili. Utekelezaji wa Taasisi ya Afrika ya Dawa ya Afrika (AMA), ulioanzishwa mwaka wa 2022, unaendelea na kuanzishwa kwa bodi ya wakurugenzi. Wakati huo huo, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC-Afrika) kilifanyiwa maboresho kwa nia ya kuongeza utendaji kazi na kuanzisha na kuendesha mfuko wa Afrika wa kushughulikia majanga. Suala la uhamiaji linabaki kuwa tatizo kubwa la Umoja wa Afrika. Umoja wa Afrika umeandaa nyaraka zinazohusu vipengele muhimu vya uhamiaji, ikiwa ni pamoja na utawala, sera za kupambana na biashara haramu ya binadamu, biashara ya wahamiaji, pamoja na mchakato wa kuwarudisha wahamiaji na kuwajumuisha tena kwenye jamii zao. Aidha, mkutano wa kwanza unaohusu wahamiaji waliopotea uliandaliwa kwa ushirikiano na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu. Wakati huo huo, Mpango wa Afrika wa Mazungumzo ya Kidiplomasia (INDABA) kuhusu uhamiaji ulianzishwa. Wakati tarehe ya mwisho ya Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) inapokaribia, Umoja wa Afrika unazidisha juhudi zake ili kufikia malengo ya Malabo, ukilenga katika kuimarisha ushirikiano, uhamasishaji, mawasiliano na utafutaji wa rasilimali; kuboresha miundombinu vijijini na uwezo wa masoko kwa ajili ya mazao ya kilimo; uzinduzi wa mkakati wa kilimo wa kidigitali wa Afrika; na maendeleo ya sekta ya kilimo, kwa kuhusisha wanawake na vijana wengi zaidi. Maendeleo makubwa pia yamepatikana katika kulinda afya ya wanyama na kutoa haki ya ardhi kwa jamii za vijijini. Kuhusu mazingira, Umoja wa Afrika umebuni mikakati inayojumuisha udhibiti wa hatari, mabadiliko ya tabianchi na uchumi wa bluu, na hivyo kuweka viwango vya kawaida vya sera za ndani na mfumo wa majadiliano na wabia wa nje. Tukio kuu la mwaka huu lilikuwa ni mkutano wa kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA kuhusu mabadiliko ya tabianchi, uliofanyika Nairobi, Kenya, Septemba 2023. Mkutano huu ulikuwa fursa kwa Afrika, kutokana na uwepo wa wadau mbalimbali, kuimarisha msimamo wake wa pamoja kuhusu masuala ya tabianchi kwa kuzingatia COP 28. Utaratibu mpya wa ufadhili umependekezwa ili kukidhi mahitaji ya kifedha ya Afrika, ikiwa ni pamoja na msamaha wa madeni. Majadiliano yalisababisha kupitishwa kwa Azimio lililozingatia ukuaji unaozingatia na suluhisho za ufadhili wa mabadiliko ya tabianchi. Katika sekta ya elimu, Umoja wa Afrika umefanya jitihada za kuharakisha utekelezaji wa mkakati wa elimu wa bara 2016-2025, kwa kuzingatia mpango wa malipo ya walimu na programu ya elimu ya ubunifu barani Afrika, ambapo mkutano wake wa kila mwaka ulifanyika Novemba 2023.

Mipango mingine ililenga kuanzisha Idara ya Afrika ya Ujuzi wa Kimataifa ndani ya AUDA-NEPAD, ili kuwapa vijana ujuzi wa kitaaluma na kuwatayarisha kwa ujasiriamali. UA pia imeandaa programu za elimu kwa ajili ya afya na ustawi wa vijana, pamoja na usawa wa kijinsia.

Taasisi ya Afrika ya Maendeleo ya Elimu (IPED) iliendelea kusaidia wizara za elimu za Nchi Wanachama katika ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya takwimu kwa ajili ya kuunda sera za habari. Semina za mtandaoni ziliandaliwa kuhusu mada kama vile uhamasishaji na ushirikiano, mafunzo na kujenga uwezo, na utafiti. Chuo Kikuu cha Afrika, ambacho ni mpango muhimu wa Umoja wa Afrika, kimetoa ufadhili wa masomo kwa vijana 3,474 wenye vipaji, wakiwemo wasichana 1,194, kwa kozi za uzamili na udaktari, kutoka Nchi 51 Wanachama. Hii inaashiria uwekezaji mkubwa katika mustakabali wa maarifa wa bara. Mkakati wa bara wa sayansi, teknolojia na ubunifu umerekebishwa kwa uangalifu, ikitarajiwa kusasishwa na kuongezwa muda hadi 2034. Msaada wa utafiti umeimarishwa na kuundwa kwa taasisi kadhaa za mtandao, ambazo zitaendelea na jitihada zao za ubora hadi katikati ya 2024. Uchunguzi wa maeneo unaoongozwa na Taasisi ya African Observatory of Science, Technology and Innovation, pia imenufaika kutokana na msukumo mpya. Katika sekta ya utamaduni, shughuli za UA zimeunganishwa kwenye miradi mikubwa kama vile Jumba Kuu la Makumbusho la Afrika na ukuzaji wa mafunzo yanayotolewa kuhusiana na urithi wa kiutamaduni. Makao makuu ya muda ya Tume ya UA ya Sauti-Video na Sinema yatakuwa nchini Kenya, hivyo basi kuimarisha ushawishi wa kiutamaduni. Ushirikiano ulitiwa saini kati ya UA na Uturuki ili kukuza ufundi, na juhudi zilifanyika katika kukuza lugha za Kiafrika pamoja na changamoto za utamaduni na lugha, hususani katika tasnia ya sanaa kwenye nchi za Afrika Magharibi. Mwaka wa 2024 utakuwa mwaka muhimu wa michezo kwa kuandaa Michezo ya Afrika huko Accra, Ghana, kuanzia Machi 8 hadi 23. UA, inayojishughulisha sana na maandalizi ya tukio hili, inazikaribisha Nchi Wanachama zote kushiriki kikamilifu katika michezo tofauti iliyo kwenye programu. Kuagizwa kwa ofisi za michezo za kanda hurahisisha uandaaji wa mashindano ya kanda ya maandalizi ya tukio hili kubwa la michezo la bara. Mikutano miwili ya kwanza kuhusu uanaume chanya ilisababisha uamuzi wa kihistoria wa wakuu wa nchi na serikali: kuandaa mkataba wa UA wa kukomesha unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana. Kando ya mkutano wa kawaida wa 36 Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA, Mkutano wa awali wa jinsia ulikuwa fursa ya kujadili ushirikishwaji wa kifedha wa wanawake, kwa kuzingatia protokali ya Maputo, inayosubiri kuridhiwa.

Nchi Wanachama zimetakiwa kuharakisha ukombozi wa wanawake na vijana ili kupunguza kwa kiasi kikubwa umaskini unaowaathiri. Uhusiano na Wanadiaspora wa Afrika umeimarishwa kupitia mipango kama vile Soko la Maendeleo ya Wanadiaspora wa Afrika na Mpango wa Kihistoria wa Uwekezaji wa Diaspora ya Afrika (HADIP) ambao unalenga kujenga uhusiano wa karibu kati ya Afrika na jumuiya zake za nje. Mwaka wa 2023 ulishuhudia mfululizo wa mikutano iliyozaa matunda na wabia wetu wa pande mbili na wa kimataifa, iliyohitimishwa na kukubaliwa kwa UA kama mwanachama kamili wa G20, kuashiria hatua muhimu ya kuunganishwa kwa UA katika utawala wa kimataifa. Kutambuliwa huku hutuhimiza kutathmini upya kwa kina na kwa kutazamia ushirikiano wetu ili kuhamasisha na kulinda maslahi yetu kwa uthabiti. Mageuzi ya kitaasisi ya UA, yanayokamilishwa hivi sasa, yamewezesha kuboresha ufanisi wa kibajeti na kuongeza rasilimali watu. Mapendekezo kutokana na ukaguzi yametekelezwa kwa kiasi kikubwa, na hivyo kuunganisha kipindi chetu cha mpito kuhusiana na usimamizi unaozingatia matokeo. Katika hali ya kuwiana na maendeleo haya, ni muhimu kudumisha ufuatiliaji makini wa utekelezaji wa maamuzi yanayochukuliwa na vyombo vyetu vya ushauri. Mwisho unaonyesha mshikamano unaotusukuma na kujumuisha kujitolea kwetu kwa pamoja kuelekea kutimiza maono tuliyo nayo kwa Afrika. Afrika inakabiliwa na changamoto nyingi

lakini pia ina rasilimali nyingi. Wakati umefika wa kutoa msukumo mpya wa ubora na kiasi kwa mradi wa ushirikiano wa kanda katika Afrika kwa ujasiri, uamuzi na shauku.

## 1. UTANGULIZI: MWAKA WENYE CHANGAMOTO LAKINI WENYE MAFANIKIO YA KUTIA MOYO

Ripoti hii, ni mwendelezo wa nyingine zilizotangulia, inalenga kuwasilisha muhtasari wa kina na sahihi wa mipango mikuu iliyotekelezwa katika mwaka wa 2023 na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na vyombo vingine vya Umoja wa Afrika ndani ya mfumo wa maelekezo ya kimkakati yaliyoainishwa kwa Nchi Wanachama. Shughuli hizi zilifanyika katika muktadha wa uchumi wa kimataifa uliotikiswa na kukosekana kwa utulivu na ishara ya kutokuwa na uhakika ambayo huficha makadirio yoyote yenye matumaini. Ikiathiriwa na matokeo ya usimamizi wa uchumi wa kimataifa uliogawanyika, Afrika inakabiliwa na athari za janga la Uviko-19, athari za mgogoro wa Urusi na Ukraine, na matokeo ya mabadiliko makubwa yaliyotokea katika miaka ya hivi karibuni wakati wa mgogoro wa Israel na Palestina. Mbali na changamoto hizo ni kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, ambayo yanaathiri sana tija ya kilimo na usalama wa chakula. Kwa upande wa kisiasa, matukio ya ukosefu wa uthabiti, yaliyosababishwa hasa na mabadiliko ya serikali kinyume na katiba, yamelitikisa bara la Afrika, kudidimiza maendeleo ya kidemokrasia na utawala na kuleta wasiwasi kuhusu mustakabali wa RECs. Pamoja na hayo, kama juhudi zilizochukuliwa katika kipindi cha muongo mmoja uliopita ndani ya mfumo wa Ajenda 2063 hazingezuiliwa na vikwazo vya ndani na nje, zingeweza kuunganisha jitahada zetu kwenye kasi ya kuelekea maendeleo ya Afrika. Hata hivyo, Umoja wa Afrika na vyombo vyake havijakwepa uzito wa vikwazo hivi. Tukiongozwa na uvumilivu na imani isiyoyumba katika siku zijazo, mwaka 2023 tulikamilisha tathmini ya muongo wa kwanza wa Ajenda 2063, ambapo matokeo yake yalisababisha maandalizi ya Mpangokazi wa muongo wa pili. Mwaka 2023, uliowekwa maalumu kwa Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika (AfCFTA), ulishuhudia kukamilika kwa shughuli muhimu zinazochochea kuanzishwa kwake. Idara na vyombo vinavyohusika viliendelea kutekeleza programu zao kikamilifu kwa ushirikiano na uratibu.

Programu hizi zilinufaika kutokana na usimamizi bora wa kibajeti na uboreshaji wa rasilimali kutokana na mageuzi ya kitaasisi, hasa kipengele cha SACA. Mizania yao inaonyesha nguvu ya utendaji licha ya changamoto zinazohusiana na ufadhili na rasilimali watu. Mafanikio binafsi ya idara na vyombo vya UA yanaonekana vizuri, lakini uzuri huo ungeweza kuimarishwa kama maendeleo yangekuwa sawa katika sekta zote. Kwa mfano, maendeleo katika eneo la amani na usalama yangeimarika kama yangeambatana na maendeleo sawa katika sekta ya kijamii na kiuchumi. Katika eneo la ushirikiano, UA imeunganisha mafanikio yake huku ikifanya kazi ya kurekebisha mbinu zake na wabia, kwa kuzingatia uwezo wa Afrika, mabadiliko ya kijiografia na uhusiano na Nchi Wanachama wake.

Katika mabadiliko haya, UA imeanza kwa usahihi ushirikiano wake ndani ya taasisi zinazohusika na utawala wa kimataifa, kama inavyothibitishwa na uanachama wake katika G20, hatua inayozingatiwa kama hatua ya awali kuelekea kuwepo kwa ufanisi katika utawala wa kimataifa. Maendeleo haya, hata hivyo, yanachangiwa na utambuzi wa changamoto nyingi ambazo ziko kwenye njia yetu kuelekea maendeleo jumuishi, hali ambayo muhimu kwa ajili ya kukuza sauti yetu katika anga la kimataifa. Miongoni mwa changamoto hizi, tunaona kiwango cha chini cha matumizi ya maamuzi ya vyombo vyetu vya majadiliano, utegemezi mkubwa wa kifedha ambao bado uko juu sana kwa wabia wetu, na tofauti kati ya

uwezo wetu halisi na matarajio yetu. Ni muhimu kwamba mawazo yetu ya kimkakati sasa yanachochewa na changamoto hizi na sehemu ya mfumo wa kimataifa unaoendelea kubadilika. Maendeleo haya yanaonyesha changamoto za ziada ambazo zinatusukuma kuimarisha mshikamano wetu ili kukuza sauti ya Afrika. Sauti ya umoja na yenye nguvu, yenye uwezo wa kusikika kwa uwazi kwenye ngazi ya dunia pamoja na ugumu wa changamoto za kisasa.

Hitimisho la ripoti hii litajikita katika kueleza zaidi changamoto zilizoainishwa. Haitaishia kwenye kuziorodhesha tu, lakini itatafuta kuimarisha uelewa wa masuala haya. Aidha, hitimisho litatoa mapendekezo ya vitendo ambayo yanatarajiwa kukidhi matarajio halali ya Bara letu. Mapendekezo haya yanalenga kuzalisha na kutumika kama jukwaa la mjadala madhubuti la majadiliano kati ya Nchi Wanachama ili kushughulikia masuali ya kimsingi kwa mustakabali wa Umoja wetu.

Yote yanahusu nini? Yanaonyesha shauku isiyoweza kubadilika ya kutafuta maboresho katika michakato yetu ya kufanya maamuzi katika utendaji kazi na usahihi.

# 2. MATOKEO MUHIMU YA UTEKELEZAJI WA AJENDA 2063 VIPAUMBELE VYA MKAKATI

## 2.1. UCHANGANUZI WA KIMATAIFA WA MPANGO WA KWANZA WA MIAKA KUMI YA UTEKELEZAJI WA AJENDA 2063 NA MAANDALIZI YA MPANGO WA PILI WA UTEKELEZAJI WA MIAKA KUMI

### 2.1.1. MBINU BUNIFU NA JUMUISHI

Kilele cha Mpango wa Kwanza wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (FTYIP) wa Ajenda 2063 mwaka 2023 ni hatua muhimu ya kihistoria kwa Umoja wa Afrika (AU), ikiashiria wakati muhimu katika dhamira isiyoyumba ya taasisi kwa ajili ya kukuza maendeleo makubwa na endelevu katika bara zima la Afrika. Uamuzi wa Baraza Kuu EX.CL/Dec.1164(XL) umeipa AUC na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD) jukumu zito, likiwapa jukumu la tathmini ya kina ya FTYIP (2014 - 2023) na maandalizi ya Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP). Mpango huu wa kimkakati, unaoitwa "Mradi Maalum wa Ajenda 2063" unasisitiza kujitolea kwa UA katika kutimiza malengo kabambe yaliyoainishwa katika Ajenda 2063, mwongozo wa dira ya mabadiliko ya kijamii na kiuchumi barani Afrika kwa zaidi ya miaka 50. Mradi Maalum ulizinduliwa Juni 2022 wakati wa Mkutano wa Kamati ya Mawaziri ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Ajenda 2063, ambayo iliongezwa na kujumuisha mawaziri wa Umoja wa Afrika wanaohusika na mipango ya maendeleo ya kitaifa na fedha.

Kwa kutumia mbinu shirikishi, ushirikishwaji uliimarishwa katika kurugenzi zote, idara, na miundo ndani ya Umoja wa Afrika (UA). Mbinu hii shirikishi ya kazi iliegemea zaidi kwenye dhamira ya nchi wanachama, iliyowezeshwa kupitia Kikosi

Kazi cha Ajenda 2063 na kamati ndogo za Ajenda 2063 katika ngazi za mabalozi na wizara. Katika mwaka mzima wa 2023, mchakato huu wa uchanganuzi uliendelea kwa ushirikiano ndani ya vyombo vya Umoja wa Afrika na kwa ushirikiano wa karibu na nchi wanachama. Aidha, Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi unakamilishwa na mkakati wa miaka 5 ulioandaliwa ili kutathmini hali ya utekelezaji ya nusu muhula. Mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini umeanzishwa ili kufuatilia maendeleo thabiti na ya utaratibu.




Pia, TWG ilitayarisha nyaraka mbili, zilizothibitishwa na Wataalamu wa Sekta husika kutoka Nchi Wanachama (52), RECs (7) na Vyombo vya UA. Aidha, nyaraka hizo ziliwasilishwa kwa Kamati ya Mabalozi na Mawaziri ya ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Ajenda 2063 na Baraza Kuu wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA Februari 2023.

Kufuatia Mkutano wa Februari, Baraza Kuu liliiagiza AUC kuandaa Mkutano wa Baraza Kuu ili kutoa mwongozo wa kimkakati kwa rasimu ya nyaraka. Mkutano ulijumuisha Mawaziri wa Mipango ya Maendeleo na Fedha, ulifanyika Oktoba 2023 mjini Kigali, Rwanda. Mkutano ulipitisha kwa muda rasimu hiyo, ikisubiri idhini ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Februari 2024.

Baada ya Mkutano wa Baraza Kuu, OSPD, kwa kushirikiana na AUDA-NEPAD, iliandaa warsha ya uthibitishaji wa Viashirio na Mfumo wa Gharama wa STYIP mjini Nairobi, Kenya, Desemba 2023. Wataalamu wa sekta husika kutoka nchi wanachama (49) walihudhuria warsha, ambayo ilijumuisha wataalamu wa mipango, takwimu, Ufuatiliaji na Tathmini, Kamati ya Wataalamu ya F15, Wawakilishi wa RECs (6), idara za AUC, na Vyombo vya UA.

### 2.1.2. UCHANGANUZI WA KIMATAIFA WA MPANGO WA KWANZA WA UTEKELEZAJI WA MIAKA KUMI WA AJENDA 2063 : MUONGO WA MAENDELEO NA DIRA YA BAADAYE, KUOANISHA UMUHIMU, UWIANO, UFANISI NA UENDELEVU

FTYIP (2014-2023) inajikita kwenye matarajio saba ya watu wa Afrika: "Afrika tunayoitaka ifikapo 2063". Pia inajumuisha malengo ishirini, maeneo thelathini na tisa ya kipaumbele, na shabaha zinazohusiana. Aidha, Mpango huo unaainisha aina ya miradi inayoongoza ili

kuharakisha utekelezaji wa mwongozo wa maendeleo wa Afrika. Matokeo ya tathmini yanawasilishwa hususani kuhusiana na umuhimu, uwiano, ufanisi, uendelevu na vigezo vya matokeo.

- **Uchanganuzi wa Umuhimu**: Matokeo ya tathmini yalidhihirisha uhusiano mkubwa kati ya FTYIP na mipango ya maendeleo ya taifa (NDPs).
- **Kuhakikisha Uwiano**: Matokeo ya tathmini yanaonyesha kiwango kikubwa cha uhusianio kati ya Ajenda 2063, FTYIP na mipango mingine ya maendeleo ya kanda, bara na kimataifa, ikijumuisha mipango ya maendeleo ya kiwango cha REC, Hi-5s inayosimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo hapa chini.

Kiwango cha Uhusiano kati ya Agenda 2063, SDGs na Hi5




- **Kutumia vizuri Rasilimali**: FTYIP haikutengewa bajeti, jambo ambalo lilileta changamoto katika kutathmini ukubwa kamili wa pengo la rasilimali, jambo ambalo liliathiri utafutaji wa rasilimali za kutekeleza Mpango huo. Matokeo ya jumla yanaonyesha, miongoni mwa mengine, kuwa kuna haja ya kujenga uhusiano kati ya amani, usalama na maendeleo katika Utekelezaji wa Ajenda 2063. Aidha, mkazo unaweza kuwekwa ili kuanzisha mfumo thabiti na wa kina wa ufadhili wa Ajenda 2063 msukumo wa kuhamasisha na kupeleka rasilimali watu na fedha za ndani za uhakika na endelevu.
- **Kufikia Malengo**: Uchanganuzi unaonyesha matokeo mchanganyiko lakini kwa matokeo ya jumla yalionyesha kuwa "hali sio nzuri". Uchanganuzi ulionyesha kuwa katika viashirio 10, Bara la Afrika lilivuka malengo husika, ambapo viwango vya ufaulu vilikuwa kati ya 51% na 100% kwenye viashirio 30. Hata hivyo, ufaulu wa Afrika kwenye viashirio 16 ungeweza kuwa wa juu zaidi, ambapo ulikuwa kati ya 1% na 50%, na mbaya zaidi katika viashirio 13 ambapo alama ya mwaka 2023 ilikuwa mabaya zaidi kuliko mwaka 2013.

Mfano wa matokeo kuhusu ufanisi




- **Kuhakikisha Matokeo ya Muda Mrefu:**
  - Uungaji mkono wa Kisiasa na Uongozi unaozingatia Ajenda: Uungwaji mkono wa kisiasa kwa Ajenda 2063 ulidhihirishwa hasa katika ngazi za juu za serikali za kitaifa. Hata hivyo, kuna haja ya kuwa na uhusiano zaidi kati ya viwango vya kujitolea vilivyoonyeshwa na watunga sera katika majukwaa ya uratibu wa mabara na yaliyoonyeshwa wakati wa Utekelezaji wa Ajenda 2063 katika nchi zao.
  - Kujumuisha Ajenda katika ngazi zote za Utekelezaji
    - *Ngazi ya Kitaifa*: Utekelezaji wa Ajenda 2063 katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ulihitaji kuimarishwa.
    - *Ngazi ya Kanda*: Ilihitajika kuwa na ushahidi zaidi unaoonyesha uhusiano thabiti kati ya vipaumbele vya RECs na vipaumbele vya Mpango wa kwanza wa miaka kumi wa Ajenda 2063.
    - *Ngazi ya Bara*: Taasisi za AU zinahitaji kufanya kazi zaidi ili kutoa miongozo ya sera kuhusu utumikaji wa ndani ya nchi, ujumuishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Ajenda 2063.
  - Ufadhili Endelevu wa Ajenda 2063:
  - Uhamasishaji wa Umma, Ushiriki, na Uungaji mkono: Kiwango cha uelewa wa Ajenda 2063, hasa katika ngazi ya kitaifa na ya jamii, kinaweza kuwa cha juu zaidi.

- **Tathmini ya Miradi ya Mikuu**: Tathmini ya FTYIP ilibaini maendeleo tofauti ya miradi kuu, kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo hapa chini.




Kwa kuhitimisha, Matokeo ya Tathmini yalibainisha kwamba:

Ajenda 2063 FTYIP
- Inafaa Sana
- Inafaa Kiasi
- Ufanisi dhaifu
- Inayofaa Kiasi
- Dhaifu katika uendelevu
- Athari inayojitokeza

$

## 2.1.3. MAANDALIZI YA MPANGO WA PILI WA UTEKELEZAJI WA MIAKA KUMI: KUWEKA MWONGOZO

STYIP ya Ajenda 2063 ni mrithi wa FTYIP. Maandalizi ya STYIP yaliongozwa na matokeo, mafunzo tuliyojifunza, na mapendekezo ya Tathmini ya FTYIP ya Ajenda 2063. Ilihusisha mchakato wa mashauriano na shirikishi na Nchi Wanachama, RECs, Vyombo vya UA, na Taasisi Maalumu.

Ingawa muongo wa kwanza ulishuhudia Nchi Wanachama wa UA zikifanana katika baadhi ya vigezo muhimu vya kijamii na kiuchumi, muongo wa pili ni kipindi cha kuharakisha Utekelezaji wa afua za Malengo na vipaumbele vya kimkakati. Hivyo Umoja wa Afrika utaongeza juhudi na msukumo ambao ulisaidia kuongezeka kwa mipango ya pamoja kama vichocheo vya kuharakisha maendeleo katika muongo wa pili. Utekelezaji Bora wa STYIP utafungua njia kwa muongo wa tatu, ulioandaliwa kama kipindi cha Afrika kupata matokeo makubwa zaidi. Wa nne utakuwa wa uthabiti, wakati muongo wa mwisho utazingatia ushawishi mkubwa wa Afrika katika masuala ya kimataifa.

(Tazama Kielelezo hapa chini)




Hivyo, Afrika inachukua misimamo ya pamoja katika masuala mengi yanayohusu maendeleo ya Bara la Afrika. Muhimu kati ya hiyo ni pamoja na:

- Azimio la pamoja na dhamira isiyoyumba ya Nchi zote Wanachama wa UA kutekeleza mpango mmoja wa maendeleo - Agenda 2063.
- Kukubaliana kuhusu Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mifumo ya chakula, mazingira na masuala ya mabadiliko ya tabianchi na kuonyesha juhudi za pamoja kati ya Nchi Wanachama wa Afrika kushughulikia kwa pamoja magonjwa kama vile Ebola na UVIKO-19.
- Aidha, nafasi ya RECs -- vizuizi vya utangamano wa kanda na bara, inazidi kuimarika, kama inavyoonyeshwa, miongoni mwa mengine, kupitia mikutano ya kila mwaka ya Uratibu ya UA ya nusu mwaka ambayo kwa kiasi kikubwa inalenga kujadili majukumu muhimu ya RECs na ushirikiano wa UA.

Katika muktadha wa Dira ya UA ya *"Afrika iliyounganishwa, yenye ustawi na amani, inayoendeshwa na raia wake yenyewe na kuwakilisha nguvu ya nguvu katika uga wa kimataifa"* na kuhamasishwa na haja ya kuongeza kasi ya Utekelezaji, Afrika itatekeleza malengo saba katika kipindi cha miaka kumi ijayo (2024-2033). Malengo hayo yatatoa mwongozo wa jumla katika mipango ya maendeleo, utekelezaji na uwekezaji katika Bara. Malengo saba yamepewa msukumo na matarajio saba ya Ajenda 2063 na yameainishwa kwenye kielelezo hapa chini.




Matarajio yameunganishwa, na raia wa Afrika kama msingi wake. Kila lengo lina aina ya **vipaumbele vya kichocheo**, shabaha zinazolingana, na mikakati elekezi. Aidha, Mpango umejikita kwenye njia kuu tatu zitakazoongoza utekelezaji, ambazo ni mifumo ya UA ya bara, mifumo ya kanda, na Mipango ya maendeleo ya kitaifa.

Mpango wa Pili wa Miaka Kumi wa Ajenda 2063 pia unajumuisha masuala wezeshi nane kwa ajili ya Utekelezaji bora wa Mpango. Haya ni pamoja na i) uratibu; ii) mawasiliano na uhamasishaji; iii) ushirikiano; iv) ufadhili; v) ufuatiliaji, tathmini, data, uwajibikaji, na kujifunza; vi) uundaji wa Ajenda 2063; vii) kutumia teknolojia zinazofaa katika Utekelezaji wa STYIP; na viii) kukuza uwezo. Aidha, mawazo makuu na mambo muhimu ya kuzingatia kwa ufanisi wa Utekelezaji wa Mpango yameainishwa. Yanajumuisha ushiriki na ushirikishwaji wa wadau wote wakuu, uoanishaji thabiti wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na Mipango ya Kanda na Bara, uwezo thabiti wa kibinadamu na kitaasisi, na umiliki kamili na wajibu wa kutekeleza STYIP kwa Nchi Wanachama wa UA.

Kwa mukhtasari, hitimisho la Mpango wa Kwanza wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (FTYIP) wa Ajenda 2063 mwaka 2023 ni alama ya mafanikio muhimu kwa Umoja wa Afrika (UA), kuonyesha dhamira yetu thabiti kwa maendeleo ya kina na endelevu katika bara zima la Afrika. Mchakato wa tathmini kamili, unaojumuisha Tathmini ya Mafanikio, Tathmini ya Msaada wa Utekelezaji, Mapitio ya Miradi Bora, na Uzoefu uliopatikana, hutoa maarifa muhimu ya kuunda Mpango ujao wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP).

STYIP inazingatia kimkakati vipengele muhimu, ikiwa ni pamoja na Utafutaji Endelevu wa Rasilimali, Ubora wa Utekelezaji, Mfumo wa Uwajibikaji, Ujenzi wa Uhimilivu, Utumikaji wa ndani na Umiliki, Uimarishaji wa Kimuundo, na uanzishwaji wa Mfuko Thabiti wa Maendeleo. Mtazamo huu wa kimkakati unaonyesha dhamira

yetu kwa mbinu iliyochanganuliwa na ifaayo katika kukuza maendeleo shirikishi katika bara zima la Afrika.

Muhtasari huu wa kimkakati unajumuisha maendeleo yetu ya kitaasisi na kuchukua hatua kwa ajili ya kuendelea na mipango yenye matokeo katika siku zijazo. Sehemu zifuatazo za Ripoti ya Mwaka zitajikit kwa undani zaidi, zikielezea shughuli mbalimbali za UA ambazo kwa pamoja zinachangia katika mchakato wa utekelezaji wa Ajenda 2063.

## 2.2. AMANI, USALAMA, UTAWALA NA DEMOKRASIA: NGUZO MUHIMU KWA BARA

AUC kupitia jukumu lake la kukuza amani, usalama na utawala barani Afrika imekuwa ikijikita katika kutekeleza nguzo tano (5) za kimkakati ambazo ni:

- Utekelezaji wa muundo mpya wa PAPS (muungano wa DPA-PSD) kwa uratibu ulioimarishwa na matokeo.
- Kuimarisha tena Mfumo wa Tahadhari za Mapema wa Bara, Kuzuia Migogoro na Usuluhishi.
- Uwezo Jumuishi wa Kudhibiti Migogoro, hasa Kukabiliana na Ugaidi na Misimamo mikali.
- Kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora; na
- Ushirikiano Jumuishi na Mzuri kwa Usalama wa Binadamu.

Baada ya kuunganisha Idara za Masuala ya Kisiasa (DPA) na Amani na Usalama (PSD) na kuunda Idara ya Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama (DPAPS), AUC imefanikiwa kuunganisha kazi ya idara hizi mbili za zamani. Kurugenzi ya Kudhibiti Migogoro (CMD) na Kurugenzi ya Utawala Bora na Kuzuia Migogoro (GCP) sasa zinashirikiana katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano, ujumbe wa waangalizi wa uchaguzi, ambazo hapo awali zilisimamiwa na DPA pekee ya zamani bila kuhusisha PSD, sasa zinapangwa kimsingi na GCP. Hata hivyo, CMD inashiriki kikamilifu katika kuhakikisha mafanikio ya ujumbe huu. Mbinu hii ya ushirikiano imeboresha ushirikiano kwa kiasi kikubwa.

Ujumbe wa UA wa waangalizi wa uchaguzi unasisitiza kwa kiasi kikubwa uzuiaji wa migogo, ukinuia kuepusha migogoro isizidi kuwa migogoro kamili. Kwa kutumia nyenzo zilizopo, AUC ilituma Jopo la Wenye Busara kwa diplomasia ya kuzuia katika nchi zinazofanya uchaguzi mwaka 2023. Jopo la Wenye Busara pia lilitumwa kwa Jamhuri ya Afrika ya Kati na Jamhuri ya Chad ili kushirikisha vyama na kuhimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya amani kupitia majadiliano. Ujumbe huu umefanikiwa.

Wasiwasi mkubwa umekuwa kuhusu ushughulikiaji wa changamoto kubwa za usalama za bara hili zinazosababishwa na watu kutoka nje, hususani kuongezeka kwa ushiriki wa mamluki na kampuni za kijeshi za binafsi. Katika kukabiliana na changamoto hii, AUC imeanzisha mapitio ya Mkataba wa OAU wa Kutokomeza Mamluki barani Afrika kuanzia 1977. Lengo ni kusasisha mkataba huo ili

kushughulikia kwa ufanisi hali ya sasa na kuhakikisha umuhimu wake katika kushughulikia masuala ya usalama ya kisasa.

### 2.2.1. UHIMILIVU WA BARA: JUHUDI ZA UA KATIKA KUDUMISHA AMANI NA USALAMA

Katika mwaka huu, bara la Afrika limeshuhudia mapinduzi mawili zaidi, yakitokea Niger na Gabon. Hii inafanya jumla ya idadi ya Nchi Wanachama zilizosimamishwa na Baraza la Amani na Usalama (PSC) kutokana na mabadiliko ya serikali kinyume na katiba kufikia sita (6): Mali, Sudan, Burkina Faso, Guinea, Niger, na Gabon.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, AUC ilitathmini usimamizi wa Vikwazo vya AU kupitia PSC, ikitoa mwongozo wa kisiasa ili kuimarisha ufanisi wake katika kuzuia mapinduzi ya kijeshi. AUC imetoa msaada wa kitaalamu na kifedha kwa Nchi Wanachama zinazopitia mabadiliko ya kisiasa. Adiha, msaada umetolewa kwa mataifa yaliyoathiriwa na migogoro na operesheni za kusaidia amani kama vile Ujumbe wa Mpito ya Umoja wa Afrika nchini Somalia (ATMIS) na mipango ya kanda kama vile Kikosi Kazi cha Pamoja cha Kimataifa (MNJTF) dhidi ya Kundi la Kigaidi la Boko Haram, Ujumbe wa SADC nchini Msumbiji (SAMIM), na Jeshi la Kanda la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC RF) katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kutokana na wasiwasi wa SADC kuhusu kuenea kwa juhudi za amani mashariki mwa DRC, AUC ilianzisha Jukwaa la Pande nne kwa ajili ya kuratibu na kuoanisha mipango ya amani katika eneo hilo. Jukwaa hilo linahusisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS), Mkutano wa Kimataifa wa Kanda ya Maziwa Makuu (ICGLR), na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Jamhuri ya Rwanda. Mkutano wa 1 wa wakuu wa nchi na serikali wa pande nne, uliofanyika Luanda, Angola, tarehe 27 Juni 2023, ulipitisha Mfumo wa Pamoja wa Uratibu na Uoanishaji wa Programu za Kulinda Amani Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Aidha, AUC imeunga mkono mchakato wa amani unaoongozwa na UA na Ethiopia kwa kuanzisha Mfumo wa Uhakiki, Uthibitishaji na Uzingatiaji (MVCM) kaskazini mwa Ethiopia tangu tarehe 29 Desemba 2022. Majukumu ya MVCM yameongezwa kwa miezi sita kuanzia Januari 2024, na kuchangia maendeleo mazuri katika jimbo la Tigray.

AUC imejumuisha masuala ya wanawake, amani, usalama, ulinzi wa watoto katika hali ya migogoro, na vijana, amani na usalama katika shughuli zake zote. Kundi la 2 la Mabalozi wa Amani wa Vijana wa Afrika (AYAPs) litakamilisha ma yake majukumu yake Februari 2024, na AUC iko katika harakati za kuteua kundi la 3, lililoratibiwa kushika madaraka yake Machi 2024.
Katika kukabiliana na ongezeko la tishio la ugaidi, misimamo mikali na uhalifu uliopangwa wa kimataifa katika bara zima, AUC, kwa kushirikiana na Kamati ya Usalama ya Afrika (CISSA) na Serikali ya Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania, iliitisha

mkutano wa kitaalamu mjini Nouakchott, Mauritania, kuanzia tarehe 5 hadi 7 Novemba 2023. Mkutano huo ulilenga kufufua Mchakato wa Nouakchott na Djibouti, ulioanzishwa ili kushughulikia vitisho vya usalama katika maeneo ya Sahelo-Sahara na Pembe ya Afrika/Afrika Mashariki.

### 2.2.2. KUIMARISHA USHIRIKIANO NA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU AMANI NA USALAMA

Kwa upande wa amani na usalama wa kimataifa, maendeleo ya kihistoria, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipitisha kwa kauli moja Azimio namba 2719(2023) tarehe 21 Desemba 2023, ili kushughulikia ufadhili wa shughuli za msaadai wa amani zinazoongozwa na Umoja wa Afrika (AUPSOs). Azimio hili lililoandaliwa na wanachama wa A3 wa Baraza hilo linalojumuisha Gabon, Ghana na Msumbiji, ni hatua muhimu katika kukabiliana na changamoto zinazohusiana na migogoro, uasi na kuenea kwa makundi yenye itikadi kali yenye silaha ambayo yamezuia harakati za UA za kutafuta amani, usalama na utulivu katika kanda.

Ukosefu wa rasilimali za kutosha umekuwa kikwazo cha muda mrefu cha kuendeleza shughuli zinazoongozwa na UA. Hivyo, Azimio 2719(2023) linaonyesha juhudi shirikishi za kushughulikia masuala haya kama ilivyosisitizwa na Balozi Pedro Comissário Afonso wa Msumbiji. Mwenyekiti wa UA Mhe. Moussa Faki Mahamat amelipongeza azimio hilo kama uthi wabitisho kihistoria la kukua kwa ushirikiano kati ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Kupitisha azimio hili kunaendana na dhamira ya UA ya kuwa na ushirikiano wa kanda na juhudi zake zinazoendelea za kupambana na migogoro, uasi na ugaidi katika eneo hilo.

Azimio hilo linazingatia moja kwa moja changamoto zilizoainishwa katika mafundisho ya UA kuhusu shughuli za msaada wa amani, hasa likisisitiza kipengele muhimu cha mafanikio ya ujumbe kwa "kuoanisha rasilimali na majukumu." Waraka huo unasisitiza haja ya kuwa na uwezo unaofaa na wa kutosha, ukisisitiza kwamba kufadhili PSO za UA ambalo ni jukumu la UA, kunahitaji michango ya ziada kutoka kwa wabia wa UA. Azimio hili linaashiria maendeleo muhimu katika uhusiano kati ya Umoja wa Mataifa na UA, kushughulikia suala la ufadhili ambalo limekuwepo tangu 2007 na kuimarisha dhamira ya pamoja ya operesheni bora za kulinda amani.

### BARAZA LA AMANI NA USALAMA (PSC)

AUC inaendelea kuunga mkono Baraza la Amani na Usalama katika kutekeleza majukumu yake, kwa kushirikiana na Taasisi za UA, RECs/RMs, na wabia kama vile Umoja wa Mataifa na Umoja wa Ulaya. PSC imeshughulikia hali zote za migogoro katika bara na masuala mbalimbali ya kaulimbiu yanayoathiri amani na usalama wa Afrika. Ripoti za kina kuhusu Uenyekiti wa PSC na shughuli zake katika mwaka wa 2023 na 2024 zimeonyeshwa katika majedwali hapa chini.

**UENYEKITI WA MWEZI WA PSC**

| No. | Month (2023) | Chairing Country | Permanent Representative |
|---|---|---|---|
| 1. | January | Uganda | H.E. Amb. Rebecca Amuge Otengo |
| 2. | February | South Africa | H.E. Amb. Edward Xolisa Makaya |
| 3. | March | Tanzania | H.E. Amb. Innocent Shiyo |
| 4. | April | Tunisia | H.E. Amb. Abdelhamid Elgharbi |
| 5. | May | Uganda | H.E. Amb. Rebecca Amuge Otengo |
| 6. | June | Zimbabwe | H.E. Amb. Sophia Nyamudeza |
| 7. | July | Senegal | H.E. Amb. Mohamed Lamine Thiaw |
| 8. | August | Burundi | H.E. Amb. Willy Nyamitwe |
| 9. | September | Cameroon | H.E. Amb. Churchill Ewumbue-Monono |
| 10. | October | Congo | H.E. Amb. Daniel Owassa |
| 11. | November | Djibouti | H.E. Amb. Abdi Mahamoud Eybe |
| 12. | December | The Gambia | H.E. Amb. Jainaba Jagne |

*Source: PSC Secretariat, Conflict Management Directorate, DPAPS*

Baraza la Amani na Usalama (PSC) lilipitia upya masuala mbalimbali, ikijumuisha uchunguzi wa kina wa hali mahususi za nchi (Jedwali 1) na masuala mbalimbali (Jedwali 2). PSC Ilifanya mikutano 25 kuhusu hali ya migogoro, iilijadili masuala 20 na mengine yalijadiliwa mara mbili), mikutano 3 kuhusu masuala ya kanda, 3 kuhusu oparesheni za kulinda amani (PSO's), na mikutano 15 iliyohusu masuala mengine yanayohusiana na amani na usalama barani Afrika; kama vile uratibu na A3 na ushirikiano na taasisi/vyombo vingine.

**Table 1: Country & Regional Considerations**




*Source: PSC Secretariat, Conflict Management Directorate*

Jedwali la 2: Masuala yaliyojadiliwa

| No. | Masuala yaliyojadiliwa | Idadi | Mkutano No. |
|---|---|---|---|
| 1. | Uchaguzi barani Afrika | 2 | 1132, 1165 |
| 2. | Tahadhali ya mapema | 2 | 1138, 1170 |
| 3. | Wanawake, Amani na Usalama | 2 | 1144, 1187 |
| 4. | Uhalifu wa Mtandaoni na Usalama Mtandaoni | 2 | 1148, 1171 |
| 5. | Mabomu ya ardhini | 1 | 1146 |
| 6. | Itikadi ya Uhalifu na Chuki Barani Afrika | 1 | 1147 |
| 7. | Shughuli za Kibinadamu barani Afrika | 2 | 1155, 1178 |
| 8. | CADSP na Vyombo Vingine Husika vya Ulinzi na Usalama katika Bara | 1 | 1159 |
| 9. | Ushirikiano na Kamati Ndogo ya PRC ya Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala; na Jukwaa la AGA | 1 | 1167 |
| 10. | Mfumo wa Vikwazo vya Umoja wa Afrika | 1 | 1181 |
| 11. | Kupambana na Ugaidi na Masuala Yanayohusiana | 1 | 1182 |
| 12. | Vijana, Amani na Usalama Barani Afrika | 1 | 1183 |
| 13. | Uhusiano kati ya Mabadiliko ya Tabianchi, Amani na Usalama | 1 | 1184 |
| 14. | Ujenzi na Maendeleo ya Baada ya Migogoro barani Afrika | 1 | 1188.1 |
| 15. | Majeshi binafsi na makampuni ya ulinzi yanayofanya kazi barani Afrika | 1 | 1189.1 |
| | **Jumla** | **15** | |



### 2.2.3. KUENDELEZA UBORA WA UTAWALA: MIPANGO MUHIMU NA MAFANIKIO YA UMOJA WA AFRIKA

AUC imetekeleza kwa dhati mipango ya kuendeleza utawala, demokrasia, haki za binadamu na amani katika bara zima. Mkazo wake uko kwenye utawala wa kidemokrasia, kisiasa, sekta ya umma na sekta ya usalama, ikikuza uratibu ndani wa Jukwaa la Utawala la Afrika (AGP), linalojumuisha Vyombo vya UA, Taasisi za Kanda na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs/RMs). Juhudi ni pamoja na kukuza uzingatiaji wa hati za UA kama vile Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi, na Utawala na Mkataba wa Afrika wa Maadili na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala. AUC imesaidia nchi wanachama, ikiwa ni pamoja na maandalizi ya uchaguzi, michakato ya kikatiba, haki za binadamu, haki ya mpito, na utawala wa sekta ya usalama.

**KUKUZA DEMOKRASIA: UJUMBE WA UA WA KUANGALIA UCHAGUZI NA KUELEKEA MWAKA 2024**

Ili kuimarisha utawala wa kidemokrasia, AUC ilituma ujumbe kabla ya uchaguzi. Ilitoa msaada kwa taasisi za kusimamia uchaguzi katika nchi kama Nigeria, Sierra Leone, Comoro, Zimbabwe, Liberia, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Ujumbe wa waangalizi wa uchaguzi ulitumwa kwa nchi 11 wanachama zilizofanya uchaguzi mwaka wa 2023. Rasilimali zaidi zinahitajika ili kuimarisha uwezo wa AUC kwa ajili ya kukuza demokrasia na utawala.

Majedwali yanayofuata yanatoa muhtasari wa kina wa uchaguzi wa urais wa mwaka 2023 kote barani Afrika, yakitazamiwa mabadiliko zaidi katika hali ya kisiasa wakati wa uchaguzi ujao wa mwaka 2024. Majedwali haya yanatumika kama marejeleo muhimu, yenye ripoti zinazobadilika za kidemokrasia na kujikita kwenye hatua muhimu zinazotoa mwelekeo wa kisiasa wa mataifa ya Afrika:

| Chaguzi za Urais mwaka 2023 | Nchi |
|---|---|
| 25 Februari 2023 | Nigeria |
| 24 Juni 2023 | Sierra Leone |
| 24 Agosti 2024 | Zimbabwe |
| 26 Agosti 2023 | Gabon |
| 10 Oktoba 2023<br><br>14 Novemba 2023 (marudio) | Liberia |
| 9 Novemba 2023 | Madagascar |
| 10-12 Desemba 2023 | Misri |

| | |
|---|---|
| 20 Desemba 2023 | DR Congo |

| **Chaguzi za Urais mwaka 2024** | **Nchi** |
|---|---|
| 14 Januari 2024<br><br>25 Februari 2024 (marudio) | Comoro |
| 4 Februari 2024 | Mali |
| 25 Februari 2024 | Senegal |
| 22 June 2024 | Mauritania |
| July 2024 | Burkina Faso |
| 15 July 2024 | Rwanda |
| May – August 2024 | Afrika Kusini |
| Oktoba – Novemba 2024 | Chad |
| 9 Oktoba 2024 | Msumbiji |
| Oktoba 2024 | Botswana |
| 7 Novemba 2024 | Mauritius |
| 24 Novemba 2024 | Tunisia |
| Novemba 2024 | Namibia |
| 7 Desemba 2024 | Ghana |
| Desemba 2024 | Algeria |
| Desemba 2024 | Guinea-Bissau |
| Desemba 2024 | Guinea |
| Sudan Kusini | Sudan Kusini |

**KUTOKA KWENYE MIGOGORO HADI UTHABITI: MIKAKATI YA UA KATIKA UTAWALA WA USALAMA NA UJENZI UPYA BAADA YA MIGOGORO.**

Umoja wa Afrika (AU) unaweka haki ya maendeleo katika kipaumbele katika juhudi za kimataifa za kukuza haki za binadamu. Mashauriano yanayoendelea ya Kanda ya Afrika kuhusu Haki ya Maendeleo yanashughulikia changamoto kuu kama vile umaskini, ukosefu wa ajira na upungufu wa huduma za kijamii.

Kuhakikisha utawala bora kwenye Usalama na Ulinzi ni muhimu ili kuzuia migogoro kote barani Afrika. UA inatumia mbinu thabiti ili kushughulikia masuala ya utawala wa sekta ya usalama, ikiwa ni pamoja na kupambana na Silaha haramu Ndogo

Ndogo na Nyepesi (SALW), mabomu ya ardhini, upokonyaji silaha na ujumuishaji upya ndani ya jeshi (DDR), mageuzi ya sekta ya usalama (SSR), na silaha za maangamizi (WMD). Mipango kuhusu SALW inasisitiza athari zake kwa amani, usalama, utulivu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa silaha na usimamizi sahihi wa silaha vinasisitizwa. AUC inasaidia kikamilifu programu za DDR za Nchi Wanachama na misaada katika kurejesha sekta za usalama ili kushughulikia vitisho vinavyoendelea. UA inajihusisha katika kuimarisha uzingatiaji wa hati za kimataifa dhidi ya kuenea kwa WMD na kukuza matumizi ya amani ya sayansi na teknolojia ya nyuklia, inayohitaji kuungwa mkono kwa ufanisi na uendelevu.

Mwaka 2023, AUC ilikamilisha maboresho ya kina ya Sera ya UA ya Kujenga Upya na Maendeleo baada ya migogoro (PCRD), ikiboresha mikakati ya ujenzi mpya baada ya migogoro. Kikosi Kazi cha UA kuhusu PCRD kinawezesha uratibu, na uteuzi wa Katibu Mtendaji wa Kituo cha UA cha PCRD, chenye makao yake makuu mjini Cario, Misri, ikiwa ni hatua muhimu ya utendaji. Huku kukiwa na ongezeko la migogoro ya silaha, hasa nchini Sudan, na kuibuka upya kwa mabadiliko ya serikali kinyume na katiba na ugaidi, bara hili lilishuhudia chaguzi nyingi za amani mwaka 2023. Kutuma Jopo la timu za upatanishi za Watu wenye Busara na ujumbe wa waangalizi wa uchaguzi kulichangia katika kuzuia uwezekano wa migogoro inayohusiana na uchaguzi.

## HAKI YA MPITO NA UTAWALA SHIRIKISHI AFRIKA: MIPANGO YA UA YA MWAKA 2023 NA KUENDELEA

Umoja wa Afrika (UA) unahimiza kikamilifu haki ya mpito, hasa kupitia maadhimisho ya kila mwaka kama yale ya Mauaji ya Kimbari ya mwaka 1994 dhidi ya Watutsi nchini Rwanda. Ukisisitiza umoja kati ya Nchi Wanachama, matukio haya yanapambana na mauaji ya halaiki na kukuza amani na maendeleo. Sera ya Haki ya Mpito ya UA (TJP) na mwongozo wa utaratibu baada ya migogoro na udikteta, kukuza amani, maelewano ya kitaifa, haki, uwajibikaji, na maendeleo endelevu.

Mwaka 2023, AUC ilisaidia Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Ethiopia kuhusu Haki ya Mpito na kuandaa mkutano wa kimataifa kuhusu Machaguo ya Sera ya Haki ya Mpito. Mpango kama huo ulifanyika nchini Sudan Kusini, na kuandaa kielelezo endelevu cha haki ya mpito. Mpango wa kina wa mafunzo kuhusu haki ya mpito kwa wanawake 35 ulipelekea kuanzisshwa kwa Mpango wa Wanawake wa Afrika kuhusu Haki ya Mpito (AW4TJ).

Kongamano la 7 la Afrika la Haki ya Mpito lilifanyika nchini Morocco (Septemba 2023) lililenga "Haki ya Mpito, Ushirikishwaji, Tofauti, na Haki ya Kijamii na Kiuchumi barani Afrika." Sanjari na Maadhimisho ya Miaka 20 ya Protokali ya Maputo, kongamano hilo lilijikita kwenye changamoto zinazowakabili wanawake katika migogoro na michakato ya kujenga amani. Lilibainisha hitaji la kuongezeka kwa ujumuishaji wa wanawake na vijana katika haki ya mpito, utawala, na kufanya maamuzi. Mapendekezo yalisisitiza ushiriki mpana wa makundi haya, kwa kutambua majukumu yao muhimu katika kukuza haki kamilifu ya kijamii na kiuchumi barani Afrika.

### 2.2.4. KUDUMISHA USALAMA: KUENDELEZA AMANI KUPITIA MFUKO WA AMANI WA UMOJA WA AFRIKA (AUPF)

Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika (AUPF) ni chombo muhimu kinachounganisha rasilimali za Afrika ili kukuza amani na maendeleo. Kuufanya Mfuko wa Amani ufanye kazi kunaashiria hatua ya vitendo katika kupunguza utegemezi wa Afrika kwa ufadhili wa nje na wafadhili. Hatua hii ya kimkakati inaboresha uwezo wa bara wa kushughulikia changamoto za usalama kwa kuelekeza fedha kwenye upatanishi, diplomasia ya kuzuia, utayari wa kitaasisi, na kujenga uwezo, ikiwa ni pamoja na kudumisha Kituo cha Utatuzi wa Migogoro (CRF).

- **Muundo wa Utawala na Usimamizi**: Maboresho ya usimamizi wa Mfuko wa Amani wa AU huongeza uwajibikaji, uwazi na ufanisi wa kiutendaji. Juhudi hizo ni pamoja na kuanzishwa kwa Kamati ya Ukaguzi, uteuzi makini wa Msimamizi wa Nje wa Mfuko, na mikutano ya robo mwaka ya Bodi ya Wadhamini. Sekretarieti ilipiga hatua kwa kuandaa Hadidu za Rejea za Kikosi Huru cha Tathmini, kilichoidhinishwa na Bodi, na mchakato wa uteuzi uliowekwa kwa mwaka 2024.

- **Wasimamizi wa Mfuko**: Uteuzi wa taasisi ya Old Mutual Investment Group kutoka Afrika Kusini na Sanlam Investments East Africa kutoka Kenya kama wasimamizi wa nje wa Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika ulitokana na zabuni ya wazi ya kimataifa iliyoendeshwa mwishoni mwa mwaka 2022.

- **Malengo ya Kifedha**: Malengo ya kifedha ya Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika ni kufikia lengo la dola milioni 400 kutoka kwenye michango ya Nchi Wanachama ifikapo Desemba 2023, kulingana na kiwango cha tathmini ya kipindi cha 2020-2022 kilichoongezwa kwa mwaka mmoja hadi Desemba 2023 (Assembly/AU/Des. 838(XXXV), Februari 2022, Addis Ababa).

- **Mgawo wa CRF**: Pamoja na mgawo wa bajeti ya msingi ya Mfuko wa Amani, Umoja wa Afrika umeanzisha Kituo cha Utatuzi wa Migogoro (CRF) kama sehemu muhimu ya utaratibu wa ufadhili wa Mfuko wa Amani. Kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 21 ya Protokali ya PSC, CRF inafanya kazi kama mfuko wa kuaminika ulioundwa kushughulikia kwa haraka mahitaji ya haraka na yanayobadilika ya amani na usalama ya Afrika. Kiwango cha 2023 cha CRF kilikuwa dola milioni 7, huku kukiwa na ongezeko hadi dola milioni 10 mwaka 2024. Mpaka sasa Mfuko wa Amani tayari umetoa dola milioni 4 mwaka 2023 kupitia PAPS, huku mgao ukielekezwa kwa Jeshi la Kanda la EAC Mashariki mwa DRC (dola milioni 2) na Upungufu wa ATMIS (dola milioni 2). Malipo haya yametumia riba iliyopatikana, ikionyesha utaratibu mzuri wa usimamizi ili kuhakikisha ufanisi endelevu wa mfuko.

- **Utafutaji wa Rasilimali**: Hitaji la Mfuko wa Amani ya kupata kwa haraka rasilimali za ziada za kifedha zaidi ya uwezo wake wa sasa na michango endelevu inayotarajiwa kutoka kwa Nchi Wanachama wa Afrika inasisitiza ulazima wa kukuza uhusiano thabiti, unaoendelea na wa kimkakati na wabiawa kimataifa.

Mfuko wa Amani umeshirikiana kikamilifu na wabia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Umoja wa Mataifa kwenye Umoja wa Afrika (UNOAU), iliyotuma wasaidizi

wawili kupitia Mpango wa UN SURGE. Ushirikiano zaidi na AfrEximBank umewezesha kutumwa kwa mtaalamu wa masuala ya fedha kwa Sekretarieti. Juhudi zinazoendelea na wabia kama vile AfDB na GIZ zinaendelea, kuashiria juhudi za pamoja za kupanua mtandao wa msaada wa mfuko.

Sambamba na juhudi hizi, Sekretarieti ya Mfuko wa Amani imeandaa kwa uangalifu mwongozo wa ushirikishwaji wa wadau na kwa sasa iko katika hatua za maandalizi ya kutenhgeneza mkakati wa utafutaji wa rasilimali. Kwa pamoja, mipango hii ni mfano wa dhamira ya mfuko ya kubadilisha vyanzo vyake vya kifedha na kuimarisha ushirikiano shirikishi kwa matokeo endelevu.

Mwezi Desemba 2023, PSC na Wajumbe watatu wa Afrika waliochaguliwa na UNSC (A3) walishiriki katika Semina ya Kumi ya Ngazi ya Juu kuhusu Amani na Usalama Barani Afrika mjini Oran, Algeria, kwa mujibu wa Azimio [PSC/AHG/COMM/1.( CCCXCVII)], lililopitishwa na PSC katika mkutano wake wa 397 uliofanyika katika ngazi ya Wakuu wa Nchi na Serikali tarehe 23 Septemba 2013. Matokeo muhimu yalijikita katika kuimarisha ushirikiano wa PSC-A3 katika kuendeleza na kukuza ajenda na maslahi ya Afrika katika ajenda ya UNSC. PSC na A3 zilifanya maadhimisho yake ya Miaka 10 na kujadili Mwongozo wa Mbinu za Kuimarisha Uratibu kati ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika na Wanachama kutoka Afrika wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Mwongozo huu unalenga kutoa mwongozo wa jinsi PSC na A3 zinaweza kukuza na kutetea misimamo ya pamoja ya Afrika ndani ya UNSC kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa, hati za kisheria za UA na maamuzi husika ya Vyombo vya kisera vya UA.

## 2.3. MAENDELEO YA KIUCHUMI NA UTANGAMANO WA KANDA: VIPAUMBELE MUHIMU

### 2.3.1. MAZINGIRA YA KIUCHUMI YA AFRIKA: MAENDELEO KATIKA UCHUMI WA DUNIA NA ATHARI KWA BARA

Pato la Taifa la Afrika lilitarajiwa kuongezeka hadi asilimia 4 mwaka 2023, kiwango cha pili kwa ukubwa duniani baada ya Asia (5%) na zaidi ya Amerika ya Kusini na Karibiani (1.6%) na, inategemewa kufikia asilimia 4.3 mwaka 2024, na kuonyesha kuendelea kwa uhimilivu wa bara hili dhidi majanga (Kielelezo 1). Licha ya mwelekeo huu chanya, ukuaji umesalia kuwa chini ya wastani wa kabla ya janga, 5% na chini kabisa ya kiwango kinachohitajika cha 7 hadi 10% kinachotarajiwa katika muda mrefu kufikia Dira na Matarajio ya Ajenda 2063 kwa bara lenye umoja, amani na ustawi. Kwa ujumla, ukuaji haujasababisha mabadiliko yenye tija yanayohitajika, ikijumuisha utengenezaji wa nafasi za kazi na ujumuishaji wa mnyororo wa thamani (AUC/OECD, 2018, 2019, 2022 na 2023).

**Kielelezo 1: Ukuaji wa Pato, 2018-2027**




**Chanzo:** AUC/OECD (2023), Africa's Development Dynamics 2023: Investing in Sustainable Development, AUC, Addis Ababa/OECD Publishing, Paris, https://doi.org/10.1787/3269532b-en.

Katika ngazi ya kanda, ukuaji unakadiriwa kuwa 4.9% Afrika Mashariki, 4.3% Afrika ya Kati, 4% Afrika ya Kaskazini, 3.8% Afrika ya Magharibi na 1.4% Kusini mwa Afrika. Licha ya fursa zake nyingi, mvuto wa uwekezaji wa Afrika unabaki chini ya uwezo wake. Bara linavutia sehemu ndogo kabisa ya: (i) mtaji kutoka kwa wawekezaji wa taasisi; (ii) Uwekezaji wa moja kwa moja wa kimataifa (FDI) na (iii) uwekezaji mpya umekuwa ukihama kutoka nchi zinazoendelea hadi nchi zenye kipato cha juu. Janga la UVIKO-19 liliharakisha mwelekeo huu: mwaka 2020-21, nchi zenye kipato cha juu nje ya Amerika ya Kusini na Karibiani zilivutia 61% ya FDI ya kimataifa ya rasilimali ambazo hazijatumika (kiwango kikubwa zaidi kuwahi kurekodiwa), ikilinganishwa na 17% kwa Asia inayoendelea, 10% kwa Amerika ya Kusini na Karibiani na 6% pekee kwa Afrika (kiwango cha chini zaidi tangu 2004), (Kielelezo 2).

**<u>Kielelezo 2</u>: Uwekezaji wa wa moja kwa moja wa kimataifa kwenye rasilimali ambazo hazijatumika kwa kanda za dunia, kama asilimia ya matumizi ya mtaji wa dunia, 2010-21**




**Chanzo:** Hesabu za Waandishi kulingana na FDi Intelligence (2022), Masoko ya fDi (kanzidata),www.fdiintelligence.com/fdimarkets.

Ili kuharakisha ukuaji na kukabiliana na mazingira yasiyofaa, serikali nyingi ziliongeza matumizi yao ya kifedha katika muktadha wa kupungua kwa mapato. Kudorora kwa hali ya kifedha, kupungua kwa nafasi ya fedha na kupungua kwa mahitaji ya nje kulisababisha viwango vya deni vilivyoongezeka na visivyo endelevu.

Wastani wa uwiano wa deni barani Afrika kwa Pato la Taifa unakadiriwa kubaki juu kufikia asilimia 66 mwaka 2023 na inategemewa kufikia asilimia 65 mwaka 2024 kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kifedha yanayohusiana na kupanda kwa gharama za kuagiza chakula na nishati, gharama kubwa za huduma ya deni na kushuka kwa thamani ya ubadilishaji wa fedha. Ili kufikia ukuaji jumuishi, maendeleo endelevu na ustawi wa pamoja kuelekea Ajenda 2063 kunahitaji kupanga ajenda ya uwekezaji na kutafuta 75% ya rasilimali za kifedha ndani ya nchi. Ili kuongeza uwekezaji kutoka kiwango cha sasa cha 20% hadi 40% ya Pato la Taifa kuna haja ya kuzingatia: (i) mbinu bunifu au zisizotumika za kukusanya rasilimali za ndani na mitaji binafsi ya nje; (ii) kupunguza vivutio vya kodi vinavyosababisha hasara ya dola bilioni 220 kila mwaka; (iii) kupunguza mtiririko wa fedha haramu (IFFs) unaogharimu dola bilioni 89 kila mwaka, takriban 3.7% ya Pato la Afrika na (iv) uwekezaji mkubwa katika kuleta mageuzi yenye tija katika sekta muhimu kama vile kilimo, kilimo biashara na huduma na kupunguza utegemezi mkubwa wa mauzo ya nje ya bidhaa ambazo hazijachakatwa na uagizaji wa bidhaa za viwandani na kuathiri mchakato wa mageuzi ya viwanda. Muhimu zaidi, kuna haja ya kutumia fursa za soko zinazotolewa na Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA), soko la watu bilioni 1.4 lenye Pato la dola trilioni 4.3 na kutumia uwezo wa vijana kupitia utoaji wa ujuzi wa kidijitali, ufadhili, na huduma za ujasiriamali na kwa kuweka mfumo wa udhibiti wa mazingira rafiki kwa biashara kwa maendeleo ya sekta binafsi.

### 2.3.2. KAULIMBIU YA MWAKA YA UA: "KUHARAKISHA UTEKELEZAJI WA AFCFTA"

Mkutano wa Kawaida wa 36 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliiteua "Kuharakisha Utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA)" kama Kaulimbiu ya UA kwa mwaka 2023.

- **Kuongezeka kwa Nchi Wanachama**: Jamhuri ya Botswana, Muungano wa Comoro, na Jamhuri ya Msumbiji zimeridhia Makubaliano ya AfCFTA, na kuongeza idadi ya Nchi Wanachama kutoka 44 hadi 47.

- **Mazungumzo ya Awamu ya Pili**: Kuhitimishwa kwa mazungumzo ya Awamu ya 2 kulipelekea kupitishwa kwa hati vitatu za kisheria na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA mwezi Februari 2023. Hizi ni pamoja na Protokali za AfCFTA kuhusu Sera ya Ushindani, Haki Miliki na Uwekezaji. Aidha, Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali ulipitisha Kanuni za Mawaziri kuhusu Mipango/Kanda Maalumu za Kiuchumi.

- **Kuanzishwa kwa Baraza la Rufaa**: Baraza la Rufaa lilianzishwa kwa uteuzi wa wajumbe watano na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA Februari 2023, na hivyo kuashiria maendeleo makubwa ya kutekeleza Utaratibu wa Usuluhishi wa Migogoro ya Bara chini ya Makubaliano ya AfCFTA. Mchakato wa uteuzi wa wajumbe wawili waliosalia unaendelea.

- **Mfuko wa Maboresho wa AfCFTA**: Mfuko wa Maboresho wa AfCFTA, wenye makao yake makuu mjini Kigali, Rwanda, ulianzishwa ili kufidia upotevu wa mapato ambao baadhi ya Nchi Wanachama zinaweza kupata

wakati wa mchakato wa ushuru huria. Afreximbank imetoa dola bilioni 1 kwa Mfuko, na kuna hitaji la jumla la dola bilioni 10 katika miaka mitano ijayo kwa utekelezaji kamili.

- **Kamati za Kitaifa za Utekelezaji (NICs):** Takribani Kamati 20 za Kitaifa za Utekelezaji za AfCFTA (NICs) zimeundwa kote katika Nchi Wanachama, kulingana na uamuzi wa Mkutano wa Kawaida wa 31 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA mwezi Julai 2018.

- **Ushirikiano na Wadau**: Ushirikiano mzuri umedumishwa na AUC, vyombo vingine vya UA, ikiwa pamoja na AUDA-NEPAD, CDC Africa, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs), na Sekta Binafsi ya Afrika. Kwa kuzingatia vipaumbele vya AfCFTA, Sekretarieti ya AfCFTA imeshiriki kikamilifu katika mazungumzo, kujenga uwezo, na maendeleo ya kitaasisi. Ambapo, 92.3% ya kanuni za mwanzo zilizokubaliwa katika sekta muhimu kama vile magari na nguo zimepitishwa, na kusababisha kuongezeka kwa upatikanaji wa soko, ushuru huria, na kuanzishwa kwa mifumo ya udhibiti wa huduma za kifedha, mawasiliano na usafiri.

Mpango Elekezi wa Biashara (GTI) na Mpango Elekezi wa Biashara ya Huduma (GTiS) imekuwa na jukumu muhimu katika kukuza na kuharakisha biashara yenye tija chini ya utaratibu wa upendeleo wa AfCFTA. Inatoa msaada wa kitaalamu na shughuli za kujenga uwezo kwa Nchi Wanachama, zinazochangia katika utengenezaji wa nafasi za kazi, ustawi bora na maendeleo endelevu katika bara zima.

Uwezeshaji wa biashara na maendeleo ya miundombinu, inayozingatia biashara na bidhaa linganifu za kuuza nje/kuagiza kati ya Nchi Wanachama, bado ni muhimu. Juhudi elekezi za biashara a zinahusisha sekta mbalimbali, zikiwemo utalii, usafiri, huduma za biashara, huduma za mawasiliano, huduma za kifedha, na utalii na huduma zinazohusiana na usafiri, zinazolenga ufanisi wa kiutendaji wa AfCFTA na kuongezeka kwa biashara ya kanda na ndani ya Afrika kwa maendeleo ya kiuchumi.
.

Aidha, uhusiano kati ya AfCFTA na taasisi ya Decade of African Roots na Diaspora (2021-2032) unalenga kuendeleza juhudi zinazoimarisha ushiriki wa makundi haya. Dhamira ya AfCFTA inahusu maendeleo yanayostahimili hali ya tabianchi, nishati mbadala, ukuaji wa viwanda wa vinavyozingatia mazingira, kilimo, usalama wa chakula, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Msisitizo pia umewekwa katika kuimarishwa kwa mifumo ya elimu, ukuzaji wa ujuzi, uwezo wa kuajiriwa, na ujasiriamali ili kuendana na malengo ya biashara ya bara la Afrika, na hivyo kuchangia ukuaji mpana wa uchumi na ustawi.

Mbali na shughuli zinazofanywa na Sekretarieti ya AfCFTA, kaulimbiu ya mwaka ilihamasishwa kikamilifu na idadi kubwa ya idara na vyombo vya AUC.

### 2.3.3. MAGEUZI YA KIUCHUMI: MAENDELEO, BIASHARA, VIWANDA NA MADINI

AUC ilifanya shughuli muhimu kwa nia ya kukabiliana na changamoto zinazoletwa na kuendelea kwa majanga mengi: kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, hatari zinazoendelea za UVIKO-19, kuimarisha hali ya kifedha duniani, na athari za kuongezeka kwa mivutano ya kijiografia. Shughuli hizi zililenga kuimarisha uwezo wa Afrika wa kuendeleza: (i) mifumo ya ufadhili jumuishi na endelevu; (ii) kuimarisha utafutaji wa rasilimali za ndani; (iii) kuendeleza utafiti wa kiuchumi kupitia machapisho na tafiti; (iv) kutumia uwezo wa utalii kwa kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi; (v) kukuza ujasiriamali, maendeleo ya sekta binafsi na uwekezaji; (vi) kuendeleza mtazamo wa bara wa kuwa na miundombinu bora na (vii) utekelezaji wa Dira ya Madini ya Afrika (AMV).

**MFUMO JUMUISHI NA ENDELEVU WA FEDHA KWA AJILI YA MABADILIKO NA MAENDELEO YA AFRIKA**

Taasisi za Kifedha za Umoja wa Afrika (AUFIs) zinazojumuisha Benki Kuu ya Afrika (ACB), Mfuko wa Fedha wa Afrika (AMF), Benki ya Uwekezaji ya Afrika (AIB) na Soko la Hisa la Afrika (PASE) ni moja ya miradi mikuu ya Ajenda. 2063 ili kutimiza malengo yake ya maendeleo jumuishi na endelevu. Mwaka 2023, Kamisheni ilipiga hatua kubwa, kuelekea kuanzishwa kwa AUFIs. Hadi sasa, maendeleo yaliyofikiwa ni kama ifuatavyo:

- **Benki ya Uwekezaji ya Afrika**: tangu kupitishwa kwa Protokali ya Benki ya Uwekezaji ya Afrika mwezi Februari 2009 (Assembly/AU/Dec.212 (XII)), na kupitishwa kwa Mkataba Februari 2010 (Assembly/AU/Dec.286 ( XIV)), nchi ishirini na mbili zimetia saini na sita kuridhia hati za kisheria za AIB.
- **Mfuko wa Fedha wa Afrika**: tangu kupitishwa kwa Protokali na Mkataba wa Mfuko wa Fedha wa Afrika mwezi Juni 2014 (Assembly/AU/Des.517 (XXIII)), nchi kumi na mbili zimetia saini na mbili pekee zimeridhia (Cameroon na Chad).
- **Benki Kuu ya Afrika**: Mwezi Agosti 2023, Baraza la Magavana liliiagiza AUC na Sekretarieti ya AACB kuwezesha Utaratibu wa Mapitio ya Pamoja kwa ajili ya kufuatilia muunganiko wa uchumi mkubwa. Utaratibu huu ulioundwa baadaye, ulianzishwa mnamo Oktoba 2023. Nyaraka zinazounga mkono kazi ya Sekretarieti zitawasilishwa kwa Ofisi ya AACB na Kamati Maalumu ya 7 ya Kitaalamu (STC) kuhusu Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano ili kujadiliwa.
- **Kujadili na kupitisha rasimu ya Mkataba wa Taasisi ya Fedha ya Afrika**: Kamisheni iliwasilisha rasimu ya Mkataba uliorekebishwa wa Taasisi ya Fedha ya Afrika (AMI) kwa STC ya 6 ya Fedha, ambayo iliipendekeza kwa Mkutano wa 45 wa Magavana wa AACB ili upitishwe. Mkataba huo uliidhinishwa Agosti 2023 na kutumwa kwa ajili ya kujadiliwa na Mkutano Maalumu wa 4 wa STC mwezi Oktoba 2023. Hata hivyo, ukosefu wa maelewano kati ya wataalamu ulisababisha mashauriano zaidi. Rasimu ya Sheria Iliyorekebishwa ya AMI itawasilishwa kwa STC ya 7 mwaka wa 2024 ili kujadiliwa kabla ya kuwasilishwa kwa Vyombo vya Kisera vya AU ili kupitishwa.
- **Soko la Hisa la Afrika**: Mwaka 2023, AUC na Shirikisho la Masoko ya Hisa Afrika Afrika (ASEA) ziliendelea kuimarisha ushirikiano wao katika mfumo wa Mkataba wa Makubaliano (MoU) uliotiwa saini Julai 2022, mjini Lusaka, Zambia. Lengo ni kuharakisha utekelezaji wa PASE kupitia Mradi wa African

Exchanges Linkage (AELP) ambao sasa unaunganisha masoko ya hisa tisa (9) ya Afrika.

## UTAFUTAJI WA RASILIMALI ZA NDANI (DRM) NA MTIRIRIKO WA FEDHA HARAMU YA (IFFS)

Mwaka 2023, maendeleo makubwa katika kuunga mkono juhudi za Nchi Wanachama kuhamasisha DRM na kupambana dhidi ya IFFs yalipatikana kupitia mfululizo wa mashauriano na programu za kujenga uwezo na wadau mbalimbali ili kurejesha dhamira ya Nchi Wanachama katika kukomesha IFF.

Hatua muhimu ni pamoja na: (i) kuandaa Kamati Ndogo ya Pili ya Ushuru na Mtiririko wa Fedha Haramu, iliyofanyika kuanzia tarehe 31 Mei hadi 02 Juni 2023, mjini Addis Ababa, Ethiopia; (ii) (iii) Kupitishwa kwa azimio la kihistoria la kuanza kwa mchakato wa kuelekea Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Ushuru uliowasilishwa na Nigeria kwa niaba ya Kundi la Afrika wakati wa Kamati ya Pili ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 22 Novemba 2023. Azimio hilo liliidhinishwa na nchi 125 zikiwemo wanachama wa G77 pamoja na China, na kuonyesha ushirikiano na umoja wenye nguvu wa kimataifa wa nchi za kusini kwa lengo la kuwa na mfumo wa kimataifa wa ushuru unaozingatia maendeleo.

- **Kuanzishwa kwa Taasisi ya Ukadiriaji wa Mikopo barani Afrika:** Kwa mujibu wa Uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Assembly/AU/Des.631 (XXVIII) uliopitishwa katika Mkutano wa Kawaida wa 28 uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia Januari 2017, Kamisheni na Mpango wa Kujitathmini Afrika (APRM) zilipiga hatua kubwa kuelekea kuanzishwa kwa Taasisi ya Ukadiriaji wa Mikopo barani Afrika. STC ya 6 kuhusu Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano iliidhinisha uanzishwaji wa Taasisi ya Ukadiriaji wa Mikopo inayoongozwa na sekta binafsi bila mzigo wa bajeti kwa Nchi Wanachama.
- **Kukuza Maendeleo ya Kiuchumi kupitia utafiti na machapisho**: Tafiti na machapisho kadhaa yalifanywa ikiwa ni pamoja na 2023 Africa’s Development Dynamic (AfDD), Ripoti ya Takwimu za Mapato Afrika 2023 na tafiti mbili kuhusu minyororo ya thamani ya Kanda na Bara. AUC kwa ushirikiano wa karibu na Benki ya Maendeleo ya Afrika na AUDA NEPAD zimekamilisha Utafiti kuhusu hatua muhimu za kukuza ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu utakaokamilika mwishoni mwa 2023.

## KUIMARISHA UTANGAMANO WA KIUCHUMI: KUANDAA NJIA YA UKUAJI WA JUMUIYA YA UCHUMI YA AFRIKA (AEC)

Mwezi Julai 2023, AUC iliunga mkono shughuli za ubunifu kuelekea Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika (AEC), katika kutafuta ukuaji wa uchumi wa Afrika. AUC ilitoa Ripoti ya Ushirikiano wa Afrika (AIR), ambayo ilitumia AMRII kupima ushirikiano wa kanda. Ili kutarajia hatua zaidi ya AfCFTA, Kamisheni iliagiza ufanyike utafiti kuhusu maandalizi ya Umoja wa Forodha wa Afrika kuelekea utekelezaji wa AEC.

Hatua muhimu zilichukuliwa ili kuimarisha biashara kwa maendeleo ikijumuisha: (i) Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa WTO na majadiliano ya AGOA mwezi Septemba 2023; (ii) Mkakati wa AU E-Commerce, unaoungwa mkono na Nchi Wanachama; (iii) mapendekezo madhubuti kupitia Mpangokazi; (iv) kusasisha Mpangokazi wa BIAT; (v) kuzinduliwa kwa African Trade Observatory (ATO) mwezi Novemba na; (vi) Maadhimisho ya Jukwaa la Ushirikiano wa Afrika 2023 na Siku ya Utangamano wa Afrika. AUC, chini ya Azimio la Mkutano wa Tano wa Nusu Mwaka wa Uratibu, uliofanyika Nairobi tarehe 16 Julai 2023, ilionyesha dhamira mpya ya Nchi Wanachama katika kuharakisha ushirikiano wa Afrika ili kukabiliana na matatizo ya utandawazi kupitia sera za kanda zilizoratibiwa kwa ajili ya mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

## KUTUMIA FURSA YA UTALII KWA MAGEUZI YA KIJAMII NA KIUCHUMI

Utalii una uwezo wa kuharakisha mabadiliko ya kijamii na kiuchumi barani Afrika. Kufikia mwaka wa 2030, matumizi katika sekta ya utalii, ukarimu na burudani barani Afrika yanatarajiwa kufikia takriban dola bilioni 261.77, dola bilioni 137.87 zaidi ya mwaka 2015, Kamisheni ilifanya shughuli za kimkakati ili kutumia fursa ya utalii kama kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi shirikishi na maendeleo endelevu chini ya AfCFTA kuelekea Ajenda 2063. Haya ni pamoja na: (i) kurasimisha ubia wa kimkakati katika sekta ya utalii kupitia Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Bodi ya Utalii ya Afrika (ATB) tarehe 30 Mei, 2023; (ii) kushiriki katika matukio ya kimataifa ya watalii (Mkutano wa Uhimilivu Utalii uliofanyika Jamaika Februari 2023 na African Travel INDABA huko Durban, Afrika Kusini, 2023) na majadiliano ya kimkakati na Ufalme wa Saudi Arabia ili kuimarisha ushirikiano katika programu za elimu na mafunzo ya utalii ili kukuza stadi za utalii katika nchi za Afrika.

## KUKUZA UJASIRIAMALI, MAENDELEO YA SEKTA BINAFSI, NA UWEKEZAJI

Wakati sekta binafsi inazalisha asilimia 70 ya pato la Afrika, asilimia 70 ya uwekezaji wake na asilimia 90 ya ajira zake, AUC iliunga mkono Nchi Wanachama katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara kwa sekta binafsi kustawi kupitia kuandaa Kongamano la 14 la Sekta Binafsi la UA jijini Nairobi, Kenya kuanzia Julai 2023 na, ilitayarisha Mpango wa Bara wa Wanawake na Vijana wajasiriamali ili kushughulikia vikwazo vya sera kwa ukuaji wa ujasiriamali. AUC pia ilishiriki katika mikutano ya kimataifa kama vile Kongamano la Nne la Kiuchumi na Biashara la Afrika-Türkiye mjini Istanbul ili kuongeza mvuto wa uwekezaji wa Afrika. AUC pia iliandaa warsha ya uhamasishaji jijini Nairobi, ikilenga Mkakati wa Bara la Afrika kwa uwekezaji bora na endelevu barani Afrika. Mafanikio mengine ni pamoja na: (i) kutayarisha Mwongozo wa Sera ya Kuanzisha na Sheria ya Mfano ya ujasiriamali, ajira na ukuaji; (ii) uwasilishaji wa muundo wa Kituo cha Ubora wa Soko Shirikishi la Afrika (AIMEC) kwa Kamati Ndogo ya Muundo ya PRC.

## UENDESHAJI WA VIWANDA: KUTEKELEZA MAAMUZI YA MKUTANO WA UA KWA AJILI YA MABADILIKO YA KIUCHUMI.

Katika uga wa kimkakati wa ukuzaji viwanda, AUC wadau mbalimbali walifanya kazi ili kuharakisha utekelezaji madhubuti wa Maamuzi ya Mkutano Maalumu wa 17 wa Baraza la Umoja wa Maendeleo ya Viwanda na Mabadiliko ya Kiuchumi uliofanyika Novemba 2022 mjini Niamey Niger. STC ya 4 kuhusu Biashara, Viwanda na Madini iliahirishwa hadi tarehe na mahali vitajulikana mwaka 2024.

### MAENDELEO YA SERA YA UBORA YA BARA NA MIUNDOMBINU BORA YA AFRIKA

Mwaka 2023, Kamisheni iliimarisha dhamira yake ya maendeleo ya kiuchumi ya Afrika kwa kutekeleza Sera ya Ubora ya Afrika (AQP). Kufuatia kupitishwa kwake katika Mkutano wa 40 wa Kawaida wa Baraza Kuu, Baraza la Utekelezaji la AQP lilianzishwa ili kuendeleza utekelezaji wake. Kwa kushirikiana na taasisi za PAQI, Kamisheni ilipiga hatua katika kuandaa Mpangokazi wa Sera ya Ubora ya Afrika (AQPAP) na Mfumo wa Udhibiti wa Kitaalamu wa Bara la Afrika (ACTReF). AUC pia ilipiga hatua katika kuandaa mpango wa uidhinishaji wa Made in Africa (MiA) ili kusaidia minyororo ya thamani ya kanda kwa kutumia rasilimali za Afrika katika uwiano wa kimkakati na malengo ya viwanda na mabadiliko ya mauzo ya nje.

### UTEKELEZAJI WA DIRA YA MADINI YA AFRIKA (AMV)

Huku wastani wa asilimia 60 ya Pato la Taifa likitokana na maliasili na huduma muhimu za mfumo ikolojia, Afrika bado ina uwezo mkubwa wa kufaidika na maliasili zake ili kufadhili maendeleo endelevu shirikishi. Kwa kuzingatia fursa hizo, Kituo cha Maendeleo ya Madini Afrika (AMDC) kiliongoza utekelezaji wa Bara la Afrika wa Dira ya Madini ya Afrika (AMV), kuimarisha msingi wake wa kitaasisi na kukuza ubia muhimu. Juhudi hizi zilihusisha uratibu wa kimkakati na kuanzisha sekretarieti ya muda. Msaada huu wa kina ulipanuliwa kutoka kuunda Mkakati wa Afrika wa Madini Unaozingatia mazingira hadi kuandaa kwa ufanisi mfululizo wa Maonyesho na Kongamano la Vito vya Afrika (AGJEC). AMDC ilichangia kikamilifu katika jitihada za kujenga uwezo kwa serikali na wadau, kukuza upatikanaji wa fedha, teknolojia, na ubunifu na kuimarisha ushiriki katika minyororo ya ugavi wa ndani na kanda. Sambamba na hilo, AMDC iliweka kipaumbele katika kunzisha mtandao wa wataalamu mahiri, unaopanuka kwa kasi kupitia ushirikiano na mwingiliano wakati wa matukio. Mpango huu unalenga kuzalisha maarifa na kutoa msaada wa kitaalamu, kuhakikisha utekelezaji na ufuatiliaji wa kanuni za AMV na kuwezesha biashara ya madini.

### KULINDA MAARIFA YA ASILI YA AFRIKA KUPITIA HAKIMILIKI

Ikizingatia uwezo wa maarifa asilia ya Afrika na hakimiliki kama nyenzo za kimkakati zinazoweza kutumiwa kuwezesha maendeleo ya Afrika kupitia kutoa motisha kwa wavumbuzi, AUC ilihamasisha uongozi wake kupitia ushirikiano wa kimkakati na washirika na Nchi Wanachama ili kutumia vyema maarifa asilia na hakimiliki Kupitia utekelezaji wa mradi wa Hakimiliki na Ubunifu barani Afrika (AfrIPI), AUC inalenga, kwa ushirikiano na Kamisheni ya Ulaya na Ofisi ya Hakimiliki ya Umoja wa Ulaya (EUIPO) kusaidia mchakato wa kuunda, kulinda, kutumia, kusimamia, na kutekeleza hakimiliki (IPR) kote barani Afrika.

## 2.4 KUCHOCHEA MAENDELEO: MIUNDOMBINU, NISHATI NA DIGITALI

## 2.4.1. VICHOCHEO VYA MABADILIKO: MAGEUZI YA UENDESHAJI WA SEKTA YA ANGA, USAFIRI, RELI, BAHARI, NA MIUNDOMBINU BARANI AFRIKA

### KUKUZA SEKTA YA ANGA BARANI AFRIKA: MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA SAATM, VIWANJA VYA NDEGE BORA, NA MAFUTA ENDELEVU YA ANGA.

Pamoja na ahadi kutoka kwa Mataifa 37 ya Afrika ya kujiunga na kushiriki kikamilifu kutoka 20 katika Mradi wa Utekelezaji wa Majaribio (PIP), Soko la Usafiri wa Anga la Afrika (SAATM) linasonga mbele kwa mafanikio kuelekea utekelezaji kamili. Hatua kubwa imefikiwa na utekelezaji wa Sekretarieti ya Mfumo wa Usuluhishi wa Migogoro ya SAATM (DSM) na uanzishwaji wa mwomgozo wa shughuli zake.

AUC imeanzisha mradi unaolenga kujenga viwanja vya ndege bora ili kuimarisha usalama wa anga na kuwezesha sekta hiyo kufufuka kwa muda mrefu. Juhudi hii ya kuangalia mbele inaonyesha kujitolea ili kuboresha miundombinu ya anga na kuhakikisha uthabiti wa tasnia.

Aidha, Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Uchukuzi, Miundombinu ya mabara na Kanda na Nishati (STC-TTIIE) imetekeleza jukumu muhimu katika kuandaa na kuidhinisha mkakati wa bara wa kutumia nishati endelevu za anga (SAF).

### KUKUZA UCHUMI WA BARA: KUIMARISHA SEKTA YA USAFIRI WA BARABARA

Mkakati wa kina wa kuimarisha maendeleo ya kiuchumi ya Afrika kwa kuimarisha sekta ya usafiri wa barabara umepata maendeleo makubwa. STC-TTIIE, ikiwa imeunda na kuidhinisha mwongozo wa barabara za bara, ilianza tathmini ya msingi kwa ushirikiano na ECOWAS na ECCAS ili kujadili mapendekezo ya vyombo vya udhibiti wa usafiri wa barabarani. Ikishughulikia maswala kuhusu usalama barabarani, AUC inasimamia kikamilifu utekelezaji wa mpango wa kina wa usalama barabarani kuanzia 2021 hadi 2030. Mpango huu unahusisha uanzishwaji wa waratibu wa kitaifa wa data wenye jukumu la kutoa ripoti za kila mwaka za hali ya usalama barabarani. Aidha, juhudi zinazoendelea zinaelekezwa katika kuweka viwango na miongozo ya sekta ya usafiri mijini, inayojumuisha usafiri wa umma na usio wa magari na usafiri wa kielektroniki. Juhudi hizi zinalenga kuchangia katika kupunguza utoaji wa gesi chafu kutoka kwa sekta ya uchukuzi, kwa kuzingatia malengo mapana ya uendelevu.

### KUKUZA MAENDELEO YA KIUCHUMI: MAENDELEO NA MIPANGO KUHUSIANA NA MTANDAO WA RELI YA MWENDOKASI AFRIKA (AIHSRN)

Sekta ya reli ni muhimu katika kuendeleza ukuaji wa uchumi wa Afrika, ikilenga hasa kuendeleza Mtandao wa Reli ya Mwendokasi barani Afrika (AIHSRN) mradi unaoongoza kwenye Ajenda 2063. Miongoni mwa njia kumi na tatu za majaribio za reli, nane zimevuka hatua ya upembuzi yakinifu hadi awamu ya upangaji upya na ujenzi, na hivyo kusisitiza dhamira ya sekta hiyo kwa utekelezaji wa mradi kwa wakati.

Ukamilifu wa miradi hii ya majaribio katika awamu ya kwanza ifikapo 2033 ni alama muhimu. Warsha iliyoandaliwa Mei 2023 ililenga kusasisha mipango ya kitaifa ya maandalizi ya miradi hii, ikisisitiza kuzingatia kikamilifu kanuni na viwango vya mwingiliano wa reli. Ikitambua changamoto za kifedha zinazokabili Nchi Wanachama katika kutekeleza miradi ya reli, AUC imefanya juhudi za uhamasishaji ili kuhimiza Mataifa mengi zaidi kuridhia Protokali ya Luxembourg kuhusu treni. Hatua hii ya kimkakati iko tayari kupunguza gharama ya vifaa vya reli, na kutoa msukumo muhimu kwa uwezekano wa kiuchumi wa kupanua miundombinu ya reli ya kanda.

## KUKUZA UKUAJI WA UCHUMI: KUWEKA KIPAUMBELE KWENYE USAFIRI UNAOZINGATIA MAZINGIRA NA UFANISI WA USAFIRI WA BAHARINI AFRIKA

Kwa kutambua jukumu kubwa la usafiri wa Baharini, Bandari, na sekta ya Usafirishaji katika kuendeleza maendeleo ya kiuchumi, AUC imesisitiza umuhimu wa uchumi unaozingatia mazingira na wa kibunifu ili kushughulikia changamoto za kimataifa kama vile mabadiliko ya tabianchi na magonjwa ya milipuko katika kuratibu shughuli za usafiri wa baharini. Kwa kuelewa umuhimu wa bandari kwa biashara ya kimataifa na mafanikio ya Eneo Huri la  Biashara la Bara (AfCFTA), AUC inaweka kipaumbele kamili kwenye maendeleo ya mitandao safi, salama, yenye ufanisi na yenye njia nyingi zilizounganishwa.

Septemba 2023, AUC ilifanya utafiti kuhusu Ufanisi na Ushindani wa Bandari barani Afrika kwa AUCed na STC-TTIIE. AUC imeanzisha Jukwaa la Bandari zinazozingatia mazingira barani Afrika (AGPF) pamoja na mwomgozo na Mpango wa Utekelezaji wa Usafiri wa Majini wa 2024-2025 ili kuimarisha utendaji wa bandari.

Ikizingatiwa kuwa tasnia ya usafirishaji inachangia 2.85% pekee ya uzalishaji wa hewa ya ukaa duniani, inasalia kuwa muhimu kwa kufikia malengo ya mabadiliko ya tabianchi yaliyowekwa na Mkataba wa Paris. Sambamba na hili, AUC inahamasisha mifumo safi, yenye ufanisi zaidi, na inayoweza kubadilika kulingana na Mpango wa Kiafrika wa Mpito wa Nishati. Mpango huu unaunganishwa kwa urahisi katika Msimamo wa Pamoja wa Afrika juu ya Upatikanaji wa Nishati na Mpito, kuwezesha mpito mzuri kwa vyanzo vya nishati jadidifu.

## MPANGO WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU AFRIKA (PIDA): MUONGO WA KUENDELEZA MANDHARI YA MIUNDOMBINU YA AFRIKA

Lengo la msingi la Mpango wa Maendeleo ya Miundombinu barani Afrika (PIDA) ni kushinda changamoto za muungano waikanda kwa kuendeleza miundombinu ili kuleta mabadiliko katika bara zima. Kwa kukuza muungano, PIDA inalenga kuchochea biashara ya ndani ya Afrika, kuwezesha harakati za watu, na kuiweka Afrika kama mdau wa kimataifa. Kwa kupunguzwa kwa gharama za biashara na mtiririko usio na kikomo wa mtaji na talanta, PIDA inafungua njia kwa Afrika yenye mafanikio na iliyounganishwa.

Mwaka 2023, miradi ya PIDA ilibadilika kutoka kwenye kupanga hadi hatua za utekelezaji, na mingi sasa inafanya kazi, inajengwa, katika miamala ya kifedha, au inapitia maendeleo ya kimuundo. Ripoti ya kwanza ya Maendeleo ya miaka 10 ya PIDA ilizinduliwa Septemba 2023, nchini Tanzania

Ripoti hii ya Utekelezaji wa Miaka 10 ya PIDA inaakisi mafanikio ya PIDA katika muongo mmoja uliopita na imejikita kwenye mambo muhimu kwa siku zijazo. Aidha, inalenga kushiriki na kuanzisha mkakati wa kuvutia uwekezaji zaidi kuelekea maendeleo ya miundombinu ya kanda, ikilenga ufadhili wa PIDA kwa Utangamano wa Afrika.

## 2.4.2 KUONYESHA MWELEKEO: MAENDELEO YA NISHATI ENDELEVU BARANI AFRIKA

### KUWEZESHA MUUNGANO WA NISHATI: MAENDELEO KATIKA SOKO MOJA LA UMEME AFRIKA (AFSEM)

AUC imejitolea kuendeleza Soko la Umeme Moja la Afrika (AfSEM) kama mpango wenye maono unaolenga kuanzisha soko la umeme lililounganishwa na la ushindani la bara. Kwa kuzingatia matarajio ya Ajenda 2063, AfSEM inatazamia kutoa huduma za umeme salama, za kutegemewa, nafuu na endelevu kupitia soko jumuishi la umeme la bara. Muundo wa AfSEM unakuza sera, sheria na kanuni zinazooana ili kukuza biashara ya umeme ndani na miongoni mwa Nchi Wanachama.

Tangu kuzinduliwa kwake Juni 2021, AfSEM imepitia mchakato wa kina wa uchambuzi wa kina mnamo 2022, ukilenga kutathmini utayari wa kanda tofauti. Mwaka 2023, mipango ya kimkakati ilipewa kipaumbele, na kusababisha mipango ya kina ya utekelezaji iliyoandaliwa ili kushughulikia upungufu uliobainishwa, ikiambatana na utaratibu thabiti wa ufuatiliaji na tathmini.

Kwa msaada wa Umoja wa Ulaya (EU), STC-TTIIE ilipitisha ripoti hii muhimu, ikiwa ni pamoja na Ripoti ya Mpango Mkakati wa AfSEM, Mpangokazi, Mpango wa Biashara wa Miaka Mitano, Mpangokazi wa Mwaka 1, na Utaratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini wa AfSEM. Kwa kutambua umuhimu wa utekelezaji bora, STC-TTIIE pia iliidhinisha uanzishwaji wa Kitengo mahususi cha Mipango ya Kimkakati na Uratibu.

### KUKUZA MAENDELEO ENDELEVU: NAFASI YA KITUO CHA KUZUIA HATARI ZA JOTOARDHI (GRMF) AFRIKA.

AUC inakuza kikamilifu maendeleo ya kiuchumi ya bara kupitia Mfumo wa Kukabiliana na Hatari ya Jotoardhi (GRMF). Katika hatua ya kimkakati ya kuimarisha mchango wa GRMF, mpango mpya unaoitwa GRMF HEAT, unaozingatia matumizi ya moja kwa moja ya jotoardhi, umeanzishwa. Upanuzi huu unalenga kuongeza rasilimali za jotoardhi zenye kiwango cha chini cha ethalpy katika sekta za kilimo, usindikaji na ukarimu. Mpango huu unasisitiza dhamira ya maendeleo endelevu na kutafuta vyanzo mbadala vya nishati ili kukuza ukuaji wa uchumi barani Afrika.

### KUKUZA NISHATI ENDELEVU: MPANGO WA AUC KUHUSU UENDELEZAJI WA HAIDROJENI SAFI

AUC inafuatilia kikamilifu mipango ya kuinua hali ya bara katika ukuzaji wa haidrojeni safi. Kwa kutambua jukumu muhimu la haidrojeni safi katika mabadiliko ya nishati, pamoja na manufaa yanayowezekana kwa sekta kama vile usafiri wa mizigo mizito, usafiri wa anga, na utengenezaji wa bidhaa, AUC inalenga kupunguza athari za kimazingira katika nchi zote za Afrika. Juhudi hizi za kimkakati zinawiana na

malengo ya Ajenda 2063 ya UA, Ajenda 2030 ya Umoja wa Mataifa, na Mkataba wa Paris.

Kwa kutumia rasilimali nyingi za Afrika kwa ajili ya uzalishaji shindani wa haidrojeni safi, AUC ilifanya utafiti wa kina ambao unaangazia athari za kiteknolojia, kiuchumi, kijamii na kisiasa, na kuchagiza mtazamo mmoja wa Afrika kutambulisha sera na maendeleo ya mkakati. Ukisisitiza nafasi ya Afrika yenye manufaa na kulenga kuepuka hasara zozote katika kuzalisha na kufanya biashara ya haidrojeni safi, utafiti unasisitiza mchango unaowezekana katika nishati, miundombinu, na ukuzaji wa viwanda katika bara hili.

**KUHAKIKISHA UENDELEVU: MPANGO WA AUC KUHUSU MABADILIKO YA NISHATI BARANI AFRIKA**

AUC iko mstari wa mbele katika kuliongoza bara hili kuelekea mustakabali endelevu kwa kuongoza maendeleo ya Mabadiliko ya Nishati barani Afrika. AUC imeanzisha mkakati wa kina wa mabadiliko ya nishati kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Inatoa msaada muhimu kwa Nchi Wanachama wa UA katika kuoanisha maendeleo yao ya nishati na Mkataba wa Paris na Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Upatikanaji na Mabadiliko ya Nishati.

Hatua kubwa imepigwa kuhusiana na hili ni kuanzisha Kituo cha Msaada cha NDC katika Taasisi ya Nishati ya Afrika AUC (AFREC), inayofadhiliwa na Serikali ya jimbo la Flanders.

Wakati huo huo, AFREC inashughulikia Usimamizi wa Data ya Nishata inayotokana na viumbe hai barani Afrika (AFBIDM) kupitia utekelezaji wa kimkakati, ikitoa miongozo ya uratibu mzuri wa usimamizi wa data ya nishati inayotokana na viumbe hai. Aidha, Mfumo wa Ripoti za Nishati wa Afrika (AEIS) ulipata mafanikio makubwa kwa kuchapishwa kwa Mizania ya Nishati ya Afrika 2023, ikiungwa mkono na mafunzo ya kina kwa watoa ripoti wa kitaifa.

### 2.4.3 Kuvuka Mipaka ya Kidijitali: Kupiga hatua kwa Afrika katika AI, Usalama wa Mtandao, na Ustawi Unaoendeshwa na Data

**KUWEZESHA MUSTAKABALI WA DIGITALI**

AUC ni muhimu katika kuendeleza mfumo wa kidigitali kama msingi wa juhudi zake za kuimarisha miundombinu ya Afrika na kukuza maendeleo ya kiuchumi. Kwa kutambua umuhimu wa kimataifa wa akili bandia (AI), AUC imeanzisha Kikosi Kazi kuhusu AI na kuunda Rasimu ya Mfumo wa Dhana ya Mkakati wa AI wa Bara, unaochangia mijadala ya kimataifa kuhusu usimamizi wa AI.

Kuhusiana na usalama wa mtandao, AUC ilifanya tafiti ili kutathmini hatari na manufaa yanayoweza kutokea, ikapitia Mkataba wa Malabo, na kuunda rasimu ya sera kuhusu usalama wa watoto mtandaoni. Ikishughulikia upungufu wa ujuzi na uwezo, AUC inaweka kipaumbele kwenye usalama wa mtandao kwa Nchi Wanachama, ikisisitiza umuhimu wake. Utekelezaji wa mradi Policy and Regulation Initiative for Digital Africa (PRIDA) umejumuisha mafunzo kwa vijana zaidi ya 1500 wa Afrika, na kuliweka bara hili katika mijadala ya kimataifa ya usimamizi wa mtandao.

**KUIMARISHA MUSTAKABALI UNAOONGOZWA NA DATA: MIPANGO MKAKATI YA UCHUMI WA DATA BARANI AFRIKA**

Kupitisha Mfumo wa Sera ya Data ya UA mwezi Februari 2022 kuliashiria hatua kubwa ya kusonga mbele kwa AUC katika kuimarisha uchumi wa data barani Afrika. Mfumo huu, ulioidhinishwa na Baraza Kuu, unalenga kufungua faida za kiuchumi za mabadiliko ya kidigitali yanayotokana na data.

Mpangokazi wa kina umeandaliwa ili kuharakisha utekelezaji wake, ukiainisha shughuli za muda mfupi, za kati-- na za muda mrefu katika ngazi za bara, kanda na kitaifa. Jedwali linabainisha majukumu na wajibu wa wadau wakuu, ikiwa ni pamoja na AUC, RECs, Taasisi Maalumu za UA, na Taasisi za Kanda. Nchi Wanachama wa UA sasa zinaweza kutumia nyenzo za kujitathmini ili kutumia mfumo na kutambua msaada maalumu wa kitaalamu na programu za kujenga uwezo.

Kwa kutambua umuhimu wa kimkakati wa data katika uchumi wa kidigitali na mazingira ya biashara, AUC pia imeandaa "Miongozo ya Kukuza na Kuunganisha Vifungu kuhusu Data katika Majadiliano ya Protokali za Biashara ya Digitali." Mpango huu unalenga kuunga mkono mazungumzo yanayoendelea ya AfCFTA na kusimamia mtiririko wa data wa kimataifa, na kuimarisha dhamira ya AUC ya kuunda mustakabali unaotokana na data kwa bara hili.

## 2.5 HUDUMA ZA KIBINADAMU, AFYA, HIFADHI YA JAMII NA UHAMIAJI: MAENDELEO YA KIJAMII MSINGI WA AJENDA YA UA

### 2.5.1 UHIMILIVU WA HUDUMA ZA KIBINADAMU: KUTAFUTA NJIA ZA KUTATUA CHANGAMOTO ZA AFRIKA

Hali ya kibinadamu barani Afrika ni ngumu na yenye changamoto kutokana na migogoro, kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, na majanga ya asili. Hii imesababisha zaidi ya Waafrika milioni 26 kuhamishwa kwa nguvu. AUC inafanya kazi kwa bidii kushughulikia hali hii, ikioanisha juhudi za kibinadamu na mifumo ya amani na usalama, kushughulikia kwa haraka majanga husika, na kufanyia kazi masuluhisho endelevu.

Hivyo, AUC imetengeneza mpango mkakati wa utekelezaji wa 2023-2032 na utaratibu wa ufuatiliaji. Azimio la Malabo, ambalo liliwekwa kwenye Mkutano maalumu wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu masuala ya Kibinadamu na Ahadi, ni matokeo muhimu ya juhudi hii na inaonyesha dhamira ya AUC ya kushughulikia uhamiaji wa kulazimishwa. Hata hivyo, kufikia Oktoba 2023, ni asilimia 8.3 tu ya msaada wa kifedha ulioahidiwa wa jumla ya Dola 177,316,645 ndiyo umepokelewa.

Taasisi ya Afrika ya Masuala ya Kibinadamu (AfHA) inaonyesha maendeleo makubwa, na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA kupitisha katiba yake. Miundo na bajeti zilizopendekezwa zilichunguzwa na Nchi Wanachama kuhusu mageuzi ya kimuundo na fedha, na tathmini zinazoendelea zitaamua makao makuu ya kudumu. Taasisi inatazamiwa kuhamia makao makuu yake yaliyoteuliwa na Nchi

Wanachama kufikia mwishoni mwa 2024. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Waliorejea, na Wakimbizi wa ndani imefanya ziara za kutathmini hali ya kibinadamu katika Nchi Wanachama mbalimbali.

Aidha, AUC imewezesha mahudhurio katika Mkutano wa Sabini na Nne wa Kamati ya Utendaji ya Ngazi ya Juu ya Programu ya AUCer (ExCOM). Mipango ya kujenga uwezo, kama vile kurejesha Usimamizi wa Masuala ya Kibinadamu wa Afrika: Mpango wa Mafunzo ya Sheria na Sera mjini Bujumbura, Burundi, inasisitiza dhamira ya AUC ya kuimarisha uwezo wa Nchi Wanachama kwa ajili ya hatua madhubuti za kibinadamu.

### WITO WA AUC NA OCHA KUHUSU MASUALA YA KIBINADAMU DUNIANI KWA MWAKA 2024

Tarehe 12 Desemba 2023, AUC na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) ilizindua Wito wa Kimataifa wa Masuala ya Kibinadamu. Wito huo ulikuwa na lengo la kukusanya takribani dola bilioni 46 na kuokoa maisha ya takriban watu milioni 181 wanaohitaji msaada kwa mwaka 2024.

Hafla ya uzinduzi ilifanyika katika Umoja wa Afrika mbele ya Mh. Balozi Minata Samate Cessoume, AUCer anayeshulika na masuala ya afya, Kibinadamu na Maendeleo ya Kijamaa. Akihutubia hadhara wakati wa sherehe za ufunguzi, alijikita kwenye hali tata ya kibinadamu katika bara hilo, akisema kwamba "Barani Afrika, mgogoro wa kibinadamu unazidi kuwa mgumu kutokana na kuongezeka kwa ugaidi katika Sahel na Pembe ya Afrika, pamoja na athari za hivi karibuni za mabadiliko ya tabianchi kama vile mafuriko na mvua za El Nino zinazoathiri Mashariki na Kusini mwa Afrika." Hali ya kibinadamu barani Afrika ina changamoto, ambapo kuna wakimbizi milioni 7, zaidi ya nusu milioni wanaotafuta hifadhi, milioni 28 wakimbizi wa ndani na milioni 4.2 waliorejea ambao wanahitaji msaada, pamoja na watu milioni 1 wanaoishi kama watu wasio na utaifa.

• Tume ya Umoja wa Afrika ya Haki za Binadamu.
• Kamati ya Wataalamu wa Kiafrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto.
• Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa.
• Tume ya Umoja wa Afrika kuhusu Sheria za Kimataifa.
• Ofisi za Uwakilishi wa Kudumu za Umoja wa Afrika.
• Taasisi na Idara Maalumu za Kitaalamu za Umoja wa Afrika.
• Ofisi za Uhusiano za Umoja wa Afrika.

Kwa mujibu wa Uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali namba 635, Kamati za Wawakilishi wa Kudumu pia ni miongoni mwa vyombo vinavyohitaji kufanyiwa mapitio. Hii itabidi iingizwe katika mchakato wa mageuzi ya kitaasisi.

Kuhusiana na hili, AUC ilitia saini makubaliano ya kimkataba na kampuni ya ushauri ya Deloitte Central Africa mnamo tarehe 09 Februari 2023.

AUC pamoja na kampuni ya ushauri, walihudhuria mkutano wa PRC kuhusu mageuzi ya AU mjini Kigali, Rwanda kuanzia tarehe 08 hadi 12 Juni 2023 na kuwafahamisha washiriki kuhusu maendeleo kuhusu shughuli zilizosalia. Kampuni ya ushauri iliwasilisha rasimu ya ripoti yake wakati wa kurudi nyuma na kuingiliana na Nchi Wanachama.

AUC ilitoa muhtasari wa kina kwa Baraza Kuu na Mkutano wa 5 wa Uratibu wa Nusu mwaka kuhusu hatua iliyofikiwa katika mchakato wa mageuzi ya kitaasisi wakati wa vikao vyao vilivyofanyika Nairobi, Kenya, kuanzia tarehe 23 hadi 25 Julai 2023.

AUC pia ilihudhuria mkutano wa mawaziri kuhusu mpango wa utekelezaji wa miaka kumi wa Ajenda 2063 uliofanyika Kigali Oktoba 2023.

Kampuni ya ushauri ya Deloitte Central Africa iliwasilisha ripoti yake Septemba 2023. Ripoti hii ilisambazwa kwa Nchi Wanachama wa PRC tarehe 06 Oktoba 2023. Tarehe 13 Oktoba 2023, Mhe. Moussa Faki Mahamat, Mwenyekiti wa AUC, aliwasilisha ripoti rasmi ya Deloitte kwa Mwenyekiti wa PRC ili kujadiliwa kwa haraka na PRC. Katika ripoti yake, Deloitte Central Africa inapendekeza masuala matatu yafuatayo ya mageuzi ya vyombo, taasisi, wakala na ofisi zilizosalia: -

- Kuimarisha miundo ya sasa kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi jambo ambalo litapelekea gharama kubwa za kifedha kwa Umoja wa Afrika.

- Funga baadhi ya ofisi ambazo hazitumiki tena na hazifanyi kazi na uunde vituo vya huduma za pamoja. Hali hii itapunguza gharama za kifedha kwa Muungano.
- Mabadiliko ya jumla ya Muungano kwa kuunganisha baadhi ya taasisi au mashirika ambayo yana nakala au mwingiliano wa mamlaka na uundaji wa vituo vya huduma za pamoja. Hali hii itapunguza hata zaidi gharama za kifedha kwa Umoja wa Afrika.

Nchi Wanachama zitalazimika kuchagua kati ya mojawapo ya masuala haya matatu

Kazi nyingine itakayokamilishwa ni mgawanyo wa kazi kati ya Umoja wa Afrika, RECs/RMs na Nchi Wanachama. AUC ilitoa muhtasari wa mafungo ya kuwaleta

pamoja Mwenyekiti wa AUC na Wakurugenzi Wakuu wa RECs mnamo Januari 2023 huko Nairobi, Kenya. Kampuni iliajiriwa kusaidia katika kukamilisha mchakato huo. Mchakato wote utakamilika Februari 2024.

### 4.1.3 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAAMUZI YA VYOMBO VYA KISERA VYA AU

Kwa kuzingatia mwongozo wa Maamuzi ya Baraza Kuu Namba 1127 (XXXIX) kifungu cha 6, huku tukilenga kuweka msisitizo wa kuundwa kwa Kikosi Kazi cha Pamoja kwa ajili ya kufuatilia, kutathmini, na kuripoti kwa kina maamuzi ya Vyombo vya Sera, sehemu hii inachukua umuhimu mkubwa katika ripoti ya kila mwaka. Maamuzi haya yanatoa mchango muhimu katika kuchochea ushirikiano wenye tija kati ya Nchi Wanachama na AUC, kusaidia uanzishwaji wa Kikosi Kazi cha Pamoja.

Kwa kuzingatia aya (v) cha Ripoti EX.CL/929 (XXVIII), Kamisheni ilipewa jukumu, kwa kushirikiana na Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu, kuhakikisha inapitisha hatua muhimu za kuimarisha na kuanzisha mbinu za ufuatiliaji na tathmini za ufanisi kwaajili ya utekelezaji wa Maamuzi ya Vyombo vya Sera kupitia maboresho ya taratibu za ufuatiliaji. Msingi huo uliwasaidia kuelewa kiwango, asili, na ukubwa wa masuala ambayo yamekuwa zaidi ya ufuatiliaji lakini pia kujumuisha namna maamuzi yanavyopangwa na jukumu linavyogawanywa.

Kamisheni ilifanya tathmini ya hali na kuwasilisha ripoti ya maendeleo kuhusu utekelezaji wa Maamuzi ya Vyombo vya Sera vya AU kutoka mwaka 2011 hadi 2020, kwa Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu. Hii ilikuwa wakati wa Mkutano wa Mashauriano kati ya PRC na AUC mwezi Desemba 2022 huko Dakar, Senegal.

**Jedwali 1: Ripoti za Mapendekezo ya Dakar**

| Hali ya Utekelezaji | Shughuli |
|---|---|
| Zilitekelezwa | • Upanuzi wa uwakilishi wa watu wa msingi hadi zaidi ya mtu mmoja kwa kila idara / chombo;<br>• Mafunzo ya watu wa msingi<br>• Kuweka muda wa kuwasilisha miswada ya maamuzi<br>• Kuanzishwa kwa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini ingawa kina wafanyakazi wachache sana;<br>• Maandalizi ya Ripoti ya Kila Mwaka kuhusu Maamuzi ya Mwaka 2021, 2022 na 2023 |
| Zinaendelea | • Kujumuisha hali ya utekelezaji wa maamuzi kwenye Ripoti ya Mwaka ya Mwenyekiti<br>• Kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Ubia<br>• Kuandaa Mkakati wa Kuboresha Rasilimali watu |
| Hazikutekelezwa | • Kuandaa mkakati na muongozo wa kutafuta rasilimali kwaajili ya utekelezaji wa Maamuzi<br>• Utafiti juu ya athari za kifedha za maamuzi<br>• Kuandaa mwongozo wa usimamizi wa matokeo ya kutotekelezwa kwa Maamuzi |

| | |
|---|---|
| | • Kuweka ushirikiano na idara kama hizo katika Umoja wa Mataifa<br>• Uainishaji na kategoria ya Maamuzi ya Vyombo vya Sera vya AU<br>• Ripoti za robo mwaka na Menejimenti kwa Nchi Wanachama<br>• Kuandaa Mwongozo wa Uundaji wa Maamuzi<br>• Kuandaa kiolezo cha kuripoti Mikutano wa Vyombo vya Sera vya AU yote. |

Mbali ya mapendekezo ya Dakar yanayolenga kuboresha ufanisi wa kusimamia maamuzi ya vyombo vya sera, maamuzi mengine yanayolenga kufikia matokeo ni pamoja na Uamuzi wa Baraza Kuu EX.CL/Dec.898(XXVIII) unaoelekeza Kamisheni kwa kushirikiana na Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) kuhakikisha:

- Maamuzi yaliyopendekezwa na Kamisheni hayazidi matatu (3) kwa kila Idara na pia kuhakikisha utekelezaji kamili ndani ya kipindi cha kuripoti kabla ya maamuzi mengine kuchukuliwa juu ya suala hilo.
- Ajenda ya Mkutano Mkuu na maamuzi yamepangwa kwa mantiki ili kushughulikia masuala ya kimkakati badala ya masuala ya utawala.
- Rasilimali za kifedha za kutosha zimepangwa kuwezesh Kamisheni kutekeleza kikamilifu maamuzi ya Vyombo vya Sera;
- Kupitishwa kwa hatua muhimu za kuimarisha na kutumia kwa ufanisi mbinu za ufuatiliaji na tathmini kwaajili ya utekelezaji wa maamuzi ya Vyombo vya Sera kupitia maboresho ya kanuni za ufuatiliaji.
- Maamuzi yaliyopitishwa yanaripotiwa mara moja kwa mwaka ili kutoa muda wa kutosha wa utekelezaji na kwamba Kamisheni na Nchi Wanachama zifanye hivyo.
- Rasilimali za kutosha zinatengwa ili Kamisheni iharakaishe kuajiri wataalamu waliofuzu kwa wakati.
- Maamuzi ambayo hakuna hatua zinazochukuliwa baada ya miaka miwili (2) au mitatu (3) yanapendekezwa kufutwa na vyombo vya sera;
- Utekelezaji wa maamuzi yanayohitaji fedha kutoka kwa washirika unapunguzwa na kwamba Nchi Wanachama za AU zitoe michango yao kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa maamuzi.




NB – 5 % of actions fully implemented, 2% of actions partially implemented and 93% not implemented

KIELELEZO CHA 4 – MAAMUZI YA 2021 - 2023

Hakuna uhusiano wa wazi kati ya maamuzi, mkakati, sera, miundo, na rasilimali ambayo inaathiri kiwango cha utekelezaji hivyo kuna haja ya kurekebisha mchakato wa kufanya maamuzi kama ilivyoelezwa kwenye muongozo wa mchakato:

:




KIELELEZO CHA 1 - MPANGO ULIOPENDEKEZWA WA KUPITISHA MAAMUZI

## 4.1.4 KUJENGA MSHIKAMANO WA KIMKAKATI

Kwa lengo la kufikia umoja na mshikamano wa kimkakati ndani ya AU, Kamisheni ya Umoja wa Afrika ilianza kubuni Mpango Mkakati wa Miaka 5 kama ilivyoainishwa katika Uamuzi wa Ex. Cl 1217 (XLIII). Mpango Mkakati wa Umoja wa Afrika (2024 - 2028) unawekwa ndani ya muktadha wa Mpango wa STYIP wa Ajenda 2063. Moja kwa moja unalingana na msingi mkuu - Maono, Shabaha na matarajio saba 'Moonshots' kwa kuzingatia maadili ya AU. Maandalizi yake yalianzishwa mwezi Julai 2023 kwa uteuzi wa Wataalamu wa Masuala ya Kitaalamu kutoka Idara na Mashirika yote ya Umoja wa Afrika. Baadaye, mafunzo ya Wataalamu wa Masuala ya Kitaalamu kuhusu dhana ya Kadi ya Alama Iliyosawazishwa yalifanyika ikifuatiwa na mikutano mingi ya mashauriano, vishirikishi na vilevile vya mkakati ili kutoa mwelekeo wenye ufahamu na matarajio kama sehemu ya mkakati. Mpango huo unaonyesha mlinganisho wa programu za Mashirika ya Umoja wa Afrika ndani ya majukumu yao husika kulingana na Mtazamo wa Kadi ya Alama Iliyosawazishwa. Mtazamo huo unajumuisha wafaidika, michakato bora na ya ufanisi ya msingi wa Umoja wa Afrika, uwezo bora wa kibinadamu na kielekezi cha taasisi, na ufadhili endelevu na unaoweza kutabirika. Hivyo basi, kubuniwa kwa Malengo ya Mkakati katika Mpango Mkakati wa Kitaasisi.

### 4.1.5 KURASIMISHA MFUMO WA USIMAMIZI UNAOZINGATIA MATOKEO WA AU

Mwaka 2023 ulishuhudia maendeleo yaliyofikiwa katika vipengele vifuatavyo; Kukuza umoja wa kimkakati na umakini ndani ya AU yote; Kufanya mageuzi kuelekea RBM (Usimamizi unaozingatia Matokeo); Kuboresha mazingira kwaajili ya utekelezaji wa majukumu muhimu na maamuzi ya vyombo vya sera; Kuimarisha uwezo wa kibinadamu na kitaasisi; Kuongeza ufanisi wa operesheni kupitia utoaji wa huduma, mageuzi ya kidijitali, usimamizi wa mali, afya,na usalama; Kuhakikisha ufadhili endelevu na unaoweza kutabirika; na Usimamizi wa ubia.

Kuhamia kwenye Usimamizi unaozingatia Matokeo na maendeleo ya moduli za Usimamizi wa Mchakato wa Taasisi ni sehemu ya mchakato wa mageuzi ya ufanisi ili kufanikisha mageuzi hayo. Umoja wa Afrika kwa miaka mingi umekuwa na shauku ya kutimiza majukumu yake ndani ya mazingira yanayotokana na matokeo yaliyopangwa vizuri lakini haukufanikiwa.

Uamuzi wa Baraza Kuu wa 2023 wa Utekelezaji 1217 (XLIII) ulisisitiza umuhimu wa kuanzisha RBM ikuongozwa zaidi na mwelekeo kwamba RBM inapaswa kuwa msingi wa mzunguko wa bajeti ya miaka mingi.

Uongozi uliweka mazingira ya mpito kuwa ni mfululizo wa hatua ndogo kuelekea mageuzi ya mwisho, ambayo yatafanyika kwa muda mrefu. Katika mchakato huu wa mifumo, Kamisheni ilianza kuandaa mafunzo ya RBM na Usimamizi wa Mchakato wa Pamoja katika Mifumo ya Usimamizi wa Maarifa.

### 4.1.6 NYENZO ZA UBUNIFU KWA AJILI YA KURATIBU UENDESHAJI

Kuongeza ufanisi na kugawa rasilimali kimkakati, Kamisheni ya Umoja wa Afrika ilianza safari ya mageuzi ili kuoanisha mifumo na athari. Mabadiliko ya kimfumo yalizinduliwa, yakionekana wazi kwa kuanzishwa kwa zana mbalimbali za mkakati wa utekelezaji:

- **Kikao kazi cha Kabla ya Bajeti:** Kamisheni ya Umoja wa Afrika iliandaa kikao cha maandalizi kikiwashirikisha idara mbalimbali za Umoja wa Afrika, Mashirika Maalumu, na Ofisi. Lengo lilikuwa wazi - kubadilisha kikamilifu mchakato wa bajeti. Hatua hii ya mkakati ililenga kusawazisha maoni ya bajeti na kuhakikisha kufuata kanuni kama vile ukamilifu na mlinganisho na mipaka iliyopendekezwa. Kufichua masuala muhimu kama vile upitishaji maradufu, na pengo la mamlaka, na kutofuata mlinganisho wa Mwongozo wa Bajeti ilikuwa muhimu katika kushughulikia chanzo cha matatizo ya utekelezaji wa bajeti. Hatua hii ya maono ya mbali ililenga ubunifu wa kimkakati ili kuandaa mkutano kuu wa bajeti wa AU, kukuza mabadiliko ya kina katika mchakato wa bajeti.
- **Mkutano wa Kila Mwezi wa Uratibu wa Uendeshaji wa Wadhamini wote wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika:** (ingiza picha) Mikutano hufanyika ili "kuongoza uratibu wa uendeshaji kote barani Afrika" na "kuwaandaa Wadhamini wa Huduma na Wadhamini wa Huduma kukagua na kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mpango kazi na malengo ya utendaji wa kila mwaka wa Kamisheni." Wanatumika kama jukwaa la kufanya kazi kwaajili ya kuratibu wa uendeshaji, kubadilishana habari, kuongeza ufanisi, na kuepuka upitishaji mara mbili. Mbali na maandalizi ya mikutano ya Kamisheni na ufuatiliaji wao, pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maamuzi ya vyombo vya sera, mikutano ya kila mwezi ya uratibu wa uendeshaji husaidia kuoanisha mipango ya shughuli za Idara za Kamisheni ya Umoja wa Afrika na kukagua shughuli zinazohusisha Idara kadhaa ili kuoanisha utekelezaji na taarifa zao. Jukwaa hili lilizinduliwa mwaka 2022 na kuongezeka kwa mashirika yote na ofisi mwaka 2023 ili kuhakikisha mfumo wa ushirikiano ndani ya AU kote.

⇨ ***Tuvuti maalumu ya Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu (ODG portal):*** Zana hii inarahisisha mtiririko wa habari ndani ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Inawezesha ufuatiliaji, na sasisho kwa wakati unaofaa. Tuvuti ya (Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu) pia ina jukwaa la maarifa ambapo nyaraka muhimu zilizotengenezwa ndani ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika zinaweza kupatikana.

⇨ ***Tuvuti maalumu ya ufuatiliaji wa taarifa za kimataifa:*** Pamoja na Tuvuti ya Mkurugenzi Mkuu, Tuvuti ya Kimataifa inawezesha upatikanaji wa habari unaosasishwa moja kwa moja uliotengenezwa na Idara ili kusaidia usimamizi wa juu na uongozi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika katika kufanikisha upatikanaji wa habari zinazohusu bajeti, ukaguzi, rasilimali watu, ushirikiano, Ajenda 2053 na utekelezaji wa maamuzi. Kila tuvuti husika inasimamiwa na idara husika. Kwa vyovyote vile, tuvuti hiyo ya kimataifa huunda kiungo moja kwa moja kwa kila moja na kumpa msomaji mtazamo wa kimataifa ambapo habari tofauti zote zinapatikana kwenye jukwaa moja. Tuvuti hiyo ya Kimataifa

inalenga kuwezesha tathmini ya mageuzi na kazi ya Umoja wa Afrika kwa kufuatilia viwango vya utekelezaji, viwango vya utendaji, ukaguzi, na utekelezaji wa KPI ya maamuzi.

- ***Kalenda ya Matukio ya Kimataifa:*** Pia imejumuishwa katika Tuvuti ya Mkurugenzi mkuu, Kalenda ya Matukio ya Kimataifa inalenga kutoa maono ya kimataifa juu ya matukio makubwa yanayokuja, iwe yameandaliwa na Kamisheni au na taasisi nyingine za kimataifa.

### 4.1.7 KUIMARISHA UHUSIANO NA JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KIKANDA ZA AU NA AUDA-NEPAD

Ikumbukwe kuwa uhusiano kati ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC) na Jumuiya za Ushirikiano wa Kiuchumi (RECs) unasimamiwa na Makubaliano Rasmi (MOU). Ushiriki wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika unaratibiwa katika ngazi ya Mwenyekiti ambaye anaongoza Kamati ya Ushirikiano kama ilivyoelezwa katika MOU hiyo. Wakati ikitekeleza jukumu lake katika mwaka 2023, Kamati ya Ushirikiano ilifanya kazi kupitia Katibu wake ili kuhakikisha utekelezaji wa pamoja wa ajenda ya kuiunganisha Afrika kulingana na Mkataba wa Abuja na kuandaa Mkutano wa Tano wa Kati wa Ushirikiano (Mkutano wa Julai). Mwenyekiti pia alishiriki binafsi Mikutano ya Kila Mwaka ya Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (REC).

Katika kipindi kilichofanyiwa mapitio, 2023, Mwenyekiti aliongoza mara kwa mara mikutano ya Wakuu wa Mtandao wa Jumuiya za Ushirikiano wa Kiuchumi katika muktadha wa Kamati ya Ushirikiano. Mikutano yote ya Kamati ya Ushirikiano ilifuatiwa na mikutano ya Katibu wa Ushirikiano ambayo inajumuisha Maafisa Wasio Watendaji wa Idara muhimu za Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Maafisa Wasio Watendaji wa Jumuiya za Ushirikiano wa Kiuchumi za Kikanda na AUDA-NEPAD. Mikutano hii kwa kawaida inategemea mazungumzo, mashauriano, ufuatiliaji, tathmini, na taarifa kuhusu ajenda ya kuiunganisha kikanda na bara. Kufuatia mikutano hii ya mashauriano, Kamati ya Ushirikiano iliandaa ajenda ya Mkutano wa Kati wa Mwaka. Zaidi, Nchi Wanachama pia wanashiriki kuandaa Ajenda kupitia Kamati ya Mawaziri.

Ajenda ya Mkutano wa Kati wa Mwaka wa 2023 ilikuwa kama ifuatavyo:

- Ripoti kuhusu Hali ya Utangamano wa Afrika (Hii ilijumuisha Ripoti ya Mwenyekiti wa AUC pamoja na Wenyeviti wa kila REC/RM na AUDA-NEPAD.
- Kuzingatia na kupitisha Mgawanyo wa Kazi wenye Ufanisi kati ya AU, RECs/RMs na Nchi Wanachama katika sekta zilizosalia.
- Mafanikio ya Kati ya REC katika ajenda ya Umoja wa Afrika.
- Ripoti za Vinara wa AU na Marais.
- Ripoti ya Mkutano wa Sera wa Pili wa Kubadilishana Maarifa wa AU kati ya Kanda (I-RECKE) na uzinduzi wa Kituo cha Afrika kusaidia Mabadiliko ya Kuingiza (AFSIT), jitihada za ushirikiano kati ya AUC na Programu ya

Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) yenye lengo la kusaidia mipango iliyojumuishwa kwa nchi za Afrika zinazopitia mabadiliko ya kisiasa yenye utata.

- Azimio la Mkutano wa Kati wa Mwaka.

Shughuli zote hizi na mafanikio katika kuimarisha shughuli za AU ziliwasilishwa kwenye Mkutano wa Tano wa Kati wa Ushirikiano, uliofanyika Nairobi tarehe 17 Julai 2023. Mkutano huo ulihudhuriwa na idadi kubwa ya Marais wanaowakilisha Uenyekiti wa Jumuiya za Ushirikiano wa Kiuchumi za Kikanda (RECs) na Bodi. Baadhi ya Marais walitoa ripoti za masuala ambayo wanashughulikia.

Mapendekezo mengi yaliyotolewa yanayojumuisha maeneo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya kiuchumi, kukuza utangamano wa bara la Afrika, kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Uchumi wa Buluu, Amani na Usalama na haja ya kuhitimisha Mgawanyo wa Kazi kati ya AU, RECs/RMs na Nchi Wanachama. Mapendekezo haya yanapatikana katika Azimio la Mkutano wa Kati wa Mwaka wa Julai 2023 Ref. **MYCM/AU/Decl.(V).**

## 4.2 KUFADHILI UMOJA WA AFRIKA

Katika kipindi cha miaka saba ya Mageuzi ya Taasisi ya Umoja wa Afrika (AU), suala la ufadhili endelevu na unaoweza kutabirika wa Umoja linaendelea kuvutia umakini /usikivu. Maboresho yamefanyika kwa malipo ya michango ya Nchi Wanachama kufanywa kwa wakati, kwa sehemu kutokana na utekelezaji wenye ufanisi wa utawala wa vikwazo katika suala hili. Uendeshaji wa Mfuko wa Amani ulioboreshwa pia umepiga hatua vizuri. Kwa bahati mbaya, baadhi ya maeneo yamekwama. Kielelezo kizuri ni idadi ya nchi zinazotekeleza ushuru wa 0.2%, ambao haujabadilika kabisa kwa miaka mitatu iliyopita. Leo hii, ni nchi 17 tu zinazozingatia uamuzi kuhusu ushuru wa 0.2%.

### 4.2.1 HALI YA BAJET YA AU

Kufikia tarehe 31 Desemba 2023, jumla ya makusanyo kutoka Nchi Wanachama kwaajili ya bajeti ya kawaida yalifikia $181,210,996.23.704 sawa na 88% ya mchango wa jumla wa Nchi Wanachama kwenye bajeti ya kawaida ya mwaka 2023. Kiwango kile kile cha ukusanyaji cha 88% kiliripotiwa mwaka 2022 pia.

Ukusanyaji wa malimbikizo ya bajeti ya kawaida ulifikia $31,655,131 sawa na 28% ya jumla ya malimbikizo. Hii inaongezeka kwa 3% ikilinganishwa na 25% iliyoripotiwa mwaka 2022. Ongezeko hili linachangiwa, kwa sehemu, na juhudi za ufuatiliaji zilizofanywa na Kamisheni ikiwa ni pamoja na kutuma barua za ukumbusho ya robo mwaka kulingana na Sheria za Fedha za AU na barua zaidi za kumbusho na simu zilizofanywa kwa Nchi Wanachama walio na malimbikizo na wale walio kwenye mipango ya malipo.

Mfumo wa Tathmini wa Umoja wa Afrika uliotumika kwa kipindi cha 2020-2023 uliidhinishwa na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Kawaida wa Baraza Kuu mwezi Julai 2023 kwaajili ya kutumika kuanzia kwenye mzunguko wa mfumo wa tathmini kutoka mwaka 2024 hadi 2026.

Mwaka 2023 ulikuwa mwaka mwingine wa kubana matumizi. Michango ya Nchi Wanachama, ambayo imepunguzwa hadi $250 milioni kwa muda wa kati, kwa kweli ilipunguzwa zaidi, hadi $202 milioni (na tena hadi $200 milioni kwa bajeti ya 2024). Hii imeleta changamoto kwa kuwa majukumu, matarajio, na uanzishwaji wa taasisi mpya, haujapungua kamwe. Kama matokeo, utendaji wa Umoja dhidi ya ahadi ya Johannesburg ya kujifadhili kwa 100%, 75%, 25% kwenye uendeshaji, programu, na operesheni za kusaidia amani unazorota. Ingawa Umoja unafadhili operesheni zake kwa 100%, mchango wake kwenye bajeti ya programu umepungua hadi 12% (taasisi za bara la Afrika kama vile AfDB na Benki ya Afrexim hazijumuishwi). Kuamilishwa kwa Kituo cha Akiba cha Majanga cha Mfuko wa Amani na idhini ya miradi ya majaribio chini ya programu ya Mfuko wa Amani ilipeleka ishara chanya na inapaswa kuendelezwa.

Ongezea majedwali mawili ya buluu hapa

### 4.2.2 USHIRIKIANO NA F15

Kama ilivyotakiwa kupitia Maamuzi ya Vyombo vya Sera, Kamisheni ya Umoja wa Afrika ilisaidia ushiriki kamili wa Wataalamu wa F15 kwenye mchakato wote wa maandalizi ya bajeti ya 2024 na shughuli za uangalizi zilizofanywa kupitia Vikao vya Pamoja na Kamati za Kamisheni ya Sera za PRC ya Usimamizi Mkuu na Ushirikiano wa Masuala ya Bajeti ya Fedha na Utawala, Masuala ya Ukaguzi na Miundo. Kamisheni pia ilisaidia ushiriki wa Mawaziri wa F15 kupitia mikutano ya kisheria. Ni matumaini ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuona Mawaziri wa Fedha wanashiriki kwa bidii zaidi mikutano ya Baraza Kuu ya Bajeti iliyopangwa mwezi Julai kila mwaka kulingana na Uamuzi wa Kikao cha Utekelezaji 635.

### 4.2.3 UTEKELEZAJI WA TOZO YA 0.2%.

Tangu kupitishwa kwa Uamuzi wa kuanzisha tozo ya 0.2% ya uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi mwezi Julai 2016, Nchi Wanachama zimetaja changamoto mbalimbali zinazohusiana na utumikaji wake wa ndani au utekelezaji mzuri ambao unaweza kugawanywa katika makundi matatu: (i) kutimiza ahadi zilizotolewa chini ya mifumo biashara baina ya nchi na nchi nyingi. (ii) vikwazo kutokana na masharti ya kitaifa, sheria, kanuni na masharti ya katiba na (iii) mifumo dhaifu ya utekelezaji wa ndani.

Katika azma ya kuunga mkono Nchi Wanachama katika kukabiliana na changamoto hizi, Kamisheni ilifanya mwaka 2023 mfululizo wa mashauriano yakiwemo vikao viwili vya kazi, kimoja na Sekretarieti ya AfCFTA na kingine na Tume ya ECOWAS kwa lengo la kuchunguza njia ambazo Nchi Wanachama zinaweza kushinda. changamoto zinazohusiana na mikataba ya kimataifa kupitia makubaliano ya AfCFTA, na vile vile, kuongeza idadi ya nchi zinazotekeleza tozo hiyo kupitia jukwaa la jumuiya ya kanda, mtawalia.

Mkutano na Sekretarieti ya AfCFTA ulilenga kuchunguza njia mahususi na taratibu ambazo Nchi Wanachama wa AU zinaweza kutekeleza tozo hiyo kwa njia bora zaidi katika muktadha wa uanzishwaji wa AfCFTA au FTA za kanda au maeneo ya forodha. Hii inaweza pia kujumuisha kufafanua na kuelewa taratibu zinazohitajika, kwa Nchi Wanachama kutoa taarifa ya tozo ya 0.2% kwa Shirika la Biashara Duniani (WTO), na kujadiliana kuhusu marekebisho ya ushuru, ikiwa itaonekana kuwa muhimu.

Mkutano na Tume ya ECOWAS ulitaka kuelewa vyema mbinu zilizopo sasa za kutekeleza Ushuru wa Jumuiya ya ECOWAS, na kwa upande mwingine, ushirikiano unaowezekana na AUC kwa wafuatao kurudisha majukwaa yaliyopo ya utekelezaji wa tozo ya asilimia 0.2. Hii inaweza kusababisha makubaliano kati ya AUC na ECOWAS kuhusu kuongezwa kwa tozo ya 0.2% kwa mifumo yake ya kukusanya rasilimali, kama njia ya kuchangisha fedha kwa ajili ya UA.

Aidha, AUC ilifanya majadiliano ya mashauriano na Nchi moja Mwanachama ambayo imetekeleza kwa ufanisi tozo hiyo, na kushirikiana na mamlaka husika za serikali zinazohusika na utekelezaji wa tozo ya asilimia 0.2 ya tozo ya bidhaa kutoka nje ya nchi, kwa madhumuni ya kubadilishana uzoefu na mbinu bora, ambazo Nchi Wanachama zinaweza kusaidiwa kurekebisha mbinu zao za utekelezaji.

Ni dhahiri Umoja wa Afrika haufanyi vizuri kwenye tozo ya 0.2%. Bado kuna fursa za kutoa msukumo kwa suala hili, ambalo litaongeza uwezekano wa kutabirika katika kufadhili Umoja wa Afrika huku zikizipa Nchi Wanachama wake mkakati mzuri wa usimamizi wa ukwasi.

### 4.2.4 KUELEKEA VYANZO BUNIFU VYA FEDHA

Kwa kuzingatia vikwazo vya kijamii na kiuchumi vinavyozikabili Nchi Wanachama lakini pia kwa kuzingatia ongezeko la mahitaji ya kifedha ya AU ambayo yangeiwezesha kukabiliana na changamoto zinazoongezeka kwa kubuni vyanzo fanisi vya fedha kama vile sekta binafsi, taasisi, wasamaria wema, raslimali za ndani ya nchi n.k.

### 4.2.5 KUBORESHA UKAGUZI WA AU

**USIMAMIZI WA NDANI**

Mpango wa Mwaka wa Ukaguzi wa mwaka 2023 ulikuwa na miradi 64 ya ukaguzi inayojumuisha Makao Makuu na Ofisi za Nje ya Makao Makuu (yaani, Vyombo vya AU, Ujumbe wa Uwandani, Ofisi za Kanda, za Uwakilishi na Ofisi Maalum). Kufikia tarehe 17 Oktoba 2023, mradi 38 ilifanywa na OIO, ikiwemo maombi kutoka kwenye utawala ambayo hayakuwa kwenye mpango ulioidhinishwa mwaka 2023. Miradi hii iko kwenye hatua mbalimbali za kukamilisha (taarifa ya maendeleo/mwaka/rasimu). Kitengo cha Uchunguzi chini ya OIO pia kimefanya uchunguzi sehemu tatu tangu

mwaka 2022 na kumalizia mwaka 2023. Aidha, kati ya maombi tisa (9) ya uchunguzi yaliyopokelewa mwaka 2023, matatu yamepangwa kuanza katika robo ya nne ya mwaka 2023. Kwa upande mwingine, shughuli nne za kuwaendeleza watumishi wa ukaguzi zilifanyika mwaka 2023. Athari za jumla za shughuli za ukaguzi za AUC kwa kipindi kinachoondelea ni pamoja na zifuatazo:

- ripoti za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi hiki kilisaidia utawala katika kufanya mapitio katika ufuatiliaji na kuhakikisha kwamba ufuatiliaji thabiti unaendelezwa.
- ripoti za ukaguzi zilizoshirikishwa kwa Bodi ya Wakaguzi wa Nje wa AU (BOEA) ziliokoa muda na gharama zinazotumika katika kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha.
- ripoti za uthibitisho zilizoshirikishwa kwa Washirika ziliwafanya waendelee kutoa fedha na kutoa uhakika kuhusu matumizi ya fedha ambazo zilizokwishakutolewa.
- shughuli za kuendeleza watumishi zimeiwezesha watumishi wa AUC kujua mambo mapya katika taaluma yao. Hii imeendelea pia kuimarisha utendaji wa watumishi wa AUC pamoja na ukaguzi wa jumla wa AUC.
- Matokeo ya ukaguzi unaotakiwa kisheria yaliwasilishwa na Vyombo vya Sera, na maamuzi yalifanywa na kupitishwa ili kuimarisha uthibiti na usimamzi wa raslimali wat una raslimali fedha za Umoja wa Afrika.

## BODI YA WAKAGUZI WA NJE (BOEA)

Bodi mpya iliyoteuliwa na Baraza Kuu wakati wa Mkutano Mkuu wa Julai 2022 imesimikwa, na SAI Egypt aliteuliwa kuwa mwenyekiti, na kuchukua majukumu kuanzia Januari 1, 2023.

- AUC na Vyombo 10 vya AU vilikaguliwa. Wakaguzi 47 kutoka kwenye Bodi za Wakaguzi wa Nje za Nchi Wanachana zilipewa kazi ya kukagua AUC na Vyombo vyake.
- Bodi iliidhinisha taarifa ya ukaguzi wa nje tarehe 26 Mei 2023. Taarifa hiyo ya ukaguzi kuhusu taarifa za fedha na barua ya usimamizi vimewasilishwa kwa uongozi wa Umoja wa Afrika na nchi zote wanachama.
- **Mafanikio:** Ukaguzi wa nje wa lazima kwa AUC na Vyombo vyake ulihitimishwa kama ulivyopangwa, na ukomo wa muda uliwekwa kwenye Sheria za Fedha. Kuwasilisha taarifa za fedha kwenye Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka wa Fedha kwa PRC tarehe 31 Mei, 2023.
- Kwa kuongezea ukaguzi nje wa lazima wa mwaka wa AU, BoEA inatekeleza maombi maalum ya ukaguzi yaliyotolewa na Baraza Kuu.

## KAMATI YA UWAJIBIKAJI WA NDANI YA (IAC)

Kamati ya Uwajibikaji wa Ndani (IAC) ilihuishwa mwaka 2023 na ilifanya mikutano kadhaa, pamoja na kuchukua hatua kadhaa kufuatilia mapendekezo yote ya ukaguzi na kupendekeza hatua za kuchukua kwa uongozi wa juu wa AUC.

## 4.3 UFANISI WA UTENDAJI

### 4.3.1. UWAJIBIKAJI KATIKA UTOAJI HUDUMA

Wakati wa kutoa taarifa, AUC iliharakisha jitihada zake katika kuboresha utoaji huduma, kufanya michakato muhimu kujiendesha yenyewe, na kufanya mageuzi ya kiteknolojia na kidijitali kujenga mifumo ya kisasa na himilivu katika huduma mtambuka.

Kuhusu ufanisi, AUC imechukua hatua muhimu kushughulikia madhaifu na utendaji duni ambao unaathiri utoaji huduma. Hatua kama vile Makubaliano ya Viwango vya Huduma (SLAs) na *Dashbodi* ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu, miradi na shughuli zimechukuliwa.

### 4.3.2. TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

Mwezi Machi 2023, kulikuwa na shambulio katika mfumo wa Umoja wa Afrika. Kwa msaada wa INTERPOL na Benki ya Maendeleo ya Afrika, tuliweza kurejesha mfumo bila kulipa fidia. Kushambuliwa kwa mfumo huo ilikuwa ni ishara ya kuwa macho zaidi na kulikuwa na mambo mazuri ndani yake. Ilikuwa ni fursa kwa Umoja wa Afrika kuona haja ya kutoa kipaumbele katika uwekezaji kwenye TEHAMA hata katika nyakati za hali mbaya kiuchumi. Manunuzi makubwa ya mwisho kwa ajili ya kubadilisha vifaa vya TEHAMA kwa wafanyakazi yalikuwa mwaka 2015. Shambuli la mfumo pia liliharakisha hatua zetu katika maeneo manne ya Usimamizi wa TEHAMA; Mageuzi ya Kitaasisi Kigijitali; Kujenga Uwezo katika TEHAMA; na Kuimarisha uwezo kwenye TEHAMA.



Mafanikio makubwa katika maeneo haya wakati wa kutoa taarifa yalijumuisha:

Chini ya Utawala na Usimamizi wa TEHAMA ili kuhakikisha Uwajibikaji na Kuona Thamani, tukio la bahati mbaya la kushambuliwa kwa mfumo wakati wa robo ya kwanza ya mwaka 2023, lilihuisha haja ya taasisi ya kutoa kipaumbele kwa usalama wa mtandao. Katika hili, AU ilichukua hatua za kuimarisha miundombinu yake muhimu ya TEHAMA. Kwa hiyo, kampuni mahiri iliteuliwa kwa kufuata mchakato shindani wa kandarasi kufanya uchambuzi kiutendaji, malengo ya biashara na mahitaji ya kiusalama, tathmini ya awali ya Usalama wa mtandao ya Miundombinu yake ya TEHAMA, kutengeneza mkakati wa usalama mtandaoni, pamoja na ramani ya utekelezaji wa usalama mtandaoni.

Ili Kuharakisha Mageuzi ya Kidijitali kwa kutumia miundombinu ya kisasa, kujumuisha mifumo, usalama wa data, mwaka 2023, AU ilipata msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kubadilisha vifaa 1,200 ambavyo muda wake wa matumizi ulikuwa umekwisha. Aidha, kwa msaada wa Benki ya Dunia, ukarabati wa kituo cha *AUC Data Centre* ulikamilishwa, ambacho kitaimarisha matumizi, mifumo na uwezo wa kutunza data wa kituo hicho kwa zaidi ya 100%, na kuhakikisha uwezo wa kujitegemea na ulinzi wa data. Mabadiliko ya mfumo wa *Data Centre Firewall* pia uliimarisha Mifumo ya Kituo cha Data Centre na usalama wa *seva*. Hii itahakikisha kuendelea kwa biashara na usalama endapo mfumo utashambuliwa. Hii pia itasadia kutoa uhakika wa kuboresha upatikanaji wa huduma, matumizi na mifumo. Kituo cha AUC cha *Data Centre* kinaweza kuhudumia mahitaji makubwa ambayo yanatokana na michakato ya biashara inayojiendesha na kuhifadhi data na taarifa za taasisi, pamoja na kukidhi mahitaji ya Nchi Wanachama ambazo zitahitaji kulingana na vigezo vilivyowekwa. Kamisheni inajiandaa kuzindua kituo kipya cha AUC cha *Data Centre* ifikapo mwezi Machi 2024. Utekelezaji wa *Africa CDC Data Centre* pia umekamilika, ambacho kitaiwezesha CDC Afrika kuhodhi mifumo inayojitegemea na iliyo salama na matumizi ambayo yaifanya biashara ya CDC Afrika kujiendesha yenyewe.

Kuhusu kujenga uwezo wa TEHAMA kuwawezesha watumishi wa AU kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya taasisi, ujanja wa biashara na kufanya michakato ijiendeshe ni mambo yaliyoboreshwa na kurahisisha upatikanaji wa nyaraka, kuwepo muda wote, kupunguza muda unaotumika kuunda nyaraka, kutunza mafaili na kuchapisha, kupunguza gharama na dosari za kibinadamu, na kuboresha usalama wa nyaraka. Kwa hivyo, Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Taasisi (ESM) ulitumika ambao husaidia katika kuunda, kupanga na kutekeleza huduma, ikiwemo huduma saidizi za TEHAMA, Ralimali Watu, Vifaa na huduma kwa wateja. Vilevile, Mfumo wa Usimamizi wa Maamuzi (DIMS), nyenzo ya kidijitaki kwa ajili ya kufuatilia hali ya maamuzi mbalimbali na hatua zilizochukuliwa kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya AU vya sera uliundwa ili kuimarisha mchakato wa kushughulikia matokeo ya ukaguzi. Hatua kadhaa za kuimarisha SAP zilichukuliwa kufanya michakato ijiendeshe yenyewe, kutoa fomu na kutengeneza ripoti, na kudhibiti maeneo muhimu, ikiwemo kukamilisha Awamu ya kwanza ya SAP na AMERT.

Kuhusu kuimarisha uwezo katika TEHAMA, Kamisheni ilipata huduma za kampuni mahiri kufanya mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu usalama mtandaoni kwa ni suala kubwa linaloathiri Miundombinu ya TEHAMA ya Umoja wa Afrika, uendeshaji, na

umaarufu wake. Tumebainisha mapengo kadhaa na mahitaji ya ujuzi na stadi kwa watumishi katika maeneo ya Usalama, Utawala, Usimamizi wa Athari viwango vya ISO na mafunzo mengine ya kiufundi. Hii nia pamoja na MIS Staff Adopted ITIL, COBIT na Utendaji Bora wa ISO27000 kwa watumishi wa idara ya TEHAMA kaika maeneo ya *Cyber Security COBIT, ITIL na CompTIA.*

### 4.3.3. NYARAKA NA MIKUTANO

Katika kipindi cha kuripoti, Kamisheni iliendeleza zaidi dhamira yake ya kufanya Mikutano na kuhifadhi nyaraka kunakozingatia mazingira na, kama inavyoonyeshwa na mikakati na miradi kama vile; kupanua matumizi ya tovuti ya eConferencing kwa aina zote za mikutano (ya ana kwa ana, ya mseto, iwe imeandaliwa na UA au nchi yoyote mwenyeji) kwa upatikanaji wa nyaraka bila kutumia karatasi; ujumuishaji wa mfumo wa mkutano na jukwaa la Zoom kwa tafsiri ya moja kwa mmoja; kuanzishwa kwa mashine mpya ya kisasa ya uchapishaji ya kidijitali ambayo ni rafiki kwa mazingira na vifaa vya kumalizia uchapishaji ambavyo vinaweza kutoa machapisho yote ndani ya jengo, na tovuti iliyoboreshwa ya Conference-web ambayo husaidia katika kukusanya maombi ya mikutano na kalenda ya mikutano ili kuboresha upangaji wa mikutano

### 4.3.4. USIMAMIZI WA MALI

Umoja wa Afrika uliendelea na juhudi katika matumizi bora ya rasilimali zake kwa kuhakikisha unakamilisha ujenzi na matengenezo ya majengo kwa wakati. Hivyo, kazi za ujenzi wa ofisi mpya za Africa CDC na maabara zilikamilishwa na Africa CDC imeanza kutumia maabara hizo. Mradi sasa uko chini ya kipindi cha ushirikiano wa kitaalamu cha miaka 2 ambapo kasoro na mambo yaliyobainishwa wakati wa mchakato wa makabidhiano yanashughulikiwa. Nyongeza mpya kwenye jalada la mali ya Umoja wa Afrika ni Makao mapya ya Makamu Mwenyekiti, ambayo yalikamilishwa mnamo Desemba 2023.

Mradi wa ufungaji wa GPS, ambao ulizinduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2022, umeruhusu matumizi bora ya magari rasmi. Hutengeneza historia za safari kwa ajili ya utumiaji mzuri na bora wa rasilimali, hubainisha matumizi yoyote yasiyoidhinishwa ya magari, na hufanya ufuatiliaji wa wakati halisi kwenye njia.

Neno kuhusu New York, Brussels na Lagos?

### 4.3.5. ULINZI NA USALAMA

Madhumuni ya Kitengo cha Ulinzi na Usalama ni uundaji wa mfumo wa ulinzi na usalama unaozingatia hatari, unaolenga ulinzi wa mahali pa kazi na ukuzaji wa mifumo na zana za mawasiliano ya dharura. Katika kipindi cha kuripoti, Ukaguzi wa

miundombinu ya jumla ya ulinzi na usalama ya AUC ulibainisha hitaji la dharura la kuboresha miundombinu ya usalama ya taasisi kama vile lango la kuingilia, Kamera za Ufuatiliaji, mfumo wa kudhibiti Hatari za Moto. Hivyo, uboreshaji wa mifumo hii ya usalama katika AUC ulianza na utakamilika katika robo ya kwanza ya 2024. Miradi kama hiyo ilisaidiwa kwa Afrika CDC na PANVAC.

### 4.3.6. AFYA NA USTAWI WA WAFANYAKAZI

Katika kuunga mkono utendaji wa taasisi, tija na ufanisi wa kiutendaji, Umoja wa Afrika hutoa huduma bora za afya kwa wafanyakazi, wafanyakazi wa Balozi za Nchi Wanachama, wategemezi wao, Operesheni za Msaada wa Amani na huduma za Kibinadamu, pamoja na wajumbe wa mikutano na mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa UA. Mwaka 2023, utaratibu mpya wa kufufua miradi iliyopewa jina la "Kuimarisha Mfumo wa Utoaji wa Huduma za Matibabu" ambayo ilizinduliwa mwaka 2015. Katika suala hili, uhamasishaji wa afya na uzuiaji wa magonjwa uliongezwa kupitia elimu ya afya na mawasiliano, na kuongeza ufahamu kuhusu magonjwa sugu kama vile shinikizo la damu, kisukari, na unene uliopitiliza. Aidha, MHSD ilianza kutoa chanjo kwa watoto na watu wazima, huduma za uzazi kwa wanawake wajawazito, dawa kwa wasafiri na ushauri, ufahamu kuhusu magonjwa ya maeneo ya mwinuko, kuzuia na kudhibiti matatizo yanayohusiana na kazi, magonjwa ya akili, na kadhalika. Africa CDC ya na Taasisi nyingine mshirika pia ziliombwa kusaidia kutambua maeneo mahususi ili kuimarisha utoaji wa huduma za matibabu.
Juhudi pia zilifanywa kutambua hospitali bora na huduma za ndege za kubeba wagonjwa katika miji tofauti barani kote - Addis Ababa, Nairobi, Accra, Banjul, Dakar, Casablanca/Rabat, Abidjan na Abuja. Hii itahakikisha uhamishaji wa haraka wa wagonjwa wakati wa dharura, kutoa huduma za afya kwa wafanyikazi na wategemezi wao na pia kuzuia matumizi ya fedha binafsi.

### 4.3.7. ITIFAKI

Kurugenzi ya Huduma za Itifaki huhudumia mahitaji ya itifaki ya AUC, ikijumuisha yale ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Viongozi Waliochaguliwa, na wafanyakazi wote wa AUC. Pia inashirikiana na Balozi za Kudumu wa Nchi Wanachama na Ofisi za Waangalizi kwa Umoja wa Afrika (UA) pamoja na ofisi za uhusiano za Vyombo vya UA, Taasisi Maalumu, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs), na mashirika yanayohusiana nayo yaliyoko Addis Ababa. AUC hutumia kanuni za kawaida katika mikutano na sherehe za kidiplomasia zinazohusisha Balozi/Waangalizi wa Kudumu na wawakilishi wao.




## 4.3.8. VYOMBO VYA HABARI NA KUJENGA CHAPA

**KUTANGAZA MIAKA 60 YA OAU/AU**
AUC ilianzisha kampeni ya kina ya mawasiliano iliyoundwa kuwakumbuka baba na mama waanzilishi wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU)/Umoja wa Afrika (AU). Mpango huu ulilenga kupitia michango yao ya kimaono na kuonyesha jinsi maono haya yametafsiriwa kuwa vitendo vyenye matokeo na Umoja wa Afrika katika kutimiza wajibu wake na kuendeleza Ajenda ya Afrika 2063. Chini ya mwavuli wa maadhimisho ya miaka 60, kampeni ina kaulimbiu isemayo « Afrika Yetu, Mustakabali Wetu" na inatangazwa kupitia mitandao ya kijamii ikiwa na hashtag #OurAfricaOurFuture. Kampeni hiyo ilijumuisha shughuli mbalimbali, zikijumuisha shughuli za vyombo vya habari vya utangazaji. Hii ilijumuisha mahojiano ya televisheni ya viongozi wakuu wa UA na vyombo vya habari vya kanda na kimataifa wakati wa Maadhimisho ya Miaka 60.

**UZINDUZI WA AWAMU YA 2 YA MPANGO WA AU MEDIA FELLOWSHIP (AUMF)**
Umoja wa Vyombo vya Habari wa Umoja wa Afrika (AUMF) ulishuhudia ongezeko kubwa la shauku, huku zaidi ya maombi 6000 yalipokewa kwa awamu ya mwaka 2023, ikilinganishwa na maombi 800 kwa mwaka 2022. Ongezeko hili kubwa linaonyesha kuongezeka kwa shauku katika mpango wa AUMF. Awamu ya Pili, ilijumuisha watu 20 waliochaguliwa, kutoka nchi mbalimbali, zikiwemo Malawi, Msumbiji, Guinea ya Ikweta, Somalia, Algeria, Afrika Kusini, Botswana, Tunisia, Namibia, Togo, Kenya, Benin, Morocco, Burundi, Nigeria. , Uganda, Sudan Kusini, Gambia, Mauritius, na Misri.

**KUJENGA CHAPA YA UA NA KUTANGAZA MAMLAKA NA AJENDA ZA UA 2063**
Katika kutangaza kaulimbiu ya Mwaka 2023, AUC ilianza utayarishaji wa filamu 2: filamu ya kwanza inayoelezea Hati za Uendeshaji za AfCFTA na nyingine inahusu

utendaji kazi wa AfCFTA na kazi ya Sekretarieti ya AFCFTA pamoja na idara muhimu za utekelezaji na taasisi na kampeni ya mitandao ya kijami kuhusu AfCFTA; ilichapisha toleo la AU Echo 2023 kuendana na kaulimbiu na kutengeneza ukurasa wa tovuti kwenye https://au.int/en/theme/2023/acceleration-of-afcfta-implementation.

Aidha, AUC ilikamilisha utengenezaji wa filamu kuhusu AUC ya Afrika kuhusiana na Haki za Binadamu (ACHPR) na Mkakati wa UA wa Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake (GEWE). AUC ilianza utayarishaji wa filamu kuhusu kazi ya Africa CDC, inayotarajiwa kukamilika mwishoni mwa 2023. AUC ilianza kutengeneza kipindi cha TV, ambacho kinafanywa kwa ushirikiano na AUDA-NEPAD na kinalenga kuitangaza UA kwa kuonyesha miradi halisi ya Ajenda 2063 inayotekelezwa katika ngazi ya Nchi Wanachama na matokeo yake kwa wananchi.

#### 4.3.9. MAHAKAMA YA UTAWALA YA IES

Katika kipindi cha kuripoti, AUAT ilishughulikia malalamiko kumi na moja (11) za wafanyakazi kwa maandishi baada ya vikao kadhaa kwa njia ya video kati ya Mei na Agosti 2023. Kundi la ziada la malalamiko tisa (9) ya wafanyakazi linatarajiwa kushughulikiwa mwishoni mwa mwaka. Jumla ya malalamikos ya wafanyakazi yaliyowasilishwa kwa mwaka 2023 (mwaka hadi sasa) ni ishirini (20), ikilinganishwa na kumi na tano (15) kwa mwaka 2022, kumi na moja (11) katika mwaka 2021, na hamsini na tisa (59) mwaka wa 2020. Malalamiko ya wafanyikazi yanatarajiwa kuongezeka kutokana na mabadiliko ya muundo mpya wa wafanyikazi wa AUC kupitia Ujuzi. Hivyo AUAT imepanga kikao maalumu mwezi Novemba-Desemba 2023 ili kujiandaa kwa ongezeko la mzigo wa kuliko kawaida katika 2024.

Muda wa kuhudumu wa Wajumbe wa sasa uliisha Julai 2023. Wajumbe watatu wapya kutoka Jamhuri za Niger, Nigeria, na Rwanda waliteuliwa na Baraza Kuu mnamo Februari 2023.

### 4.4. USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

Mipango ya Usimamizi wa Rasilimali Watu katika kipindi cha kuripoti iliendelea kulenga kusaidia mageuzi ya kitaasisi. Upeo wao unahusisha; upatikanaji na usimamizi wa vipaji, kurahisisha michakato ya Utumishi katika Umoja wa Afrika, kuboresha usimamizi wa utendaji na kujenga uwezo, kutekeleza mpango wa mpito wa Kamisheni kupitia uajiri na SACA, na kutekeleza miundo mipya na/au iliyoratibiwa upya ya taasisi muhimu ikijumuisha Sekretarieti ya AfCFTA, Africa CDC, AUDA- NEPAD, Chuo Kikuu cha Afrika, Tume ya Umoja wa Afrika ya Sheria za Kimataifa (AUCIL), na Idara ya Ujenzi Mpya na Maendeleo ya Baada ya Migogoro (PCRD).

#### 4.4.1. MAENDELEO KATIKA UTEKELEZAJI WA MUUNDO WA IDARA YA AUC – MWONGOZO WA AJIRA

Kama ilivyobainishwa katika Kanuni na Sheria za Wafanyakazi, mchakato wa kuajiri wa AUC unaongozwa na kanuni za sifa, mgawo wa nchi wanachama, usawa wa kijinsia na uwakilishi wa vijana. Maadili ya UA ya uwazi, utofauti na ushirikishwaji, n.k. pia yanazingatiwa kwenye mchakato wa kuajiri.

Mfumo wa Ajira unaotegemea sifa- MBRS, chimbuko la R10 (timu ya Wataalamu 10 wa Kuajiri, wawili kwa kila eneo) iliendelea kuwa chombo muhimu cha kuimarisha ufanisi, usawa (kiasi) na uwazi wa michakato ya kuajiri katika kipindi chote cha kuripoti. .

Kujaza nafasi kwenye Muundo mpya wa Idara ya AUC uliopitishwa mwaka wa 2020 kama mojawapo ya matokeo ya mageuzi ya kitaasisi, hususani timu yake ya wasimamizi wakuu, imekuwa kipaumbele kwetu. Muundo huo unajumuisha nafasi 28 za ngazi ya Wakurugenzi na Wakuu wa Idara 60, ambapo nafasi za Wakurugenzi 25 tu na Wakuu wa Idara 40 ndio zilizotangazwa kuwa wazi kwa ajili ya ajira mpya.

Katika mwaka wa 2023, tuliimarisha timu ya usimamizi ya Kamisheni ya UA kupitia kuajiri Wakurugenzi wapya 10, na kufanya jumla ya wakurugenzi walioajiriwa na Mkurugenzi Mkuu kufikia 21 (wanne (4) waliosalia ni miongoni mwa waliotangazwa tena na kuratibiwa na mchakato kukamilika katika Robo 1, 2024). 14 [thibitisha idadi] Wakuu wa Idara, pamoja na nyadhifa nyingine muhimu, pia waliajiriwa katika kipindi cha kuripoti.

AUC ina dhamira sio tu kuvutia vipaji bora kutoka katika bara zima na Diaspora lakini pia mazingira mazuri ya kazi ambayo yanakuza ukuaji, ubunifu, na uongozi wa mabadiliko. Juhudi zetu katika kurahisisha mchakato wa ajira ni mwanzo tu. Mwaka 2023, tuliongeza mwonekano wa UA kupitia maonyesho matatu ya kitaaluma ili kuvutia vipaji mbalimbali kutoka katika bara zima na ughaibuni. Pia tulishiriki kikamilifu katika programu za uhamasishaji ili kuungana na watarajiwa wanaoshiriki maono yetu ya umoja, ustawi na amani barani Afrika. Kwa ndani, takribani wafanyakazi 174 walihudhuria kozi za ana kwa ana, huku wafanyakazi 534 walijiandikisha kwenye kozi mbalimbali za kujisimamia wenyewe kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Mafunzo wa Taasisi (LMS).

Mwako 2024, tunalenga kuboresha Mfumo wetu wa Kuajiri Kulingana na sifa zaidi, kuhakikisha kuwa unabadilika kulingana na mahitaji yanayobadilika ya kazi yetu na soko linalobadilika la vipaji. Hii itaendana na uamuzi wa Baraza Kuu EX.CL/Dec.1126(XXXIX) ambao *"uliomba Kamisheni kuendelea kutekeleza mfumo wa MBRS na Mgawo unaozingatia uwiano kwa urahisi na kuboresha mifumo hii, kupitia sera husika na kuzingatia mafunzo tuliyojifunza pia na mapendekezo yaliyotolewa na Nchi Wanachama".*

Sehemu hii inapaswa kuangaliwa

### 4.4.2. MAENDELEO YA UTEKELEZAJI WA MUUNDO WA IDARA YA AUC KUPITIA SACA

Sehemu ya kukamilishwa

# 5. NAFASI YA AFRIKA KATIKA JUMUIYA YA KIMATAIFA

## 5.1 MWELEKEO MPYA: KUJENGA MUSTAKABALI WA USHIRIKIANO WA UMOJA WA AFRIKA

Kuna juhudi zinaendelea kufanywa ili kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za kikanda za Afrika na Umoja wa Afrika ili kuongeza ufanisi wao katika kupaza sauti moja ya Kiafrika katika ngazi ya kimataifa. Mafanikio ya mipango hii yanategemea azma ya nchi za Afrika kushirikiana na kushughulikia changamoto zao kwa pamoja.

Kimataifa, miongoni mwa washirika muhimu ni Umoja wa Ulaya (EU) na nchi wanachama wake binafsi, Umoja wa Mataifa (UN), China, Marekani (USA), Jumuiya ya Nchi za Kiarabu, India, Korea, na Uturuki. Mwaka 2023, Mwenyekiti wa Kamisheni alipokea maafisa wakuu kutoka nchi washirika mjini Addis Ababa. Waziri wa Mambo ya Nje wa China aliteua AU kama ziara yake ya kwanza nje ya China. Mazungumzo kati ya viongozi yalilenga mapitio ya ushirikiano wao wenye mafanikio, kuthibitisha ahadi za kuimarisha ushirikiano wao imara ndani ya mchakato wa FOCAC, na uzinduzi rasmi wa Ofisi za Africa CDC.

Kwa kuongezea, Mwenyekiti alifanya mikutano na Waziri Mkuu wa Italia na Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa na Ujerumani kujadili mambo yanayohusiana na kufuatilia ahadi zilizotolewa wakati wa Mkutano wa 6 wa AU-EU na kuboresha mazungumzo ya mara kwa mara kuhusu maslahi ya pamoja. Ziara ya NaibuWaziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki ilitoa fursa ya kuthibitisha jukumu muhimu la upatanishi la AU katika mgogoro wa Sudan na kutathmini msaada unaoweza kutolewa na Uturuki. Mbali na Mkutano wa AU wa Februari, Mwenyekiti alifanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ili kusisitiza azma yao ya kushughulikia changamoto muhimu za amani na usalama. Zaidi ya hayo, Mkutano wa kikazi na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani kwenye Makao Makuu ya AU uliwezesha mazungumzo na kubadilishana maoni kuhusu masuala ya kikanda na kimataifa.

Mwenyekiti wa Kamisheni alishiriki kikamilifu Mkutano wa 9 wa Mawaziri wa Kamati ya Ushirikiano wa Afrika- na Jumuiya ya Nchi za Kiarabu uliofanyika Septemba 22, 2023, pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UNGA). Mkutano huo

ulipitia utekelezaji wa maazimio kutoka Mkutano wa Nne wa AU-LAS mnamo Novemba 2016, ikiwa ni pamoja na Rasimu ya Mpango Kazi, Misingi, na Vigezo vya Kushiriki. Aidha, maandalizi ya Mkutano wa 5 wa Ushirikiano wa Afrika na Jumuiya yan chi za Kiarabu yalijadiliwa, na Mwenyekiti akiongoza Sekretarieti mbili kutatua kwa makini masuala yaliyosalia, ikiwa ni pamoja na mambo yanayohusiana na tarehe za mikutano ya maandalizi kwa ajili ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

Kuhusu kukamilisha Rasimu ya Sera na Mfumo wa Mkakati wa Ushirikiano wa AU, kama ilivyoamriwa na Uamuzi wa Baraza kuu  EX.CL/Dec.1189 (XLII) mnamo Februari 2023, Kamisheni  iliwasilisha toleo lililorekebishwa ili kujadiliwa na Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu(PRC) . Toleo hili lililorekebishwa linategemea misingi ifuatayo:

- Kuheshimu na kutekeleza kikamilifu vipengele vya sheria, hasa jukumu na mamlaka ya Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika.
- Kutekeleza kikamilifu maamuzi ya Baraza kuu namba 635 na 762
- Wito uliotolewa na wengi wa Marais na serikali za AU kutekeleza kikamilifu mbinu za uwakilishi kwenye matukio ya kimataifa
- Mapendekezo ya kutofautisha kwa njia ya ubunifu kati ya Ushirikiano wa Kitaasisi unaoendeshwa na Mwenyekiti wa Kamisheni na ushirikiano wa serikali kwa serikali unaoendeshwa na Nchi Wanachama wa UA.

Umoja wa Afrika sasa uko katika wakati muhimu, unaoonyesha haja ya kufanya tathmini ya kina ya mkakati wake wa ushirikiano. Kuna haja ya kujitathmini upya sio tu njia lakini pia misingi inayousaidia Umoja huu wa Afrika. Wakati jukumu la Afrika kwenye jukwaa la kimataifa linavyoendelea kubadilika katika mandhari ya kijiopolitiki inayobadilika, AU lazima ijiwekeze kimkakati ili kujenga ushirikiano zaidi ya maoni ya utaratibu tu, ukiendana na matarajio makubwa ya bara hilo la Afrika. Mageuzi haya ya kifikra ni muhimu ili kuhakikisha kwamba ushirikiano wa AU unaleta mchango wa kweli katika kufikia malengo makuu ya maendeleo, amani, na utulivu kote barani Afrika.

## 5.2 KUTOKA KUTAMBULIWA MPAKA KUWA NA USHAWISHI: UANACHAMA WA UMOJA WA AFRIKA KWENYE JUMUIYA YA NCHI ISHIRINI TAJIRI DUNIANI YAANI G20

Ikikabiliwa na changamoto lukuki, Afrika imefikia mafanikio ya kipekee ambayo yameimarisha hadhi yake kimataifa. Maendeleo muhimu sana yalifikiwa Septemba 9, 2023, wakati wa Siku ya Umoja wa Afrika, wakati wa mkutano wa G20 huko New Delhi,India,  ilipitisha rasmi uamuzi wa kukubalia AU kama mwanachama wake mpya, ikilinganisha na Uamuzi wa Mkutano Mkuu wa /AU/Dec.845(XXXVI). Kupata kiti ndani ya G20 kulikuwa ishara muhimu sana, ikithibitisha Afrika kuwa na ushawishi mkubwa  kimataifa wenye uwezo wa kuleta mageuzi.

Mchakato wa kufikia uanachama wa G20 ulichukua juhudi kubwa za miaka saba za kudai kutambulika Kati ya mambo muhimu katika safari hii ilikuwa ni utulivu wa kidiplomasia wa AU kwa maandamano ya umoja na mshikamano wakati mgumu  wa

janga la UVIKO-19 na uanzishwaji wa Eneo la Biashara Huria la Afrika (AfCFTA), ukichangia sana kuingizwa kwa AU kwa njia inayostahili kwenye G20. Kabla ya AU kujiunga, G20 iliwakilisha karibu 85% ya Pato Ghafi la dunia na 75% ya biashara ya kimataifa, pamoja na theluthi mbili ya idadi ya watu duniani. Awali, ilifikiriwa kama jukwaa lisilo rasmi la ushirikiano wa kiuchumi kimataifa, G20 imekuwa mhimili mkubwa wa utawala wa kimataifa unaopanga majibu ya sera kwaajili ya utulivu wa kiuchumi na changamoto za ulimwengu. Bila kuwa na ushawishi, Afrika hadi sasa imebaki kuwa mpokeaji pasipo kushiriki badala ya kuwa msaidizi katika mazungumzo yanayounda hatima yake ya kiuchumi, ikisababisha maamuzi yasiyokidhi mahitaji ya kikanda kwa ufanisi. Miradi muhimu, kama Mfumo wa Kawaida wa G20 wa kurekebisha Deni, imekwama kwa sehemu kutokana na kukosekana kwa uwakilishi wa Afrika, ikifanya maamuzi haya kuwa dhaifu, ya polepole, na yenye utata. Kwa kuzingatia changamoto za madeni na fedha za Afrika, uanachama wa AU kwenye G20 unatoa motisha na mwongozo kwa nchi za Afrika kushirikiana katika sera za nje za kiuchumi na kifedha.

Uanachama wa G20 unatoa fursa kwa AU kusimamia maslahi ya nchi wanachama wake katika utawala wa kimataifa, ikiruhusu bara hilo kusonga mbele katika ajenda za masuala ya kimataifa, kuhakikisha maamuzi ya sera yanayofaa kwa uchumi wa dunia na kurahisisha ushirikiano wa kimataifa juu ya masuala muhimu. Uanachama wa AU unaweza kurahisisha kufanikisha uelewa na kutambuliwa kwa dhahiri uwezo mkubwa wa Afrika wa kubeba jukumu kuu la kusukuma mageuzi ya kijani duniani na kwa kukuza mfumo wa ushirikiano wa kufanikisha hili kwa manufaa ya pande zote.

Mifumo madhubuti, michakato ya umoja, na kuweka mikakati kwa haraka, pamoja na tathmini kamili ya fursa, ni muhimu katika kufanikisha faida zinazotarajiwa za uanachama wa AU kwenye G20. Kwa hivyo, mahitaji ya uwezo wa Kamisheni ya AU, nchi wanachama, na vigezo vya uwakilishi wa G20 lazima vionekane wazi ili AU iweze kukutekeleza kikamilifu majukumu yake mapya ya utawala wa kimataifa. Mchakato huu ulianza kwenye Mkutano wa G20 Compact with Africa huko Berlin, Ujerumani, ambapo Mhe. Mwenyekiti wa Kamisheni Moussa Faki Mahamat alishiriki pamoja na Marais 18 wa Kiafrika. Kwa wakati huohuo, ujumbe ulioongozwa na Mhe. Albert M. Muchanga, Kamishna wa AU kwenye ETTIM, ulishiriki mikutano ya awali ya Sherpa Track ya Urais wa G20 wa Brazil mnamo Desemba 2023. Zaidi ya hayo, majadiliano rasmi yameanzishwa katika ngazi ya PRC ili kupanga mikakati ya AU kushiriki mikutano ya G20, kwa kuanzisha Kikundi Kazi cha PRC kitakachoshughulikia Mbinu na Vipaumbele vya Uanachama wa AU kwenye G20. Katika ngazi ya Kamisheni ya AU, Kikundi Kazi Ndani ya AU kuhusu G20, kinachoongozwa na Kamishna wa ETTIM na kusaidiwa na Mkurugenzi Mkuu wa AU,kilichoshirikisha Wadhibiti wote muhimu wa AU, kilianzishwa ili kuwezesha ushiriki bora na wa maana wa AU kwenye mikutano ijayo ya G20, ikijumuisha Mkutano wa Viongozi wa G20 na kuandaa mapendekezo ya mfumo kamili wa sera, bajeti, na taasisi.

## 5.3 KUJENGA MAELEWANO: MFUMO WA URATIBU WA NGAZI TATU KATIKA UHUSIANO WA AU-UN

Uhusiano wa mashirikiano unaokua kati ya Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Mataifa (UN) umekomaa kwa kuwa ushirikiano wa kina, haswa chini ya uongozi wa Mhe. Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU (AUC) na Mhe. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UNSG) mwaka 2023, kufuatia mkutano wa kila mwaka uliofanyika Novemba 2023. Mikutano na mashauriano imetoa mchango muhimu katika kusimamia mahusiano kati ya taasisi hizo mbili. Ushirikiano wa AU-UN umefikia hatua muhimu, ikionekana kuwa mfumo bora wa utawala na usanifu ulioundwa kwa kuboresha uratibu. Usanifu huu wa ubunifu, unaotambulika kama mfumo wa "tabaka tatu" wa uratibu, unajumuisha Mkutano wa Kila Mwaka wa AU na UN, mazungumzo ya kimkakati ya ngazi ya juu ikiwa ni pamoja na ana kwa ana, pamoja na kigezo cha kitaalamu na kazi; kila kimoja kikitumikia kazi tofauti. Mbinu iliyopangiliwa hivi imejiweka vizuri kujenga uwezo mkubwa, ikisisitiza umuhimu wa kuimarisha uratibu kati ya mashirika ya AU na UN, muhimu kwa kuingiza kikamilifu Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya 2030 na Ajenda 2063.

Mbinu iliyopangiliwa na iliyoundwa kwa umoja sio tu inapunguza upungufu bali pia inaongeza matumizi ya rasilimali kwa ufanisi, ikisaidiwa na wadau wa ndani na nje pamoja na washirika wa maendeleo. Ushirikiano wa kipekee kati ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa unatoa mapenzi muhimu kwa ushirikiano wenye mafanikio katika kushughulikia vipaumbele na mahitaji ya dharura ya bara la Afrika. Mfumo wa Maendeleo unategemea kanuni zilizowekwa katika mfumo wa mkakati wa ushirikiano wa AU na UN kwa ajenda ya 2017–2027 ya ujumuishaji na maendeleo ya Afrika. Ushirikiano huu unafanana na utekelezaji wa Ajenda 2030 na Mpango wa Pili wa Miaka Kumi ya Utekelezaji, pamoja na baadaye, Ajenda 2063, ukiwa kama mfumo mkuu wa ujumuishaji na maendeleo ya Afrika. Vigezo ndani ya ushirikiano huu hufanya tathmini ya utendaji wa Afrika katika uga wa kisiasa, kiuchumi, na kijamii.

Kwa kuzingatia maeneo ya kimaudhui yaliyoanzishwa mwaka 2018 chini ya "Mfumo wa AU na UN wa Kutekeleza Ajenda 2063 na Ajenda 2030" na "Mfumo wa Pamoja wa UN na AU kwa Ushirikiano Ulioboreshwa katika Amani na Usalama," mashauriano yanayoendelea kati ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa yamekuwa fursa ya ushirikiano. Mazungumzo ya Kimkakati ya Ngazi ya Juu kuhusu Maendeleo Endelevu yalianzishwa ili kushughulikia vipaumbele vikubwa ndani ya ushirikiano huu wa pamoja, ikitoa mapendekezo ya kujadiliwa kwenye Mkutano wa Kila Mwaka wa AU na UN. Mikutano miwili ya Mazungumzo ya Kimkakati ya Ngazi ya Juu ilifanyika mwezi Mei na Novemba 2023.

Mkutano wa Saba wa Kila Mwaka wa AU na UN, ulioitishwa na Katibu Mkuu wa UN António Guterres na Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU, ulihakiki maendeleo katika kutekeleza "Mfumo wa Pamoja wa UN na AU kwa Ushirikiano Ulioboreshwa katika Amani na Usalama" na "Mfumo wa AU na UN kwaajili ya Ajenda Mbili Zilizopangwa." Kukubali na kuidhinisha pendekezo la kipaumbele cha ushirikiano katika ufadhili wa

maendeleo endelevu mwaka 2024, Mwenyekiti na Katibu Mkuu walitoa wito wa mageuzi katika mfumo wa kifedha wa kimataifa ili kuimarisha uwezo wa Afrika kukabiliana na changamoto za karne ya 21. Kusisitiza uhusiano kati ya kuimarisha ushawishi wa kimataifa na uwezo wa Afrika na nchi zaidi kumiliki, nafasi ya sera, na udhibiti wa miamala ya kiuchumi na kifedha, Mwenyekiti na Katibu Mkuu walisisitiza jukumu la taasisi zenye ufanisi, haswa mifumo ya kutafuta rasilimali za ndani. Walionyesha uwezo wa ushirikiano kati ya AU na UN katika kufikia malengo haya. Walihimiza Mazungumzo ya Kimkakati ya Ngazi ya Juu ili kutafuta njia bora zaidi ya kunufaika na uwepo wa Umoja wa Mataifa barani Afrika. Mkutano wa Nane wa Kila Mwaka wa AU na UN umepangwa kufanyika jijini Addis Ababa mwaka 2024.

Kuufikisha ushirikiano wa AU na UN katika ngazi ya juu kabisa ambayo ni wa kitaalamu na kiutendaji kazi, taasisi hizo mbili zilikutana Dar-es-Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 4 hadi 6 Desemba 2023 katika Semina yao ya Kwanza ya Sera ya Ngazi ya Juu iliyopewa jina "Kuelekea 'Afrika Iliyotangamanishwa': Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Ajenda 2063 ya Afrika Tuitakayo" katika Ngazi ya Wakurugenzi.

## 6.4 KUBUNI NJIA MPYA YA UBUNIFU KWA AJILI YA UTAFUTAJI WA RASILIMALI

Kwa kuzingatia azma yake ya kushughulikia changamoto za bara, AUC inashirikiana kwa kiasi kikubwa na taasisi za Kiafrika, ikihakikisha kupitishwa kwa misimamo ya pamoja inayounganisha sauti mbalimbali katika bara hili. Juhuhudi hizi zinazolenga kitu kimoja zinasukumwa na ulazima wa Afrika kuzungumza kwa sauti moja, kuzidisha ushawishi wake katika kushughulikia masuala ya kimataifa. Kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha misimamo hii ya pamoja, AU inafanya bidii kutumia sauti hii iliyoshikamana kimataifa wakati inaposhirikiana na washirika mbalimbali. Kupitia ushirikiano huu wa kimkakati, AU inajitahidi kujenga ushawishi wake wa pamoja, ili kukuza maslahi na vipaumbele vya bara la Afrika katika mazungumzo na majadiliano ya kimataifa.

Ushirikiano na taasisi za kifedha za Kiafrika ni muhimu kwa malengo na utekelezaji wa mipango ya Umoja wa Afrika. Taasisi hizi, ikiwa ni pamoja na benki za maendeleo za kikanda na taasisi za kifedha za kitaifa, zinapaswa kushiriki kikamilifu kwa kutoa ufadhili, ujuzi wa kitaalamu, na mwongozo wa kimkakati. Kulinganisha malengo yao na vipaumbele vya AU kunahakikisha mkakati mahsusi, ukiwezesha rasilimali na kupunguza urudubishwaji wa kazi. Kuweka mifumo madhubuti ya ushirikiano, kama vile kamati za pamoja na mashauriano ya mara kwa mara, ni muhimu. Ushirikiano wenye tija unachagiza utulivu wa kiuchumi na maendeleo endelevu na kufungua fursa za Afrika. Taasisi hizi kwa pamoja zinashinda vikwazo vya kifedha kupitia ushirikiano wenye ufanisi, na kuifanya Afrika kuwa na ustawi.

## 6. HITIMISHO: TUNATAKA UMOJA WA AFRIKA WA NAMNA GANI?

Umuhimu wa ripoti ya mwaka ya 2023 ni kwamba ina tathmini mbili. Ile ya shughuli zilizofanywa katika mwaka huo lakini pia ile ya muongo wa kwanza wa utekelezaji wa Ajenda 2063. Kutokana na mchanganyiko wa tathmini hizi mbili, bila shaka, ni utambuzi wa maendeleo makubwa katika maeneo mbalimbali ya shughuli za Umoja wetu, lakini pia. upungufu mwingi unaohusiana na sababu mbalimbali:

- Kuhusiana na masuala ya ndani, kuna utegemezi mkubwa wa wabia katika suala la kufadhili programu zetu, uwiano kati ya matarajio yaliyotangazwa ya Nchi Wanachama na utekelezaji wa maamuzi, changamoto ya mchakato wa ujumuishaji inayotokana na vikwazo vingi vya kimuundo, usimamizi na matokeo ambayo msingii wake umewekwa kwenye bidii, mtazamo, vitendo nk.

- Kuhusiana na muktadha wa kimataifa, unaokabiliwa na misukosuko ya kijiografia, kiuchumi, kiteknolojia na kuitamaduni, na kusababisha athari mbaya kwa uchumi wa Afrika na athari ya kudorora, na kuzuia ukuaji wao, na hivyo kuziweka nchi zetu katika hali ngumu ya kijamii na kiuchumi inayochochewa na mzigo mzito wa madeni. Ripoti ilijikita kwenye masuala haya tofauti na hitimisho hili lingependa kuelezea baadhi ya njia za kuyashughulikia kwa ufanisi zaidi.

Kwa kuzingatia kwamba matatizo na upungufu unaoonekana hauwezi kuepukika, huenda ukakwamisha utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo.

**Amani na Usalama**

Katika eneo la amani na usalama, Umoja wa Afrika umepata uzoefu mkubwa katika kuzuia migogoro, usimamizi, utatuzi na ujenzi upya baada ya migogoro. Ni mchakato wa kujifunza na maboresho endelevu mara nyingi huathiriwa na sababu za ndani na nje, ambazo si rahisi kuzidhibiti kila wakati. Wakati tukijadili mafanikio ya PRC na utekelezaji wa Mpango wa Amani na Usalama wa Afrika (APSA), ni muhimu kuchukua hatua kwa maeneo yaliyotambuliwa kama vile uratibu bora kati ya UA na RECs kwa upande mmoja na Umoja wa Mataifa kwa upande mwingine, uhamasishaji wa ufadhili ili kuwezesha shughuli za PRC, pamoja na uimarishaji wa uwezo wa kukadiria na kufuatilia. Kwa hiyo wakati umefika wa kutafakari kwa kina nyenzo za Umoja wa Afrika kwa ajili ya amani na usalama kuhusiana na masuala muhimu yafuatayo:

- Uharaka wa mageuzi ya PRC;
- Ufanisi wa vikwazo kwa mabadiliko yasiyo ya kikatiba lazima utathminiwe ili kuoanisha vitendo vyetu na malengo;
- Ufadhili wa shughuli za amani na usalama lazima uendane na changamoto na matarajio ya Bara letu.

Mbali ya vikwazo hivi vilivyobainishwa kama sababu za amani na usalama katika Bara, Umoja wa Afrika umejaribu kufikiria kuhusu amani katika uhusiano wake wa kiutendaji na maendeleo, katika maono yaliyoimarishwa ya uhusiano wa "amani, usalama" na maendeleo".

Inawezekana kuwa ukosefu wa usalama unaozikumba nchi zetu kadhaa ni matokeo ya ucheleweshaji wa maendeleo. Hivyo, Umoja wa Afrika umefanya kazi ya kuimarisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii ya Nchi Wanachama, ambayo yangeboresha uhimilivu wao kwa sababu za kukosekana kwa utulivu zilizobainika katika miaka ya hivi karibuni, hususani matatizo ya nje yanayotokana na migogoro ya kifedha na migogoro mingine ya kijiografia kwa upande mmoja, na majanga ya asili yanayotokana na upungufu kwenye usimamizi na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa upande mwingine.

**Ajenda ya Maendeleo na Utangamano wa Kanda**

Inaonekana kwenye ripoti hiyo kwamba afua za Umoja wa Afrika zimejikita katika Ajenda 2063, mikakati na programu za kisekta kwa ujumla zikisaidiwa kifedha na wabia. Ili kuboresha ufanisi wa utekelezaji wake, mikakati na programu zinahitaji umiliki mkubwa zaidi wa Nchi Wanachama na kuzingatia muktadha unaobadilika kila mara na kuambatana na ufadhili unaotabirika na endelevu. Aida, itakuwa vizuri kuhakikisha uthabiti kati ya malengo na mwelekeo wa mikakati mbalimbali ili kuhakikisha uwiano wao na Ajenda 2063. Hivyo, juhudi za mashauriano na uratibu kati ya idara mbalimbali zitalazimika kuongezwa. Shughuli za idara mbalimbali katika mwaka unaojadiliwa zilielekezwa kwenye lengo la jumla la mabadiliko ya kiuchumi ambayo ni msingi wa maendeleo. Hatua iliyofikiwa katika mkabala huu ingeweza kuwa kubwa zaidi ikiwa vikwazo vinavyohusishwa na (i) ufadhili vingeondolewa kupitia utekelezaji wa taasisi za fedha za Afrika (ii) ukosefu wa rasilimali watu unaoonyeshwa na viashirio vya kutisha kuhusu hali ya elimu; (iii) kupunguza gharama za uzalishaji kwa kuboresha miundombinu na kuwekeza katika mabadiliko ya nishati. Kuhusiana na maendeleo jumuishi, janga la Uviko-19 na athari za mgogoro wa Urusi na Ukraine inapaswa kutuhimiza kulenga zaidi watu walio hatarini kupitia utekelezaji wa mitandao ya usalama wa kijamii. Pia, uzoefu uliopatikana kutokana na migogoro hii umebainisha haja ya kuimarisha juhudi zilizowekwa katika maeneo ya usalama wa chakula na usalama wa afya. Makubaliano kuhusu jukumu la ujumuishaji wa kanda kama kichocheo cha mabadiliko ya miundo haipaswi kuficha matatizo yaliyoonekana katika ngazi ya RECs na katika kiwango cha ushirikiano wa bara unaoungwa mkono na AfCFTA. Masuala ambayo yaliongoza ujumuishaji wa bara letu yanapitia mabadiliko makubwa katika muktadha wa sasa. Hali hii inatutaka kuhoji na uwezekano wa kufikiria upya utaratibu wetu wa ujumuishaji kupitia matukio ya hivi majuzi yanayotuzunguka. Uratibu kati ya UA na RECs lazima uendelee unapaswa kujikita kwenye hatua madhubuti zinazoakisi uwiano kati ya RECs, nguzo za kitaasisi za utangamano, na maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika.

**Ushirikiano wa Kimataifa ili Afrika iwe na Sauti yenye nguvu Duniani**

Ushirikiano wa kimataifa hauwezi kuendelea kuonekana tu kupitia msingi wa ufadhili unaotolewa kusaidia programu za UA. Afrika inatoa zaidi kwa wabia wa kimataifa kuliko inavyopokea na Bara letu halina nafasi inayostahili katika jumuiya ya kimataifa. Huu ni wakati wa kupitia kwa kina vigezo vya ushirikiano wetu wa kimataifa kwa manufaa ya uhusiano bora, wa kisasa na unaofaa zaidi kwa wote. Hili ndilo suala halisi la kimkakati kwenye ushirikiano unaojadiliwa hivi sasa katika ngazi

ya Nchi Wanachama na ambao Kamisheni imewasilisha mapendekezo yake kwa usahihi ili kuweka maudhui ya kimkakati katika msingi wa waraka huu. Mapendekezo haya ya ubia wa kimkakati kwa siku zijazo yanatokana na miongozo iliyowekwa, kwa busara zao, na Wakuu wa Nchi na Serikali, hususani katika maamuzi 635 na 762, na kuungwa mkono na mapendekezo ya mchakato wa Mageuzi ya Kitaasisi uliofanywa kwa juhudi za Rais Paul Kagame. Dunia inatarajia mengi kutoka Afrika na Bara letu lazima liwe sehemu ya Historia. Utangamano lazima uzingatiwe ndani ya mfumo wa mahusiano ya ubia na Mataifa, jumuiya za kanda na taasisi za kifedha. Mkakati wa ushirikiano unaokamilishwa sasa unapaswa kuzingatia masuala ya baadaye ya kijiografia na kisiasa na vipaumbele vya bara ili kuongeza faida za kiuchumi, kisiasa na kijamii za ushirikiano huu tofauti. Kuna haja ya haraka ya kufafanua zaidi suala linalohusiana na ushiriki, jukumu la wahusika tofauti, yaani, Nchi Wanachama, UA, RECs, n.k., kuondoa mkanganyiko kati ya viwango vya nchi mbili na kimataifa na muundo wa kuweka utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ambao hutoa ripoti kuhusu kiwango cha umuhimu wa kila moja ya ubia na ukamilishano wao kutokana na mtazamo wa Kiafrika. Ushirikiano unapaswa uimarishe jukumu la Afrika na uwepo wake katika taasisi za utawala za kimataifa, kama vile kukubaliwa kwa UA kama mwanachama wa G20. Suala hili na mengine mengi yanatutaka kutengeneza dira yenye kutoa mchango mkubwa na wenye manufaa kutokana na uwepo wetu katika taasisi hizo.

**Kuimarisha Ufadhili na Ufanisi wa Umoja wa Afrika**

Ripoti ya mwaka huu pia ilionyesha kiwango cha chini sana cha utekelezaji wa maamuzi. Hitimisho la mkutano wa pamoja kati ya Kamisheni-COREP uliofanyika Dakar mnamo Desemba 2022 kuhusiana na suala hili linaonyesha kiwango cha utata wa muundo na utekelezaji wa maamuzi. Kwa hakika, vikwazo vya kitaalamu na kifedha vinazuia uboreshaji wa kiwango cha utekelezaji wa maamuzi, lakini kiini cha tatizo kinatokana na utashi wa kisiasa na kutofautiana kwa maslahi ya Nchi Wanachama. Suala la ufadhili wa UA ni tatizo la mara kwa mara. Mageuzi ya kitaasisi yamewezesha maendeleo ingawa malengo ya awali hayajafikiwa kikamilifu. Kutokana na kushindwa kwa Nchi Wanachama kukusanya rasilimali za ziada, utegemezi kwa wabia unaweza kuendelea, kufuatia mwelekeo ulioonekana katika miaka ya hivi karibuni. Ufumbuzi wa tatizo hili uko katika ngazi mbili. Ngazi ya kwanza ni ya kitaalamu na inahusu uboreshaji endelevu wa usimamizi wa bajeti ambao unaweza kusababisha kuongeza matumizi sahihi ya rasilimali za kifedha.

Mageuzi ya kitaasisi yaliwezesha kuanzishwa kwa kanuni muhimu na uimarishaji wa shughuli za ukaguzi wa ndani na nje, pamoja na usimamizi unaozingatia matokeo. Hatua kwa hatua inabidi zifuatwe, kwa sababu ni mchakato mgumu ambao unahitaji kujenga uwezo wa watendaji wa Umoja wa Afrika na maendeleo ya mfumo wa ripoti. Hivyo mabadiliko itabidi yaendelee kwa kasi. Ngazi ya pili ni ya kisiasa na inawezesha urekebishaji upya wa vipaumbele kuhusiana na uwezo halisi wa kifedha wa Umoja wa Afrika kama ilivyoainishwa na mhimili wa kwanza wa mageuzi ya kitaasisi. Hapa jukumu la Nchi Wanachama ni lile la vyombo vya maamuzi. Hivyo nia ya kuwa na maono ya muda wa kati yenye vipaumbele vilivyoainishwa vyema kwa wakati, ikiambatana na ufadhili mkubwa. Kwa kufahamu jukumu lisiloweza kubadilishwa la rasilimali watu, zoezi linalenga ujuzi wa ukaguzi kwa nia ya kuajiri

waliohitimu zaidi na wenye uwezo mkubwa limeingia katika awamu yake ya mwisho. Mageuzi haya yanatarajiwa kupunguza utegemezi wa utaalamu kutoka nje, kuboresha rasilimali za Umoja wa Afrika na kuboresha ubora wa utaalamu wa uandishi wa ripoti na nyaraka zingine za kazi ambazo hutumika kama msingi wa kufanya maamuzi. Kwa kuzingatia majanga mbalimbali, fedha, mabadiliko ya tabianchi na usalama, maendeleo ya Afrika yanategemea uwepo wa nyenzo za tahadhari na ufuatiliaji ili kuepuka hasara inayoletwa na majanga haya, ambayo gharama zake za kibinadamu na kifedha ni kubwa sana. Inapendekezwa kuweka mifumo ya kuunganisha hatari ili kusaidia Nchi Wanachama. Ambapo maswali ya kimkakati yanaibuka:

- Uamuzi gani umechukuliwa wa kiwango cha juu zaidi, kuhifadhi 0.2% ya mapato ya ushuru wa forodha kwa bajeti ya Umoja wa Afrika? Ni nchi 17 pekee zinazoitekeleza kwa sasa. Hata hivyo, ndio suluhu la suala la kugharamia shughuli za Umoja wetu.

- Kuhusiana na hili, nini kifanyike ili kuhakikisha uzingatiaji wa Kanuni muhimu na malengo ya Johannesburg, ingawa hili inabidi kuamuliwa kwa kauli moja na Nchi Wanachama?

- Njia gani zinaweza kutumika kwa ufadhili wenye ubunifu? Ni muhimu hapa kuoanisha rasilimali na matarajio.

**Kuimarisha jukumu la Kamisheni na kuimarisha Utawala bora**

Ili kuweza kusonga mbele kwa uthabiti na kiutendaji katika miradi muhimu ya Bara letu, wakati umefika wa kutafakari kwa kina mfumo wa utawala wa Umoja wa Afrika na kufafanua majukumu na wajibu wa kila upande. Iwe kuhusu masuala ya Amani na Usalama, ushirikiano wa kimataifa, usimamizi wa fedha na rasilimali watu, Kamisheni na Rais wake wanapaswa waone majukumu na wajibu wao ukifafanuliwa kikamilifu kwa kufuata Sheria Anzilishi, na pia katika kanuni hizo za uwajibikaji kamili. Kwa hakika majibu yanayofaa yangeweza kutolewa hapa. Kadhalika, mgawanyiko wa kazi kati ya Kamisheni na Vyombo, kati ya Kamisheni na RECs, kati ya Kamisheni na vyombo mbalimbali vya Nchi Wanachama lazima uwekwe wazi kwa manufaa ya uoanishaji, uwiano na ufanisi. Tafakari na mapendekezo haya yanatolewa wakati Kamisheni ya sasa inaanza mwaka wake wa mwisho wa mamlaka. Hivyo ni wakati mwafaka wa kuchukua maamuzi ya kijasiri na madhubuti yanayoweza kuiwezesha Kamisheni hii na Vyombo vingine vya Umoja wa Afrika ili kuharakisha utekelezaji wa shughuli zao na hivyo kuandaa mazingira bora zaidi ya kipindi cha mpito kwa timu itakayochukua madaraka baada ya mwaka mmoja. Kwa kufanya hivyo, kamisheni ya sasa haiwezi "kushutumiwa" kutumikia maslahi yake yenyewe. Pia ni fursa ya kuweka utekelezaji wa mpango wa pili wa Ajenda 2063 kwenye mkondo sahihi pamoja na kuuwezesha Umoja wetu kukabiliana kikamilifu na changamoto na matarajio ya sasa. Hivyo, 2024 na zaidi itaonyesha mwanga, wakati mwafaka kwa Afrika.

## 7. RIPOTI YA VINARA (MUHTASARI MKUU)

### 1. MFALME LETSIE WA III WA UFALME WA LESOTHO, KAMA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KATIKA LISHE NA RIPOTI YA MIAKA MIWILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA LISHE WA VIONGOZI WA KIAFRIKA (ALN).

Muhtasari huu wa Utekelezaji unawasilisha kazi ya Kinara wa Lishe kwa kipindi cha 2022/2023. Kinara alitumia muda kushiriki na kushughulikia wadau mbalimbali wa mikakati ya ubunifu inayopendekezwa ili kufanikisha ajenda ya lishe ya bara la Afrika huku pia akihakikisha kwamba Lesotho inatimiza jukumu muhimu la kuendeleza lishe na usalama wa chakula.

Mwezi Mei 2022, tukio muhimu la ngazi ya juu lilifanyika wakati wa Mkutano Maalumu wa Umoja wa Afrika wa Kibinadamu na Mkutano wa Ahadi za michango huko Malabo, Guinea ya Ikweta. Wadau muhimu ikiwa ni pamoja na AUDA-NEPAD, FAO, WFP, Benki ya Maendeleo ya Afrika, na Viongozi wa Lishe wa Afrika (ALN-AfDB), walijadili Hali ya Usalama wa Chakula na Lishe barani Afrika na kupendekeza uwekezaji wa kifedha wa ndani katika usalama wa chakula na lishe, na kipaumbele maalumu kwaajili ya kukuza uhusiano wa muda katika muktadha wa kibinadamu. Pia, ilisisitiza umuhimu mkubwa wa uwekezaji katika data na mifumo ya tahadhari za mapema ili kuimarisha uwajibikaji na maandalizi kwa ajili ya dharura**.**

Mwezi Desemba 2022, Kinara wa Lishe wa Umoja wa Afrika alishiriki Mkutano wa ngazi ya juu ulioandaliwa na Serikali ya Cote d'Ivoire. Mkutano wa ngazi ya juu kuhusu kauli mbiu ya Mwaka wa Lishe wa Umoja wa Afrika ulimalizika kwa kupitishwa kwa Azimio la Abidjan na Mataifa Wanachama wa Umoja wa Afrika.

Mwezi Machi 2023, Mazungumzo ya ngazi ya juu kuhusu Fedha za Lishe yalifanyika Lesotho, ambapo mikakati ya kuimarisha uwekezaji, utekelezaji, na uratibu kwa ajili ya kuongeza lishe na usalama wa chakula barani Afrika ilijadiliwa. Mawaziri wa Afrika, Wabunge, Sekta Binafsi, na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa, walipitisha wito wa hatua uitwao "Kuhamasisha Fedha za Ubunifu kwa Mapambano Dhidi ya Ulegevu/Udumavu wa Lishe" kwa kuzingatia mageuzi ya kiuchumi ya Afrika na malengo na utekelezaji wa Mpango kwa Vitendo wa Azimio la Abidjan.

Ilizinduliwa sambamba na Mkutano wa Vyama vya Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa juu ya Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) mnamo tarehe 9 Desemba 2023, waraka huo unawaomba Viongozi wa Afrika kufanya kampeni kwa kujumuisha lishe kama eneo kuu la uwekezaji kwa kutumia fedha za hali ya hewa kupitia Michango ya Kitaifa Inayoamuliwa (NDCs).

Mwezi Februari 2023, Ufalme wa Lesotho, AUC, AfDB na FAO waliratibu kongamano la chakula cha jioni la ngazi ya juu kikiwa na mada "Maendeleo na Mafanikio katika Kukabiliana na Udumavu wa Lishe barani Afrika." Viongozi wa kisiasa walisisitiza umuhimu wa kufadhili na kuwekeza katika kilimo, lishe, usalama wa chakula na umuhimu wa ushirikiano na ushirikiano wa pande nyingi, ushiriki wa

sekta binafsi na matumizi ya AfCFTA kukuza biashara ya chakula chenye lishe ndani ya bara la Afrika**.**

Katika Ufalme wa Lesotho, Kinara wa Lishe wa Umoja wa Afrika alitembelea miradi ya jamii inayofanya kazi katika ngazi ya msingi, ikiwa ni pamoja na mama wanaonyonyesha, wajawazito, walezi wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, na kuhusisha wanajamii wote, wote wakiwa wamejizatiti katika kuzingatia kanuni bora za lishe kama njia ya kupambana na magonjwa yanayohusiana na lishe. Kinara wa Lishe wa Umoja wa Afrika alishirikiana na Wizara ya Kilimo, Usalama wa Chakula, na Lishe kufanya kampeni ya kukuza vilabu vya lishe sawa nchini kote**.**

## 2. MFALME MOHAMMED WA VI WA UFALME WA MOROKO NA KINARA WA UHAMIAJI KATIKA UMOJA WA AFRIKA.

Mfalme Mohammed wa VI, Mfalme wa Moroko, ameteuliwa kuwa Kiongozi wa Umoja wa Afrika kuhusu Masuala ya Uhamiaji, katika Mkutano wa 28 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU).

Katika suala hili, Mfalme Mohammed wa VI alipendekeza pawepo na maono ya pamoja ya Kiafrika kuhusu uhamiaji katika Ajenda ya Kiafrika ya Uhamiaji. Maono haya yanapata tafsiri kuu katika jarida la l'Observatoire Africain des Migrations (OAM) **-** lililozinduliwa huko Rabat mnamo 2020, na katika Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji Salama, wa Utaratibu na wa Kawaida **-** unaojulikana kama "Mkataba wa Marrakech," ambao ni upanuzi wake kimataifa.

Moroko imeendelea kuhimiza na kupata utambuzi mkubwa wa Ajenda ya Kiafrika ya Uhamiaji katika makongamano yote ambako Moroko inashiriki, ikionyesha umuhimu wa kipekee wa Uchunguzi wa Uhamiaji wa Kiafrika.

### I. KUONGEZEKA KWA SHUGHULI ZA KITUO CHA UTAFITI WA UHAMIAJI CHA AFRIKA.

1. Kwa mujibu wa malengo yake, tangu kuzinduliwa kwake mwaka 2020, Kituo cha Utafiti wa Uhamiaji cha Afrika (OAM) kimejitahidi kuboresha uzalishaji, ukusanyaji, usambazaji, na uchambuzi wa data za uhamiaji zenye uhakika na ubora.
2. Ndani ya mwaka 2023, Kituo hicho kiliongeza shughuli zake katika muktadha wa kufanya kazi kikamilifu. Kwa kweli, kilifanya semina kadhaa, warsha, na mikutano ikilenga si tu kuimarisha ushirikiano na washirika wanaofanya kazi katika uhamiaji, bali pia kuweka mipango mahususi inayoweza kuchangia katika kuboresha utawala wa uhamiaji barani Afrika.
3. Hivyo, mwezi Julai 2023, OAM ilifanya warsha nchini Togo, ikilenga njia za utafiti na upatanisho wa data za uhamiaji. Warsha hiyo ilishuhudia ushiriki mkubwa kutoka kwa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (JUK). Baadaye, kikao kazi kilipangwa nchini Moroko kujadili mahitaji ya kuanzisha vituo vya kikanda vya data ndani ya JUK za Kiafrika.

4. Aidha, Mkutano wa COP.28 huko Falme za Kiarabu ulikuwa fursa kwa OAM kuelezea umuhimu wa data ili kutazama na kufahamu vyema mjadala muhimu kuhusu uhusiano kati ya uhamiaji na mabadiliko ya tabia nchi, hususan barani Afrika.

5. Mbali na uendeshaji kamili wa OAM, changamoto inayojitokeza sasa ni kurudia pendekezo kuu la pili la Ajenda: kuanzisha nafasi ya Mjumbe Maalum wa Umoja wa Afrika kwa ajili ya Uhamiaji.

## II. KUENDELEZA AJENDA YA UHAMIAJI YA KIAFRIKA.

1. Tangu Ufalme wa Moroko uchaguliwe kuwa nchi mwenyeji wa utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji Salama, wa Utaratibu na wa Kawaida, uitwao Mkataba wa Marrakech, haukupunguza juhudi za kuhimiza Ajenda ya Kiafrika kuhusu Uhamiaji na kupaza sauti ya Afrika kimataifa.

2. Baada ya Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri wa Nchi Mwenyeji wa Utekelezaji wa Mkataba wa Marrakech, uliofanyika Rabat Machi 25, 2022, Moroko ilikuwa mwenyeji wa mashauriano ya kimataifa kati ya jumuiya za kiuchumi za kikanda, ikijumuisha Afrika, Ulaya, na Mashariki ya Kati mnamo Januari 26 na 27, 2023; mkutano huo uliwezesha kubadilishana mawazo kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Marrakech na njia ya kuuendeleza.

3. Kufuatia mazungumzo yaliyoanzishwa huko Rabat, mazungumzo mengine ya kikanda ya ndani ya Afrika yalifanyika Accra kuanzia Novemba 28 hadi 30, 2023. Yalijadili mada muhimu za Ajenda ya Kiafrika kuhusu Uhamiaji, kama vile umuhimu wa kuwa na data za kuaminika, kukuza mazungumzo yenye uwiano, na kuunga mkono njia za uhamiaji wa kawaida.

4. Mazungumzo ya kikanda ya ndani ya Afrika pia ni fursa ya kutilia mkazo kuwa uhamiaji wa Kiafrika kwanza ni wa ndani ya kanda na unaongezeka kwa kasi. Jitihada za kuhimiza Moroko zinajitahidi kukuza usimamizi wa uhamiaji ulio na msingi wa data sahihi inayoelezea kwa uaminifu hali ya uhamiaji barani Afrika. Data inaonyesha kuwa shinikizo la uhamiaji kwa kiasi kikubwa linawekwa kwa nchi za Afrika, wakati chini ya asilimia 12 ya uhamiaji usio rasmi kwenda Ulaya unatoka Afrika. Zaidi ya hayo, data hizi zinaonyesha kuwa hakuna nchi ya Afrika inayoshika nafasi kati ya nchi kumi na tano kuu za asili za wahamiaji wa kimataifa, na hakuna kati yao inayojumuishwa kati ya njia kumi na tano kuu za uhamiaji wa kimataifa kati ya nchi mbili.

5. Pia, hii inazingatia ushirikiano wa Moroko kama mwenyeji mwenza wa shughuli za nchi mwenyeji wa Mkataba wa Marrakech. Kwa kutumika kama jukwaa la kuimarisha mshikamano kati ya Ajenda ya Kiafrika kuhusu Uhamiaji na Mkataba wa Marrakech, ushirikiano huu pia unachangia kukuza mazungumzo yenye uwiano kuhusu uhamiaji, ukipinga vikali mazungumzo yanayodhalilisha na ufupishaji wa kuchosha ambao unatumika kuwabagua wahamiaji.

6. Hatimaye, Ufalme uliandaa, kuanzia Juni 13 hadi 15, 2023 huko Rabat, Mkutano wa Tatu wa Kimataifa kuhusu Afya ya Wakimbizi na Wahamiaji. Uliandaliwa kwa ushirikiano na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), na Kamishna Mkuu wa Umoja wa

Mataifa kwa Wakimbizi (UNHCR). Mkutano huo ulipelekea kupitishwa kwa Azimio la Rabat, ambalo linatoa kichocheo halisi cha kuboresha ustawi na afya ya wakimbizi, wahamiaji, hasa barani Afrika.

## III. Afrika kama kitovu cha Mchakato wa Uhamiaji na Maendeleo

1. Mwaka 2023, Ufalme wa Moroko ulichukua uenyekiti wa Mzungumzo wa Afrika na Ulaya kuhusu Uhamiaji na Maendeleo, unaojulikana kama Mchakato wa Rabat, kwa mara ya pili. Kama mwanzilishi wa mpango huu, Ufalme wa Moroko ulitumia uenyekiti wake kama fursa mpya ya kuinua sauti ya bara la Afrika. Kupitia mwaka mzima, Moroko ilihakikisha kwamba mikutano yote iliyoandaliwa katika muktadha huu ilikuwa na uenyekiti wa pamoja wa Kiafrika na Kiulaya. Pia, ilijitahidi kuimarisha mazungumzo kati ya Afrika na Ulaya juu ya suala la uhamiaji, ikizingatia hasa umuhimu wa uhamiaji katika maendeleo.
2. Mkutano wa Kimataifa kuhusu Maendeleo na Uhamiaji uliofanyika Roma tarehe 23 Julai 2023 ulikuwa fursa kwa Ufalme wa Moroko kusambaza ujumbe wa mshikamano, uwajibikaji wa pamoja, na ushirikiano, kulingana na Ajenda ya Kiafrika kuhusu Uhamiaji. Moroko pia ilichukua fursa ya mchakato ulioanzishwa na Mkutano wa Roma kufanikisha mazungumzo kati ya Mchakato wa Rabat na Mchakato wa Roma na kwa kujenga uwezo wa uhamiaji salama, wa utaratibu na wa kawaida: kuzungumzia changamoto zake na kutumia fursa zinazotolewa, hasa kwa Afrika.
3. Kila mkutano pia ni fursa kwa Moroko kuweka mtazamo wa kibinadamu kwenye suala la uhamiaji. Moroko inaamini kwamba ukweli katika njia na uwajibikaji katika mchakato huenda sambamba na mtazamo wa kibinadamu. Kwa sababu, ufanisi wa sera ya uhamiaji inayowajibika unatokana hasa na mkusanyiko wa vipengele vya usalama na vipaumbele vya haki za binadamu.
4. Hatimaye, Ufalme wa Moroko, ambao unashiriki kikamilifu kazi za Jukwaa la Uhamiaji na Maendeleo ya Kimataifa (GFMD), unahusika sana katika maandalizi ya Mkutano wa 14 wa GFMD, uliopangwa kufanyika kuanzia tarehe 23 hadi 25 Januari 2024.

Kwa muhtasari, Mkutano wa 37 wa Viongozi wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) ni fursa mpya ya kuthamini athari kubwa na mchango muhimu wa jukumu la Mtukufu, Mfalme Mohammed wa VI, kuhusu suala la uhamiaji barani Afrika. Utekelezaji kamili wa OAM na kuongezeka kwa shughuli zake, kuimarisha mshikamano kati ya Ajenda ya Kiafrika kuhusu Uhamiaji na Mkataba wa Marrakech, nafasi muhimu ya Afrika katika mchakato wa uhamiaji na maendeleo, vinaonesha mchango huu.

## 3. MHE. ABIY AHMED, WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA DEMOKRASIA YA KIFEDERALI YA ETHIOPIA NA KINARA WA AU WA UKAGUZI WA KILA BAADA YA MIAKA MIWILI WA CAADP

# RIPOTI YA NNE YA UKAGUZI WA KILA BAADA YA MIAKA MIWILI YA UMOJA WA AFRIKA WA UTEKELEZAJI WA AZIMIO LA MALABO KUHUSU UKUAJI NA MAGEUZI YA KILIMO YALIYOSONGEZWA KWA USTAWI WA PAMOJA NA KUIMARISHA MAISHA BORA YA WATU.

(UAMUZI WA MKUTANO WA /AU/2(XXIII)) WA JUNI 2014)

## MUHTASARI

Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliidhinisha Azimio la Malabo la Mpango Kamambe wa Maendeleo ya Kilimo barani Afrika (CAADP) wa Ukuaji na Mageuzi ya Kilimo kwa Ustawi wa Pamoja na Kuimarisha Maisha Bora ya Watu mwezi Juni 2014 huko Malabo, Guinea ya Ikweta. Azimio hilo limejulikana sana kama Azimio la Malabo. Chini ya ahadi nambari saba ya azimio la Uwajibikaji wa Pamoja kwa Vitendo na Matokeo, Viongozi wa Kiafrika waliamua: kufanya Mapitio ya Kilimo ya kila baada ya miaka miwili ambayo yanajumuisha, kufuatilia na kuripoti maendeleo ya utekelezaji wa masharti ya azimio. Kwenye Wito wa Hatua, Viongozi wa Kiafrika waliiomba Kamisheni ya AU na Shirika la UNECA (NPCA), sasa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD), kwa kushirikiana na washirika: kufanya Mapitio ya Kilimo kila baada ya miaka miwili, kuanzia mwaka 2017, na kuripoti maendeleo kwenye Mkutano mkuu wakati wa Mkutano wa kawaida wa Januari 2018.

Kama ilivyoagizwa na Mkutano wa AU, AUC na AUDA-NEPAD wamekuwa wakitoa ripoti ya ukaguzi wa CAADP kila baada ya miaka miwili tangu mwaka 2017. Kwa kweli, ripoti ya kwanza ya ukaguzi wa CAADP iliwasilishwa kwenye Mkutano wa AU mwezi Januari 2018 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Ethiopia ambaye alikuwa, mwaka 2017, ametajwa kuwa Kiongozi wa CAADP. Tangu wakati huo ripoti imekuwa ikizalishwa na kuwasilishwa kwenye Mkutano wa AU kila baada ya miaka miwili, bila kukosekana. Mwezi Februari 2024, Waziri Mkuu wa Ethiopia, Mhe. Abiy Ahmed, katika jukumu lake kama Kiongozi wa CAADP, atawasilisha Ripoti ya Nne ya Ukaguzi wa Kila Baada ya Miaka Miwili ya CAADP kwenye Mkutano Mkuu wa AU.

Ripoti ya ukaguzi wa CAADP inatoa picha na mwelekeo wa mageuzi ya kilimo barani Afrika kwa kipindi cha 2015 - 2025, ndani ya muundo wa CAADP, kama chombo cha kuchangia katika kufikia malengo ya Mpango wa Miaka Kumi wa Kutekeleza Ajenda 2063 ya Afrika. Katika ripoti hii, nchi arobaini na tisa (49) ziliripoti, pungufu kutoka nchi 51 zilizoripoti kwenye ripoti ya tatu ya ukaguzi wa CAADP mwaka 2021.

Ripoti inaonyesha kwamba hakuna nchi inayoendelea vizuri kwenye awamu ya nne ya ukaguzi wa CAADP. Walakini, nchi 26 zimeona alama zao zikiboreshwa tangu awamu ya tatu ya ukaguzi wa miaka miwili mwaka 2021. Mbali na dharura ya kujenga sekta imara ya kilimo barani Afrika kama ilivyoelezwa wakati wa Ukaguzi wa Tatu wa Miaka Miwili, ripoti hii inasisitiza umuhimu wa kuharakisha utekelezaji wa

Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA). Inatarajiwa kwamba hii itachochea mazingira mazuri na uwekezaji kwaajili ya ajenda ya mageuzi ili kuleta faida iliyokusudiwa kama ilivyoelezwa katika Mpango wa Uwekezaji wa Kilimo wa Kitaifa (NAIPs) na Mpango wa Uwekezaji wa Kilimo wa Kikanda (RAIPs).

**4. MHESHIMIWA ABDEL FATTAH EL-SISI, RAIS WA JAMHURI YA KIARABU YA MISRI, KINARA WA UMOJA WA AFRIKA WA KUFUFUA NA KUTEKELEZA KWA VITENDO SERA YA UMOJA WA AFRIKA YA UJENZI NA MAENDELEO BAADA YA MIZOZO (PCRD).**

**<u>Mapitio ya Sera ya Umoja wa Afrika ya Ujenzi na Maendeleo Baada ya Mizozo.</u>**

- Ninafurahi kutoa ripoti juu ya maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa maagizo ya Mkutano wa Umoja wa Afrika na Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kuhusu umuhimu wa mapitio ya Sera ya Umoja wa Afrika ya Ujenzi na Maendeleo Baada ya Mizozo (AU PCRD), iliyoamuliwa wakati wa Mkutano wa Kawaida wa 9 uliofanyika Banjul mnamo tarehe 28-29 Juni 2006.
- Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika (PSC), katika kikao chake cha 670 cha Machi 2017, kilisisitiza kuwa upande wa PCRD bado ni "kiungo dhaifu" katika utekelezaji wa Mimarathi ya Afrika ya Amani na Usalama (APSA) na Mimarathi ya Utawala wa Afrika (AGA). Katika kikao chake cha 1047, iliiomba kuwa sera ya AUPCRD ifanyiwe mapitio ili kukabiliana na mazingira ya usalama yanayoendelea kubadilika, ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa AU PCRD ili kutokomeza kabisa kujirudia kwa mizozo, na kupachika vipengele vya ujenzi wa amani. Hili lilijirudia katika Uamuzi wa Mkutano wa AU 815 (XXXV) wa tarehe 6 Februari 2022, pamoja na Uamuzi wa Mkutano wa AU 842(XXXVI) wa tarehe 18-19 Februari 2023.

- Ninaipongeza Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa kuchukua hatua za haraka kuhusu jukumu hili, kupitia uteuzi wa kundi la Wataalamu mwezi Machi 2022, na kuitisha warsha huko Accra mwezi Septemba 2022, ambayo ilipendekeza kuongezwa kwa nguzo mbili mpya zinazohusu Mazingira' na 'Vijana' kati ya nguzo sita zilizopo za sera ya PCRD: Uongozi wa Kisiasa; Usalama; Haki za Binadamu; Haki za Mageuzi na Upatanishi; Ujenzi na Maendeleo ya Kiuchumi na Jamii; Jinsia; na Msaada wa Kibinadamu na Dharura. Juhudi hizi pia zilipokelewa vyema na Mkutano wa Kawaida wa AU katika mkutano wake wa 36, ambao uliiomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuhitimisha mapitio hayo mwaka 2023.
- Kufuatia maagizo yangu, kama Kinara wa Umoja wa Afrika wa Ujenzi na Maendeleo Baada ya Mizozo Barani Afrika, Wizara ya Mambo ya Nje ya Misri ilikuwa mwenyeji wa Warsha ya pili ya Kitaifa ya Mafunzo ya Umoja wa Afrika kuhusu Mapitio ya Sera ya Umoja wa Afrika ya Ujenzi na Maendeleo Baada ya Mizozo, kuanzia tarehe 30 Mei hadi 1 Juni, 2023 mjini Cairo, kwa kushirikiana na Tume ya Umoja wa Afrika, Wakala wa Maendeleo wa Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD) na Kituo cha Kimataifa cha Cairo cha Kutatua Migogoro, Kulinda Amani na Kujenga Amani (CCCPA).

- Warsha hiyo ilimaliza mapitio ya Sera ya AU - PCRD kwa mafanikio na kupendekeza kupanua wigo wake ili kushughulikia mizozo yote. Sera iliyorekebishwa inalenga kuimarisha ushirikiano wa operesheni kati ya Mimarathi husika ya sera za AU na jitihada za kikanda, pamoja na mjadala unaoendelea wa kimataifa kuhusu ujenzi wa amani na kudumisha amani, ikiwa ni pamoja na kutumia njia ya pamoja. Kwa minajili hiyo, nilipendekeza kubadilisha jina la sera na vyombo na miundo husika ya AUC, ikiwa ni pamoja na Kituo cha AU kwa PCRD, kuwa Kituo cha AU cha Ujenzi wa Amani, Ujenzi na Maendeleo (PBRD).
- Mapitio haya yanaashiria hatua muhimu na wakati muafaka kwa Afrika kuifikia amani endelevu na maendeleo, haswa wakati inalingana na jitihada zetu za pamoja za kukamilisha mpango wa miaka kumi wa utekelezaji wa Ajenda 2063. Kwa hivyo, nashauri Mkutano ujao wa AU uridhie matokeo ya warsha ya Cairo pamoja na sera iliyorekebishwa.
- Kuwianishwa kwa Kituo cha Umoja wa Afrika kuhusu Ujenzi na Maendeleo Baada ya Mizozo (AUC PCRD)
- Misri pia imeshirikiana  kwa karibu na Kamisheni ya Umoja wa Afrika ili kuianzisha kikamilifu Kituo cha AU cha PCRD, ambacho ni hatua muhimu katika jitihada za Afrika za kuimarisha amani na kuleta maendeleo endelevu na kuongeza umiliki wa Afrika wa ajenda zake za amani na maendeleo.
- Katika suala hili, ninapongeza uteuzi wa mkurugenzi mtendaji wa AUC - PCRD na natumai kumaliza zoezi la kuajiri wafanyakazi wengine wa Kituo, ili kuwezesha Kituo kuongoza utekelezaji wa Sera iliyorekebishwa ya AU PCRD / AU PBRD kupitia kutoa majibu ya mahitaji na vipaumbele vya ujenzi wa amani barani Afrika.
- Kama Kinara wa PCRD, niliagiza Serikali ya Misri kutoa msaada wote unaohitajika kwenye Kituo cha AU cha PCRD kinachochipukia, ikiwa ni pamoja na kujenga makao makuu ya Kituo kwenye mji mkuu mpya wa utawala wa Misri, ambao utakuwa tayari kuzinduliwa  hivi karibuni.
- Katika kusonga mbele, natarajia kujihusisha zaidi na AUC - PCRD katika kutekeleza maamuzi yote yanayohusiana na shughuli za ujenzi wa amani barani Afrika.
- Kusonga mbele kwa ushirikiano wenye ufanisi na wenye matokeo Chanya ya  kudumisha amani
- Kama sehemu ya jitihada zangu za kusonga mbele kwa njia kamili na iliyoundwa vizuri kuhusu amani na usalama barani Afrika, ikiwa ni pamoja na ushirikiano wenye tija, Wizara ya Mambo ya Nje ya Misri, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Kituo cha Kimataifa cha Cairo cha Kutatua Mizozo, Kulinda Amani na Kujenga Amani (CCCPA), ilikutana kwenye Mkutano wa 14 wa Wataalamu wa  Mitaala Maalumu na Wawakilishi ili Kuchagiza Amani, Usalama na Utulivu barani Afrika huko Cairo, Misri, kuanzia tarehe 17 hadi 18 Oktoba 2023.
- Mkutano huo uliwakutanisha pamoja uongozi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Wawakilishi na Mabalozi Maalumu kutoka mashirika ya kimataifa na kikanda, ikiwa ni pamoja na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Ulaya (EU), pamoja na Wakuu wa Taasisi za AU na Ofisi za Uhusiano wa AU, na Jopo la Wazee wenye Hekima. Iliwapa fursa ya pekee ya kutafakari umuhimu wa kutanguliza na kuiimarisha diplomasia ya kuzuia

migogoro na mazungumzo ili iwe kitovu cha vipaumbele vya Umoja wa Afrika kote barani, pamoja na kukuza ushirikiano wa kimkakati unaotumia faida linganifu ya wadau wote ili kuhakikisha kuwa kazi zao zinakamilishana. Kumbukumbu ya wiki ya tatu ya Ujenzi na Maendeleo Baada ya Mizozo ya Umoja wa Afrika

- Katika muktadha wa kumbukumbu ya wiki ya tatu ya Umoja wa Afrika ya Ukarabati na Maendeleo Baada ya Mizozo, nilitangaza uzinduzi wa "Tuzo ya Jukwaa la Aswan kwa ajili ya Ujenzi na Maendeleo Baada ya Mizozo (PCRD)" ili kutambua na kuibua masuluhisho na majibu ya Kiafrika kwa changamoto za ujenzi wa amani ambazo ni kipaumbele zaidi barani Afrika.
- Kwa kusudi hilo, wito wa uteuzi ulitolewa wakati wa wiki ya Ukarabati na Maendeleo Baada ya Mizozo mwezi Novemba 2023. Tuzo hiyo itakuwa ya kuheshimu mtu, shirika, mpango au mradi wa Kiafrika ambao umetoa mchango mkubwa katika kufuatilia amani, usalama na maendeleo katika jamii, nchi au eneo husika la bara la Afrika. Itakabidhiwa wakati wa toleo la 4 la Jukwaa la Aswan mnamo 2024.

## 5. MHESHIMIWA FAURE ESSOZIMNA GNASSINGBE, RAIS WA JAMHURI YA TOGO NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA JUU YA SAATM

Mradi kabambe wa Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika, MUTAA ulizinduliwa wakati wa Mkutano wa 30 wa Kawaida wa Mkutano Mkuu wa Viongozi wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika tarehe 28 na 29 Januari 2018 huko Addis Ababa, Ethiopia.

MUTAA, ambao ni utekelezaji halisi wa nia ya kisiasa ya viongozi wa Kiafrika, bila shaka una faida kadhaa kwa bara zima, ikiwa ni pamoja na uundaji wa ajira mpya, ongezeko la Pato la Taifa, kuboresha mawasiliano kwa kufungua njia mpya za usafiri, kupunguza gharama za tiketi za ndege, na kuchagiza ushirikiano kati ya makampuni ya ndege.

Mwaka 2015, wakati wa kupitishwa kwa tamko la kuanzisha Soko Moja la Usafiri wa Anga barani Afrika (MUTAA), nchi kumi na moja (11) wanachama wa Umoja wa Afrika walitangaza ahadi yao ya dhati ya kuunda Soko Moja ifikapo mwaka 2017. Wakati wa uzinduzi wa soko hilo mwaka 2018, idadi ya nchi zilizosaini ahadi ya dhati ilikuwa ishirini na tatu (23). Hadi leo, idadi hiyo imeongezeka hadi thelathini na saba (37), ikionyesha zaidi ya 88% ya safari za ndege ndani ya Afrika na zaidi ya watu milioni 800 barani Afrika.

Kwa kuharakisha utekelezaji wa MUTAA, Mradi wa majaribio ya utekelezaji wa MUTAA (SAATM Pilot Implementation Project) ulizinduliwa tarehe 14 Novemba 2022 huko Dakar. Mradi huu una lengo la kuhamasisha nchi wanachama wote kuharakisha utekelezaji wa Uamuzi wa Yamoussoukro wa MUTAA, na kwa sasa una jumla ya nchi ishirini (20).

Rais wa Jamhuri ya Togo, Mheshimiwa Faure Essozimna GNASSINGBE, Kinara wa MUTAA, anaendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kwamba Nchi zote za Afrika zinajiunga. Pia, amechukua hatua kadhaa kwa lengo la kupata uungaji mkono kutoka kwa tasnia ya anga na taasisi za kifedha kwa ajili ya ufadhili wa mradi huo. Hivyo, amepata ufadhili wa dola milioni 7 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ili kusaidia CAFAC, ambacho ni chombo cha utekelezaji wa DY/MUTAA.

Katika kutekeleza mchakato wa kuanzisha MUTAA, hatua muhimu za kufanya ni:

Kuendelea na kampeni ya kuzishawishi nchi zingine wanachama wa Umoja wa Afrika kujiunga,

• Kuandaa mkutano wa sita wa kikundi kazi cha mawaziri wanaohusika na utekelezaji wa MUTAA kwa lengo la kukiongezea muda wake wa uongozi,

• Kuendelea na mapitio ya mikataba ya anga kati ya nchi wanachama ili kujiridhisha kuwa inalingana na maamuzi ya Yamoussoukro,

• Kuhimiza makampuni ya ndege ya Afrika kusaini mikataba ya kibiashara kama vile makubaliano ya kugawana nambari za ndege na mikataba ya ushirikiano ili kurahisisha usafiri wa abiria

## 6. MHESHIMIWA TEODORO OBIANG NGUEMA MBASOGO, RAIS WA JAMHURI YA GUINEA EKWATORIALI, KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU WAKIMBIZI

La República de Guinea Ecuatorial, cuyo lema es Unidad, Paz y Justicia y cuya constitución garantiza la protección de los derechos fundamentales de las personas que viven en todo su territorio nacional, es un país de Paz, donde reina el espíritu de respecto a las personas, panafricanismo y solidaridad humana.
Es precisamente la ideología y los principios que siempre ha definido el Presidente de la Republica, Jefe de Estado, Su Excelencia Obiang Nguema Mbasogo en su calidad de garante de la Paz y la estabilidad del país.
Esta voluntad del Presidente Obiang Nguema Mbasogo de ver un mundo cada vez mejor le ha convertido en el leit motif de la República de Guinea Ecuatorial y el país asume por consiguiente su deber moral en su rol de Embajador.
Al asumir en 2019 el liderazgo de la Unión Africana para cuestiones de refugiados, repatriados y desplazados internos, año caracterizado por la celebración del el Cincuenta (50) Aniversario de la Convención OUA de 1979 y el Décimo (10) Aniversario de la Convención de Kampala, la presidencia de la República de Guinea Ecuatorial se comprometió a trabajar estrechamente con ACNUR y la Unión Africana para establecer mejores Estándares para el tratamiento de los refugiados en los países receptores y al mismo tiempo trabajar con los países de origen para incrementar la cooperación solidaridad entre las naciones afectadas. La asunción de la responsabilidad de Guinea Ecuatorial como campeón de la Unión Africana llevo a

Su Excelencia Obiang Nguema Mbasogo, Presidente de la República de Guinea Ecuatorial, Jefe de Estado a visitar dos campos de refugiados en Uganda y Etiopia respectivamente.
Las condiciones devastadoras de estos campos motivaron al Presidente Obiang Nguema Mbasogo apoyar económicamente la construcción de una escuela primaria a los niños y niñas del campo de refugiados en la localidad de Tsore (Etiopia).
A tal efecto, el Presidente hizo un llamamiento a la urgente necesidad de soluciones ante los conflictos armados, buscar los asentamientos de las personas desplazadas, la inseguridad política, problemas del terrorismo y piratería, entre los principales males que azotan al continente africano.
En el mes de mayo de 2022, la República de Guinea Ecuatorial albergo la cumbre Humanitaria Extraordinaria de la Unión Africana y Conferencia de Donantes.

Durante las deliberaciones de la misma, los participantes han puesto de relieve la gravedad de estas situaciones, que contribuye sistemáticamente al estancamiento de los países africanos.
En su alocución, el Presdente Obiang Nguema Mbasogo participo a la audiencia que África, como fuente de la antigua sabiduría, no puede quedarse impotente para alcanzar su desarrollo por situaciones causadas por factores internos y externos. Prosiguió diciendo que África debe emprender solidariamente la lucha de su emancipación, para caminar en la unidad y solidaridad de todos, para recuperar la integridad de las Naciones.
Para ello, se debe evitar los vicios individuales, el poco respeto a los Derechos Humanos y demás factores.
La República de Guinea Ecuatorial se felicita por el creciente número de Estados Africanos que han ratificado y domesticado la Convención de Kampala, la cual es el primer y único instrumento regional jurídicamente vinculante para protección y asistencia de las personas desplazadas internamente, quienes a menudo se encuentran expuestas a mayores peligros de sufrir todo tipo de violencia y prohibidos en ejercer sus derechos fundamentales.
Considerando que el tratamiento y gestión de refugiados y de desplazados internos es un tema de alta relevancia global, impactando a millones de personas y sus países de acogidas; Guinea Ecuatorial aunque no enfrenta una crisis de desplazamientos ha estimado necesario adoptar una política clara de gestión para estar preparada ante cualquier eventualidad. Este enfoque práctico se basa en la comprensión de la volatilidad global y en el compromiso con los principios humanitarios Internacionales.

Es así como que el Gobierno de la República de Guinea Ecuatorial, en su Consejo de Ministros, adopto la creación de la Oficina de Gestión para Refugiados, Apátridas, Desplazados Internos y Retornados en Guinea Ecuatorial. La creación de la oficina demuestra el compromiso de Guinea Ecuatorial Con sus obligaciones internacionales y el cumplimiento de los requisitos globales, fortaleciendo su reputación como actor global responsable y contribuyente en la comunidad internacional.

Al establecer esta oficina, el país muestra un compromiso productivo con los principios humanitarios y sus obligaciones internacionales, posicionándose como un actor global compasivo y responsable. Cabe indicar que en ese mismo espíritu, la

República de Guinea Ecuatorial ya manifestó a la Comisión de la Unión Africana su voluntad de postular para albergar la Sede Humanitaria.

En términos de cifras, Guinea Ecuatorial ha venido contribuyendo en los programas de ayudas a los países africanos como los treinta millones de dólares ofrecidos a la FAO por la seguridad alimentaria, dos millones de dólares para Mozambique por su catástrofe natural u dos millones de dólares de contribución humanitaria.

7. **MHESHIMIWA PAUL KAGAME, RAIS WA JAMHURI YA RWANDA, KINARA WA UMOJA WA AFRIKA WA UGHARAMIAJI WA AFYA KWA KUTUMIA FEDHA ZA NDANI.**

**Mkutano wa Uongozi wa Afrika - Uwekezaji kwenye Afya (ALM)** ulizinduliwa kando ya Mkutano wa 32 wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Afrika pamoja na Mheshimiwa Rais wa Rwanda, kwa ushirikiano na washirika wa kimataifa. Azimio la ALM liliidhinishwa baadaye na Mkutano wa Umoja wa Afrika. Lengo ni kuongeza uwekezaji wa ndani katika sekta ya afya, na uongozi na uwajibikaji wa nchi ili kutimiza lengo hili.

**AUDA-NEPAD inashiriki** utekelezaji wa ALM, ikizingatia kuweka na kutekeleza Vituo vya Fedha za Afya vya Kikanda (RHFH), na kuratibu mfumo wa ushiriki wa sekta binafsi. Mafundisho muhimu, mafanikio, na ahadi za baadaye za AUDA-NEPAD katika kuendeleza ajenda ya ALM zinafuata**.**

**Mfumo wa Kufuatilia Maendeleo ya Fedha za Afya.** Zana hii ina mchango kwenye Kadi ya Alama ya Afrika iliyoidhinishwa na Mkutano wa Umoja wa Afrika (2016), na mchakato wa Kuchochea wa Kimataifa. Mfumo huu unaelekeza Nchi Wanachama namna ya kuboresha usimamizi wa kifedha wa umma, kuongeza uwekezaji wa ndani katika sekta za afya, na kutenga, kukusanya na kutumia kwa ufanisi rasilimali fedha. Mwaka 2022, AUDANEPAD na AUC waliendesha warsha ya kukagua majaribio ya Mfumo huu kwenye nchi zilizochaguliwa. Wadau walitoa maoni kuhusu zana hiyo, ikiwa ni pamoja na jinsi ya kurekebisha viashiria vyake.

**Vituo vya Fedha za Afya vya Kikanda (RHFHs).** AUDA-NEPAD ilipewa jukumu na Mkutano wa Umoja wa Afrika la kuratibu kubuni, kuanzisha na kuendesha RHFHs, ambazo lengo lake ni kukusanya rasilimali fedha kwaajili ya afya, kuboresha mgawo wa bajeti na kuimarisha ushirikiano kati ya washirika**. AUDA-NEPAD pamoja na AUC, Ofisi** ya Kinara/Mwenyekiti, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, Mfuko wa Dunia na wengine: (i) waliandaa mwongozo wa mfumo na uendeshaji wa RHFHs, (ii) waliunda na kuendesha majaribio mawili ya RHFHs kwenye jumuiya za SADC na EAC, (iii) waliendeleza ushirikiano na Jumuiya nyingine za Kiuchumi za Kikanda kama vile (ECOWAS, IGAD), (iv) waliandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli, na (v) waliandaa mfumo wa ushiriki wa sekta binafsi.

**Kadi ya Alama ya Afrika {scorecards}.** Umoja wa Afrika ulikamilisha utaftaji wa kadi ya alama ya Afrika kuhusu ufadhili wa ndani wa afya, inayopatikana mtandaoni katika lugha zote rasmi za AU (score-card.africa).

**Mazungumzo ya Kitaifa juu ya Fedha za Afya.** AUDA-NEPAD iliwezesha mazungumzo ya kitaifa ambayo yanatumika kama majukwaa ya majadiliano ya wadau wengi. Matokeo yake ni Mpango wa Msaada wa Kiufundi unaotoa mwelekeo wa Nchi kuelekea kwenye mageuzi ya kugharamia afya. Mazungumzo hayo yamefanyika Malawi (2022) na Zambia, Kenya, Msumbiji, Mauritius (2023). Yalihusisha Wizara za Fedha na Afya, sekta binafsi na AZAKI za kiraia.

**Athari na mafunzo muhimu ya utekelezaji wa shughuli za ALM.** Shughuli hizo na mazungumzo ya kitaifa hasa, yamekuwa na athari chanya katika ngazi za kikanda na kitaifa. Miongoni mwa mambo mengine, yameinua ufadhili wa afya wa ndani kama kipaumbele cha kitaifa katika maeneo ya majaribio, na kukuza juhudi za kulinganisha ufadhili uliogawanyika wa afya na Ajenda ya ALM ya bara, na kutumia maarifa yaliyopatikana kwenye mazungumzo ili kuboresha mipango ya nchi nyingine. Ni muhimu kuelewa kwamba kutekeleza mageuzi ya ufadhili wa afya kwa mafanikio kunahitaji kufuatilia kwa karibu, uwezo wa mageuzi, na msaada wa kiufundi. Pia, uongozi na umiliki wa bodi za uongozi za kikanda ni muhimu katika kujenga miundombinu ya RHFH yenye ufanisi.

**Changamoto za utekelezaji**. Raslimali za kifedha ni kikwazo kikuu katika utekelezaji wa ajenda ya ALM. Kuandaa mazungumzo ya ufadhili wa afya kunahitaji rasilimali nyingi, vilevile kusaidia utekelezaji wa mipango ya msaada wa kiufundi, kwani fedha hazipatikani au hazitoshi. Kwa hivyo, RHFHs lazima zihimize Nchi Wanachama kuonyesha umiliki kwa kutenga rasilimali kwa ajili ya mazungumzo ya kitaifa na utekelezaji wa RHFHs. Mwisho, ushirikiano na wizara na taasisi za serikali ili kuhakikisha ushiriki wa wadau muhimu ni changamoto, ambayo inahitaji ushiriki mkubwa katika ngazi ya juu kabisa**.**

**Ahadi za baadaye.** Kufuatia mamlaka yake ya kuanzisha RHFHs kwenye kanda zake tano za Afrika na kusaidia ufadhili wa afya, AUDA-NEPAD itaendelea kusonga mbele na malengo ya ALM kupitia: (i) ushiriki wa wadau, (ii) kuzijengea uwezo jumuiya za kiuchumi za kikanda, (iii) msaada wa kiufundi kwaajili ya upanuzi wa RHFHs kwenye jumuiya zingine za kikanda, (iv) kuandaa ripoti ya kila mwaka ya ALM kwaajili ya Mikutano ya AU, (v) kuweka mfumo wa ushiriki wa sekta binafsi katika ngazi ya kitaifa na kikanda, (vi) kusaidia Mazungumzo ya Kitaifa ya Ufadhili wa Afya, (vii) kutunza kumbukumbu kwa maandishi juu ya mafunzo yaliyopatikana kutokana na uendeshaji wa RHFHs, (viii) kujumuisha Mfumo wa Kufuatilia Ufadhili wa Afya katika mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini, (ix) kutumia azaki za kiraia katika ufadhili wa afya, na (x) kuboresha usimamizi wa mageuzi ya ufadhili wa afya kupitia mikutano ya mazungumzo na maafisa wa afya, Mawaziri wa Afya, na Mawaziri wa Fedha. **MWISHO.**

## 8. MHE. FELIX ANTOINE TSHISEKEDI TSHILOMBO, RAIS WA JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA WA TAASUBI YA KIUME CHANYA.

Kama Kinara wa Umoja wa Afrika wa Taasubi ya Kiume Chanya, Mheshimiwa Félix Antoine TSHISEKEDI TSHILOMBO, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, amechukua hatua kadhaa katika ya kitaifa na bara la Afrika kwa lengo la kupambana na ukatili dhidi ya wanawake barani Afrika.

I. Kitaifa

Kwa lengo la kuhamasisha wadau mbalimbali kuchukua hatua kuhusu Azimio la Kinshasa lililopitishwa tarehe 25 Septemba 2021, na kuingiza jinsia kwenye sera na programu, hatua kadhaa zimechukuliwa, ikiwa ni pamoja na:

- Kuandaa kampeni za kuelimisha na kuongeza uwezo katika vyuo vikuu 4 jijini Kinshasa, Jimbo la Haut-Katanga, na Jimbo la Kongo Central;
- Kuendelea na kampeni ya "Uvumilivu sufuri mara moja" dhidi ya ukatili wa kijinsia (ambapo Mpango wa Hatua unafanyiwa mapitio kamili);
- Kuunda Kituo cha Pamoja cha Kisekta cha kusaidia waathirika wa ukatili wa kijinsia...

II. Barani Afrika

Hatua nne kuu zimechukuliwa, ikiwa ni pamoja na:

- Ushawishi kwa Serikali ya Guinea ya Ikweta na Botswana, kwa lengo la kupitisha Mkataba wa AU wa Kukomesha Ukandamizaji dhidi ya Wanawake na Wasichana;
- Kuandaa mashauriano na viongozi wa kimila na kidini;
- Kushiriki katika mashauriano ya viongozi wa wanawake huko Moroni (Comoros);
- Kushiriki katika Mkutano wa Tatu wa Wanaume kuhusu Taasubi ya Kiume Chanya mwezi Novemba 2023 (RSA).

Ni muhimu kutambua kwamba utekelezaji wa Azimio la Kinshasa umekumbana na changamoto kadhaa kubwa. Hizi ni pamoja na vikwazo vya kitamaduni pamoja na rasilimali za kifedha zinazohitajika, ikizingatiwa ukubwa wa bara la Afrika. Aidha, baadhi ya nchi za Afrika zimechelewa kuweka mifumo ya kisheria, sera, na programu za kuendeleza haki za wanawake.

III. Matarajio

Ni muhimu:

Kuendelea na kampeni ya elimu na ufahamu kupitia mikutano na wadau wote na viongozi mbalimbali barani Afrika;
Kuendelea na shughuli za kisiasa kwa viongozi wa nchi, kwa lengo la kupitisha Mkataba wa AU wa Kukomesha Ukandamizaji dhidi ya Wanawake na Wasichana.

## 9. MUHTASARI WA MUSWADA WA RIPOTI YA PILI YA MHESHIMIWA JOÃO MANUEL GONÇALVES LOURENÇO, RAIS WA JAMHURI YA ANGOLA NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA WA AMANI NA MARIDHIANO BARANI AFRIKA, MACHI 2023 - JANUARI 2024

1. O presente Sumário Executivo, sistematiza o relatório das principais actividades desenvolvidas, entre Março de 2023 a Janeiro de 2024, no âmbito do meu mandato como Campeão da União Africana para a Paz e Reconciliação em África e mediador para desanuviar as tensões políticas, diplomáticas e de segurança entre a República Democrática do Congo (RDC) e a República do Ruanda. O exercício deste mandato está em conformidade com a decisão da 16.ª Sessão Extraordinária da Conferência dos Chefes de Estado e de Governo da União Africana (UA), sobre o Terrorismo e as Mudanças Inconstitucionais de Governo em África, realizada em Malabo, República da Guiné Equatorial, aos 28 de Maio de 2022.

2. No período em referência, dediquei esforços na coordenação e colaboração de várias iniciativas sub-regionais, regionais e ao nível do continente, com vista a contribuir para a prevenção, gestão e resolução pacífica dos conflitos prevalecentes particularmente, na Região dos Grandes Lagos, onde persiste a tensão entre a RDC e o Ruanda, o conflito na RCA, no Sudão e no Sudão do Sul. Por outro lado, registou-se igualmente a contribuição de outros actores regionais e continentais visando igualmente contribuir para a estabilidade em países, como Burquina Faso, Etiópia, Gabão, Guiné, Líbia, Mali, Moçambique, Níger e Somália.

3. No âmbito das iniciativas que liderei, sobretudo na região dos Grandes Lagos (Central) e na Região Austral de África, destaco os esforços de paz e reconciliação desenvolvidos pelas Cimeiras realizadas em Luanda, de Fevereiro e Junho de 2023, e que contribuíram para:

    a) A cessação das hostilidades na região Leste da RDC e a imposição de um cessar-fogo com o M-23;

    b) A adopção e implementação do **Plano de Acção Conjunto sobre a Resolução da Crise de Segurança na região leste da RDC**, bem como atenuar o clima de tensão e normalizar as relações político-diplomáticas entre a RDC e o Ruanda;

    c) Harmonizar e coordenar os processos de Luanda e Nairóbi;

    d) Apoiar o desdobramento pleno da Força Regional da Comunidade da África Oriental (CAO);

    e) Garantir o regresso dos refugiados às zonas de origem;

f) Estabelecer o Mecanismo Quadripartido integrando a CAO, CEEAC, CIRGL e SADC, sob os auspícios da UA e a participação das Nações Unidas, para coordenar e harmonizar as iniciativas de paz na região leste da RDC;

g) Facilitar o desdobramento da Força em Estado de Alerta da SADC, na RDC (SAMIRDC);

h) No âmbito da Presidência Rotativa da SADC, iniciei em Dezembro de 2023, a um processo de ***apaziguamento e reconciliação*** entre Sua Excelência **Dr. Mokgweetsi Masisi**, Presidente da República do Botsuana e o seu antecessor, Sua Excelência Tenente-General **Khama Ian Khama,** antigo Presidente daquele mesmo País. Um relatório detalhado será apresentado oportunamente.

i) Consolidar a comemoração pela segunda vez, do 31 de Janeiro como **Dia da Paz e Reconciliação em África**, uma responsabilidade partilhada que exige o contributo de todos os cidadãos africanos, jovens e velhos, homens e mulheres, para a manutenção da coesão e unidade social.

4. No âmbito da agenda do Campeão e das acções do **Fórum Pan-Africano para Cultura de Paz e Não-Violência "Bienal de Luanda"** realizou-se, em Luanda, em Maio de 2023, o **1.º Fórum Internacional da Mulher para a Paz e Democracia**, sob o lema **"Inovação Tecnológica como Ferramenta para o Alcance da Segurança Alimentar e Combate à Seca no continente africano"**. Este Fórum visou promover acções conducentes à paz e reconciliação continental, tendo no centro a liderança da mulher no processo de manuteção da paz e consolidação da democracia.

5. Por outro lado, Angola, em colaboração com União Africana e a UNESCO realizou em Novembro de 2023, em Luanda, a **3.ª Edição da Bienal de Luanda**, sob o tema **"Educação, Cultura de Paz e Cidadania Africana como Ferramentas para o Desenvolvimento do Continente"**, com o objectivo de promover a paz, prevenir a violência, fomentar a resolução pacífica de conflitos e o incentivo ao intercâmbio cultural em África e o diálogo intergeracional.

6. Muitos esforços foram empreendidos para a resolução pragmática e duradoura dos conflitos em África, mas continua a ser necessário a colaboração e a participação das partes interessadas, para que a mediação seja eficaz.

7. Continuarei a colaborar e a partilhar as minhas experiências enquanto Campeão da UA para a Paz e Reconciliação em África, para a promoção da paz e estabilidade no Continente, pelo que conto com o apoio da UA, das Comunidades Económicas Regionais (CERs) e dos Mecanismos Regionais

(MRs), bem como dos parceiros internacionais, no exercício pleno do meu mandato.

**10. NANA ADDO DANKWA AKUFO-ADDO, RAIS WA JAMHURI YA GHANA, KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU TAASISI ZA FEDHA ZA AU."**

1. Hii ni ripoti yangu ya nne tangu mwaka 2020 kuhusu jukumu la kihistoria la kuanzisha Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika, yaani: Benki Kuu ya Afrika, Mfuko wa Fedha wa Afrika, Benki ya Uwekezaji ya Afrika na Soko la Hisa la Kimajumuyi. Nitawasambazia, kwa nyakati tofauti, Maamuzi Matatu ya Mkutano Mkuu.
2. Awali ya yote, naomba nizungumzie umuhimu wa kuwekeza akiba katika Taasisi za Fedha za Kikanda za Afrika. Kwa sasa, taasisi nyingi za kifedha zina amana nje ya nchi zinazopelekea kupata viwango hasi vya riba. Kuweka fedha hizo kutawezesha taasisi za kifedha za kikanda za Afrika kuzitumia kwa kuongeza mkopo wao katika masoko ya mtaji ya kimataifa kwa ajili ya kukopesha sekta binafsi na za umma za Afrika hivyo kuongeza uwekezaji katika bara letu. Napendekeza Mkutano Mkuu upitishe maamuzi ya rasimu kuhusu suala hili.
3. Pia ninatoa pendekezo la kuanzisha Mkutano Mkuu wa Kiuchumi wa Afrika. Hii itatoa fursa ya kuwa mazungumzo ya kimkakati kati ya nchi za Afrika, viongozi wa kisiasa na kibiashara duniani pamoja na wafadhili wa sera na mipango ya Afrika kwaajili ya ukuaji jumuishi na endelevu. Mkutano uliopendekezwa pia utashughulikia mwenendo wa sasa ambapo viongozi wa Kiafrika hushiriki mikutano mingi kila mwaka kuhusu Afrika katika nchi nyingi duniani. Tena, napendekeza Mkutano Mkuu upitishe rasimu ya maamuzi kuhusu suala hili.
4. Kuhusu uanzishwaji wa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika, nitaanza na Benki Kuu ya Afrika. Maendeleo ya utekelezaji wa vigezo vya umoja wa kiuchumi wa Afrika (AMCP) ni hafifu. Bado tupo nyuma sana kufikia viwango vilivyokubaliwa. Tunahitaji kufanya kazi kwa bidii zaidi. Kufikia umoja wa kiuchumi na upangaji sahihi wa sera za kiuchumi na kifedha sasa imekuwa muhimu zaidi kutokana na uanachama wetu wa kudumu kwenye G20. Ili tuzungumze kwa sauti moja kwenye G20, tunahitaji sera na mipango ya kiuchumi na kifedha inayoratibika.
5. Kuna kazi inaendelea pia kuhusu rasimu ya Katiba ya Taasisi ya Fedha ya Afrika. Wataalamu wetu hawajafikia muafaka kuhusu Rasimu ya Katiba ya Taasisi ya Fedha ya Afrika na wanahitaji muda kwaajili ya mashauriano zaidi. Ninaziomba nchi wanachama kufanya mashauriano ya mwisho kuhusu rasimu iliyorekebishwa ya Katiba ya Taasisi ya Fedha ya Afrika ili kuharakisha kupitishwa na kutumika kwa dharura.
6. Sasa najielekeza kwenye Mfuko wa Fedha wa Afrika. Kufikia Desemba 2023, bado kuna nchi kumi na mbili zilizosaini Itifaki ya Kuundwa kwa Mfuko wa Fedha wa Afrika na mbili zimesharidhia tayari. Idhini kumi na tano zinahitajika ili Itifaki ianze kutumika. Nazisihi nchi wanachama kusaini na kuridhia haraka iwezekanavyo Itifaki ya kuundwa kwa Mfuko wa Fedha wa Afrika.
7. Kuhusu Benki ya Uwekezaji ya Afrika, kulikuwa, hadi Desemba 2023, bado kuna nchi ishirini na mbili zilizosaini Itifaki na nchi sita zimeridhia. Idhini kumi na tano zinahitajika ili Itifaki ianze kutumika. Nimearifiwa kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Libya imeanzisha kamati ya pamoja ya uongozi ili kuharakisha uanzishwaji wa taasisi hii ya kifedha ya bara la Afrika. Hii ni maendeleo mazuri

ambayo yanastahili pongezi. Nazisihi nchi wanachama kusaini na kuridhia Itifaki haraka iwezekanavyo.

8. Sasa naelekea kwenye Soko la Hisa la Kimajumuyi. Baada ya kusainiwa kwa Makubaliano ya Kihistoria kati ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Chama cha Masoko ya Hisa ya Afrika mwezi Julai, 2022 huko Lusaka, Zambia na uzinduzi kufanyika tarehe 7 Desemba 2022 huko Abidjan, Côte d'Ivoire wa Mradi wa Uunganishaji wa Masoko ya Hisa ya Afrika (AELP), masoko saba ya hisa katika nchi 14 za Afrika yameunganishwa. Nazitia moyo nchi wanachama ambazo bado hazijajiunga na AELP kujumuika katika jitihada hizi ili kuzidisha na kuunganisha masoko ya mitaji ya Afrika pamoja na kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za ndani.
9. Kuna utafiti unaendelea kuhusu masuala ya kiufundi yanayohusiana na uanzishwaji wa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika. Baadhi ya masuala yatakayojadiliwa katika utafiti huo ni mapendekezo mapya kuhusu muundo wa hisa, viwango sahihi vya awali vya mtaji wa hisa, na mengineyo.
10. Kuna maombi yaliyosalia ya Benki ya Umoja wa Afrika ya Biashara na Uendelezaji wa Bima ili kupata hadhi ya shirika maalumu la Umoja wa Afrika. Baraza Kuu liliiomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuweka vigezo na mfumo wa wazi wa kupokea taasisi kama mashirika maalumu ya Umoja wa Afrika na kuripoti kwenye Mkutano wa Kawaida wa 43 wa Baraza Kuu. Naamini tutachunguza suala hili wakati wa kupitia ripoti ya Baraza Kuu.
11. Pia kuna Matukio Yanayojiri katika Taasisi za Fedha na Uchumi wa Kimataifa.
12. La kwanza ni Umoja wa Afrika kuwa mwanachama wa kudumu wa G20. Nawapongeza Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika wa mwaka 2023 na Rais wa Senegal kwa mafanikio haya chanya. La pili ni kuhusu Upangaji Uliofanywa wa Haki za Usanifu Maalumu. Benki ya Maendeleo ya Afrika ilichukua hatua za kupokea na kusimamia sehemu ya dola bilioni 100 kama Haki Maalumu za Usanifu zilizoungwa mkono na nchi zilizoendelea. Sasa ni jukumu letu kusaidia Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzipata fedha hizo na kuzitumia katika kufadhili mipango yetu ya ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu katika bara letu. Nawapongeza Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na timu yake kwa kazi nzuri waliyoifanya.
13. La tatu ni Biashara ya Kaboni ambayo inazidi kushamiri kama nishati mbadala ya kijani. Nchi zetu wanachama zinahitaji mwongozo wa wazi na kujengewa uwezo ili kufanya ukaguzi, tathmini na, miongoni mwa mambo mengine, kuingia mikataba yenye tija katika soko la kaboni linaloibuka. Napendekeza tumuombe Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika atoe rasimu ya msimamo ili tuijadili wakati wa Mkutano wa Kati wa Uratibu juu ya jinsi nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zinaweza kunufaika na mikataba inayozidi kuongezeka ya biashara ya kaboni.
14. Suala la nne ni kuhusu Changamoto za Marekebisho ya Deni. Mfumo wa Pamoja wa G20 wa Marekebisho ya Deni haujakidhi matarajio. Aidha, baadhi ya benki za maendeleo ya kikanda za Afrika zimekabiliwa na masuluhisho yasiyo ya haki katika marekebisho ya deni. Huku baadhi ya taasisi za kimataifa za fedha za maendeleo za kikanda zikifutiwa malipo na marejesho kupitia marekebisho ya deni, baadhi ya benki zetu za maendeleo za kikanda hazijafutiwa na hii inaathiri vibaya taarifa zao za mali na viwango. Napendekeza tumuombe Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika atoe rasimu ya msimamo juu ya jinsi ya kurekebisha Mfumo wa Pamoja wa G20 wa Marekebisho ya Deni, ikiwa ni

pamoja na masuluhisho yasiyo ya haki ya baadhi ya benki za maendeleo ya kikanda za Afrika, kwa lengo la kutamka misimamo hiyo wakati wa Mkutano wa Fedha wa G20 na Mkutano wa Viongozi Wakuu mwaka 2024.

15. Suala la tano ni kwamba mbali na Mapendekezo ya Mapato ya Ndani na Kupunguza Uhamishaji wa Faida kwa misingi ya OECD/G20, kuna haja ya Mageuzi ya Kimataifa ya Kodi kupitia Umoja wa Mataifa. Uamuzi wa kihistoria ulifanywa katika Umoja wa Mataifa mwezi Desemba, 2023 wakati ambapo kura nyingi zilipigwa kwa lengo la kutunga mkataba wa mfumo wa kodi. Napendekeza tuwapongeze Mabalozi wetu mjini New York kwa mafanikio haya ya kihistoria na kuwasihi waungane kusaidia kupata msaada mpana wa mkataba wa mfumo wa kodi wa Umoja wa Mataifa.
16. Nitahitimisha kwa kusema kwamba tuna kazi kubwa iliyobaki ili kurahisisha uanzishwaji wa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika. Suala hilo sasa limekuwa muhimu zaidi na kuingia katika hatua ya dharura kufuatia Umoja wa Afrika kuwa mwanachama wa kudumu wa G20, ambao unalazimu kuongezwa kwa uhamasishaji wa rasilimali za ndani. Kwa hiyo, nawasihi sote tuwe tayari kuongeza bidii ya kuzifanya Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika kuanza kufanya kazi . Hii itafanya sauti ya Afrika kuwa na ushawishi zaidi ndani na nje.

## 11. MHESHIMIWA FILIPE JACINTO NYUSI, RAIS WA JAMHURI YA MSUMBIJI NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU USIMAMIZI WA HATARI ZA MAAFA BARANI AFRIKA.

**1.** Kamisheni ya Umoja wa Afrika inatekeleza mipango kadhaa, ikisaidiwa na washirika kadhaa, kama ifuatavyo:

a. Programu ya kuimarisha usimamizi wa hatari za maafa kwa ustahimilivu katika kanda na nchi za Kiafrika ikisaidiwa na Umoja wa Ulaya

**b.** Kuimarisha uwezo wa kupunguza hatari za maafa na kanuni katika eneo la Sahel, ikisaidiwa na serikali ya Uswisi, kupitia UNDP**.**

**c.** Programu ya Mfumo wa Tahadhari na Hatua za Haraka za Hatari Mbalimbali za Kiafrika (AMHEWAS), ikisaidiwa na Serikali ya Italia, UNDRR, na Taasisi ya CIMA. Ni muhimu kusisitiza kwamba serikali ya Angola imetoa mtaalamu wa TEHAMA kwaajili ya Programu ya AMHEWAS. Tunapenda kutumia fursa hii kuishukuru sana serikali ya Angola kwa msaada wake.

d. Programu ya Ustahimilivu wa Mijini wa Afrika (AURP), iliyothibitishwa na wataalamu wa kiufundi kutoka Mataifa Wanachama na Jumuiya za Uchumi za Kikanda (RECs) mwezi Februari 2023 na inatarajiwa kutekelezwa kwa msaada wa GIZ.

**2.** Mwaka uliopita, nimeendelea kuhamasisha rasilimali na kukuza uhamasishaji kuhusu uhusiano kati ya maafa na kutokuwepo kwa usawa, ambao ulikuwa ujumbe muhimu kuhusu maadhimisho ya IDDRR ya mwaka 2023. Wakati wa COP28, nilizindua Ripoti ya Miaka Miwili ya 2019-2020 kwa Programu ya Hatua (PoA), chini

ya Mfumo wa Sendai kwa kupunguza Hatari za Maafa barani Afrika; na kushirikiana na na AUC, mikutano miwili ya pembeni ambapo niliwaomba washirika kusaidia maendeleo ya Programu ya AMHEWAS, pia nilizindua Ripoti ya Hiari ya Msumbiji kuhusu Ukaguzi wa Kati wa Utekelezaji wa Mfumo wa Sendai kwa kupunguza Hatari za Maafa mwaka 2015-2030; na kitabu kuhusu Ujenzi wa Ustahimilivu wa Hali ya Hewa nchini Msumbiji: Mfano wa  Shule Salama, kilichotengenezwa kwa msaada wa UN-HABITAT.

**3.** Maafa makubwa yaliyoripotiwa mwaka 2023 ni pamoja na: Kimbunga cha Tropiki Freddy, kilichoathiri Madagascar, Malawi na Msumbiji; Tetemeko la Ardhi huko Morocco, Mafuriko huko Libya; pamoja na Mafuriko na Maporomoko ya Ardhi huko Tanzania. Hivi karibuni, mwezi Januari 2024, Madagascar iliharibiwa na Kimbunga cha Tropiki Alvaro. Kutokana na matukio haya, tumetuma ujumbe wa mshikamano kwa Nchi Wanachama zilizopatwa na maafa, na kufanya juhudi za kukusanya rasilimali kwa ajili ya ujenzi baada ya maafa.

**4.** Kwa kuzingatia changamoto na fursa zilizobainika mwaka 2023, natoa mapendekezo kadhaa kwa AUC, Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ili kuimarisha juhudi za kupunguza Hatari za Maafa barani Afrika**:**

**a.** Nchi Wanachama zinahimizwa kuimarisha uwezo wa taasisi za kitaifa za Usimamizi wa Hatari za Maafa (DRM/DRR). Kuna haja ya kuajiri rasilimali watu na kuimarisha mamlaka ya taasisi za DRM/DRR ili ziweze kusimamia kwa ufanisi ukusanyaji wa data za hasara za maafa katika sekta zote**.**

**b.** AUC inapaswa kushirikiana na washirika wake kutekeleza Programu ya AMHEWAS, kurahisisha kuundwa kwa mifumo ya onyo la mapema dhidi ya hatari mbalimbali, na kuimarisha uwezo wa nchi na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ili kuchukua hatua za haraka.

Ili nafasi ya kupunguza Hatari za Maafa ndani ya muundo wa AU irasimishwe na kuwa taasisi lazima iambatane na ongezeko la bajeti zitokanazo na michango ya Nchi Wanachama kwaajili ya kupunguza Hatari za Maafa. Inapendekezwa kwamba AUC itenge baadhi ya fedha zinazotokana na michango ya Nchi Wanachama kwa ajili ya kufadhili Programu ya AMHEWAS.

## 12. MHESHIMIWA DR. JOSE MARIA PEREIRA NEVES, RAIS WA JAMHURI YA CABO VERDE, KINARA WA UMOJA WA AFRIKA WA UHIFADHI WA URITHI WA ASILI NA UTAMADUNI BARANI AFRIKA KWA MWAKA 2023

O Presidente da República de Cabo Verde, Doutor José Maria Pereira Neves, foi nomeado *Champion* da União Africana para a Preservação do Património Natural e Cultural de África no mês de fevereiro de 2023.

No mês de maio, na **Revista para os Profissionais do Património Africano**, o Presidente de Cabo Verde apresentou a missão do *Champion* e a sua visão de uma governação compartilhada do Património Natural e Cultural da África para a sua melhor preservação.

O **dia 5 de maio de 2023, Dia Internacional do Património Mundial Africano**, foi celebrado sob o lema "*O nosso Património Natural e Cultural ao serviço de uma África sem fronteiras*". Foi organizada uma Conferência Internacional e Online desde a sede da UNESCO em Paris que se iniciou com a mensagem de Sua Excelência Doutor José Maria Neves. No mesmo dia, em Cabo Verde, **no Palácio do Povo, na Cidade do Mindelo, em São Vicente**, o *Champion* da União Africana presidiu um colóquio sobre "*Do que falamos quando falamos de preservar o Património Natural e Cultural de África*".

No dia 20 de maio, presidiu, **no Palácio do Presidente da República de Cabo Verde na Cidade de Praia,** uma Conferência Comemorativa do Dia da África sobre "*Identidade e preservação do Património Natural e Cultural Africano*".

Na sequência da **45ª Sessão do Comité do Património Mundial, Riad, Arábia Saudita, 10-25 de setembro de 2023**, o *Champion* enviou às Organizações, às Instituições do Património Mundial, aos Técnicos Africanos para a Preservação do Património Natural e Cultural, **uma Declaração** congratulando-se com o número histórico de sítios africanos inscritos na Lista do Património Mundial em 2023 e apelando ao reforço das sinergias e das inteligências colaborativas para manter ou melhorar este nível de inscrições para a África nos próximos cinco anos e além.

O Presidente da República de Cabo Verde pretende, no segundo ano do seu mandato de *Champion*, contando com a colaboração dos seus pares africanos e do mundo e com os investimentos privados, continuar a advogar para mais ações e esforços na Preservação do Património Cultural Material e Imaterial, do Ambiente, das Espécies e Áreas Protegidas terrestres e marinhas.

**13. MHESHIMIWA WAVEL RAMKALAWAN, RAIS WA JAMHURI YA USHELISHELI NA KINARA WA UCHUMI WA BULUU**

Jamhuri ya Shelisheli, kama Kinara wa Uchumi wa Buluu wa Umoja wa Afrika, imeshiriki kikamilifu kwenye makongamano na mikakati muhimu ya kikanda na kimataifa kote mwaka 2023. Mazungumzo haya yalilenga kupigania kanuni endelevu, kukuza ushirikiano, na kuwa kinara wa Uchumi wa Buluu katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Uchumi wa Buluu wa Shelisheli unatoa njia kwa Mataifa Madogo yanayoendelea ya Visiwa (SIDS) kuboresha ustawi wa kijamii na kiuchumi wa watu wao. Kuzingatia athari kwa jamii ni muhimu si tu katika ngazi ya ndani nchi, bali pia kikanda na kimataifa.

Kipindi chote cha mwaka huo, makongamano mengi muhimu ya uchumi wa buluu yalipangwa. Ingawa Ripoti ya Uchumi wa Buluu ya Shelisheli ya mwaka 2023 haijataja kikamilifu shughuli nyingi zilizofanyika katika uga huu katika ngazi ya ndani,

ni muhimu kutambua kwamba nchini Shelisheli, asilimia 50 ya taasisi za umma zimeungana chini ya mwamvuli wa Uchumi wa Buluu ili kuwa vinara wa ajenda hii.

Zaidi ya hayo, Shelisheli imepiga hatua katika kuboresha mipango yake ya elimu. Mradi wa uhamasishaji wa bahari umekamilika na unatarajiwa kutekelezwa mwaka 2024. Aidha, kampeni kubwa ya uelimishaji imeanzishwa katika shule zote za sekondari za umma. Kampeni hii ilianza mwaka 2022 na kuendelea nchini kote mpaka mwaka 2023, ikapelekea 100% ya shule zote za sekondari na 99% ya shule zote za msingi kufikiwa na kampeni hiyo ya uelimishaji.

Kwa kuongezea, kumekuwa na mafanikio mengi ya kuvutia yaliyofanywa katika jitihada za utafiti. Haswa, mkusanyiko wa zaidi ya miradi 170 ya kuvutia ya Uchumi wa Buluu ilitekelezwa katika kipindi cha miaka mitano chini ya mradi wa SWIOfish3. Miradi hii ilijumuisha vipengele mbalimbali kama vile kujengea uwezo, kusimamia utawala, kupanua Maeneo Tengefu ya Bahari, na kuboresha usimamizi wa bahari. Ni vyema kubainisha kwamba, kati ya miradi hii, zaidi ya asilimia 90 imetekelezwa kwa mafanikio, na zaidi ya miradi 50 iko tayari kwa maboresho ya sekta ya uvuvi. Zaidi ya hayo, Idara ya Uchumi wa Buluu pia imesimamia zaidi ya miradi 20 ya ruzuku ya Uchumi wa buluu, ikichangia zaidi katika maendeleo na mafanikio ya jitihada hizi.

Shelisheli inasonga mbele kwa kuchukua hatua kubwa za ajenda ya uchumi wa buluu kupitia utekelezaji wa Mradi wa Pamoja wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG). Kwa undani zaidi, imepiga hatua kubwa katika kutafuta mbinu bunifu za ufadhili wa Biashara na Uchumi wa Buluu 122 zilizotambuliwa katika sekta ya uchumi. Zaidi ya hayo, nchi yetu inazisaka kwa bidii fursa za biashara katika uchumi na uchumi wa buluu katika kanda za COMESA na SADC, ikithibitisha zaidi nafasi yake kama kinara wa ukuaji endelevu wa kiuchumi.

Kwa kuongezea, kulikuwa na makongamano kadhaa muhimu ya uchumi wa buluu kikanda na kimataifa, ambayo yalishuhudia ushiriki wa Shelisheli na nchi zingine za Kiafrika, baadhi yao ni:

• Mkutano wa Mawaziri wa AIODIS kuhusu Uchumi kwa ujumla, ambao ulisisitizia mikakati ya pamoja kwa ajili ya kupunguza matumizi ya plastiki, kukuza uanzishaji wa biashara ndogo, na kuidhinisha Azimio la Mawaziri la maendeleo ya uchumi wa mzunguko katika kanda;

• Mkutano wa 9 wa Mazungumzo wa Bahari ya Hindi, ambao ulirahisisha ushirikiano kwenye vipaumbele vya kikanda katika sekta za uvuvi, bandari, mafuta na gesi, bioteknolojia ya baharini, kwa uchache tu;

• Kuidhinishwa kwa Mkataba wa Bahari wa BBNJ, ambao unazingatia uhifadhi na matumizi endelevu ya "bahari kuu" zaidi ya eneo maalumu la kiuchumi la nchi (EEZ);

• Jopo la Bahari, ambalo Shelisheli iliungana nalo mwaka 2023, ambalo linafungua njia ya kuimarisha uhusiano wa pande mbili, kuhamasisha maendeleo ya Uchumi wa Buluu, na kuongeza ushirikiano kati ya nchi za kaskazini na kusini katika ngazi ya kimataifa.

Kwa kuhitimisha, ni muhimu kusisitiza kwamba tukizingatia kuwa ajenda ya uchumi wa buluu ya Afrika inalenga kuleta mageuzi ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa binadamu kupitia matumizi busara ya rasilimali zilizopo baharini, inapendekezwa kuwa jitihada zifanyike katika ngazi ya kanda wa ili:

• Kuendeleza nguvukazi yenye msukumo katika muktadha wa uchumi wa buluu;

• Kuimarisha ushirikiano wa kitaifa kati ya serikali, viwanda, na jumuiya za kiraia ili kushughulikia masuala ya maslahi ya pamoja, na;

Kwa hiyo, kuongeza ushirikiano wa kikanda ili kuvutia rasilimali za kiufundi na kifedha na kusukuma mbele maslahi ya pamoja kwa maendeleo ya kimataifa na ajenda ya uchumi wa buluu.

## 14. MHESHIMIWA ABDELMADJID TEBBOUNE, RAIS WA JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA WATU WA ALGERIA NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA UGAIDI NA ITIKADI KALI.

### Muhtasari Kamili na Mapendekezo kuhusu Ugaidi na Itikadi Kali barani Afrika.

**1.** Utangulizi: Tishio linalozidi kuongezeka la ugaidi barani Afrika linakaribia viwango visivyokuwa vya kawaida, kwa mawanda na kijiografia. Hali hii tete inajumuisha mchanganyiko wa vurugu zinazotokana na itikadi, uhalifu ulioandaliwa kimataifa, na uasi. Licha ya juhudi za pamoja, upinzani wa makundi ya kigaidi unaendelea, ukisababisha mashambulizi yenye madhara kwa raia, vikosi vya usalama, na miundombinu muhimu. Maeneo yaliyoathiriwa yanashuhudia kupungua kwa imani ya umma katika uwezo wa serikali zao kulinda, hali inayosababisha mazingira ya kutokuwa na usalama na hofu.

**2.** Hali ilivyo katika Kanda Tofauti: Ugaidi barani Afrika unatawaliwa na makundi ya kienyeji yanayohusishwa na D'aesh au Al-Qaida. Kituo cha Kiafrika cha Utafiti juu ya Ugaidi kiliripoti zaidi ya matukio ya kigaidi 2,952 mnamo 2023, yakiwa na jumla ya vifo vya watu 15,556. Raia bado wanabaki kuwa waathirika wakuu, huku umuhimu wa kuchukua hatua za Pamoja ukizidi kuongezeka. Afrika Magharibi na Sahel zinajitokeza kama kama kanda zenye harakati nyingi za ugaidi, na kutokuwepo kwa utulivu wa kisiasa na kuondoka kwa misaada wa kigeni kukichagiza hali hiyo.

**3.** Sababu za Kushamiri kwa Ugaidi: Changamoto mpya zinazosababisha kushamiri kwa tishio la ugaidi ni pamoja na fedha za uendeshaji wa operesheni, utambuzi wa Wapiganaji wa Kigeni wa Kigaidi, makundi ya kigaidi kutumia teknolojia zaidi, athari za migogoro na kutokuwepo kwa utulivu wa kisiasa, na ushiriki wa makundi binafsi ya watu wasio katika serikali ikiwa ni pamoja na Kampuni Binafsi za Kijeshi/Mamluki. Uhusiano kati ya uhalifu ulioandaliwa kimataifa na ugaidi unahamia mtandaoni, kuongeza ugumu wa mandhari ya usalama.

**4.** Kuimarisha Mfumo wa Kitaifa: Aliishukuru AU kwa kupitisha mfumo wa kupambana na ugaidi wenye mantiki. Walakini, mabadiliko yanayojitokeza ya

tishio yanalazimu kupitiwa upya kwa mafanikio, kubaini mianya, na kuboresha mfumo wa kisheria, mpango wa utekelezaji, na kuimarisha uwezo wa taasisi maalumu husika, unaoongozwa na Kituo cha Kiafrika cha Utafiti juu ya Ugaidi (ACSRT). Ukuaji wa bajeti una umuhimu mkubwa katika kukabiliana kikamilifu na vitisho vinavyobadilika mara kwa mara.

**5.** Kutekeleza Maamuzi Yanayosubiriwa: Hatua za dharura zinahitajika kuhusu maamuzi yanayosubiriwa na AU, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Kamati ya Mawaziri ya AU ya Kupambana na Ugaidi (AUMCCT), kuweka Orodha ya Makundi ya Kigaidi ya Kiafrika, na Amri ya kukamatwa barani Afrika. Utekelezaji wa Kamati ya Kikundi cha Utendaji cha PSC inayohusika katika Kupambana na Ugaidi na Mfuko Maalumu wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ni muhimu kwa suluhisho endelevu.

**6.** Kuimarisha Ushirikiano: Kuhusu juhudi mpya na imara ndani ya Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, na Umoja wa Afrika ni muhimu katika kufuatilia kwa pamoja amani, usalama, na utulivu. Ushirikiano wa kimkakati miongoni mwa vikosi vilivyotumwa lazima uimarishwe ili kuzuia makundi ya waasi kujikusanya tena.

**7.** Mapendekezo: Kukabiliana na kuenea kwa tishio la ugaidi, mapendekezo ni pamoja na ushirikiano wa ubunifu, kuchanganya hatua za kijeshi na mbinu ya usalama wa binadamu, kujenga uwezo endelevu wa kupambana na ugaidi, kuamini mipango inayotolewa na Afrika, na kuendeleza zana za uamuzi zinazoweza kubadilika. Michango ya rasilimali fedha kwa kiasi kikubwa ni muhimu katika ngazi ya kitaifa, kikanda, na bara.

**8.** Hitimisho: Uwepo wa mabadiliko ya haraka ya shughuli za kigaidi unathibitisha umuhimu wa ushirikishwaji wa jamii na kujenga uelewa. Ufanisi wake unahitaji operesheni za kijeshi zinazoongozwa na taarifa zilizoboreshwa na mbinu ya Usalama wa Binadamu inayoshirikisha wadau, inayoshughulikia haki, ulinzi, ujumuishaji, elimu, na huduma za kijamii ili kuteka mioyo na fikra za jamii lengwa .

## 15. MHESHIMIWA EVARISTE NDAYISHIMIYE, RAIS WA JAMHURI YA BURUNDI NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KATIKA KUKUZA MPANGO WA "VIJANA, AMANI NA USALAMA BARANI AFRIKA"

Kwa mujibu wa Uamuzi wa [Mkutano mkuu /AU/Dec.842(XXXVI)] wa Mkutano wa 36 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (UA) uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 18 na 19 Februari 2023, **Mheshimiwa Evariste NDAYISHIMIYE**, **Rais wa Jamhuri ya Burundi**, aliteuliwa kuwa "Kinara wa Umoja wa Afrika kwaajili ya kukuza "Mpango wa Vijana, Amani na Usalama barani Afrika".

Ripoti ya kwanza ya Kinara huyu kuhusu hali ya utekelezaji wa ajenda ya Vijana, Amani na Usalama barani Afrika, inaonyesha hatua kuu zilizofikiwa na Kinara wa Ajenda ya Vijana, Amani na Usalama, ikiwa ni pamoja na mazungumzo na vijana wa Kiafrika ndani ya mwaka 2023, ambayo yalikuwa na kauli mbiu iliyolenga utekelezaji wa Ushirikiano wa Biashara Huria Barani Afrika (AfCFTA), pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mfumo wa Bara la Afrika wa Vijana, Amani na

Usalama, na Mpango wa miaka kumi (2020-2029) wa utekelezaji wake. Inaonyesha mafanikio yaliyofikiwa kuhusu nguzo tano, fursa na changamoto za utekelezaji wa Mfumo wa Bara la Afrika na Mpango wa miaka kumi wa utekelezaji wake. Pia inatoa mapendekezo ya kuharakisha utekelezaji wa Ajenda ya Vijana, Amani na Usalama barani Afrika, huku ikizingatia pia kauli mbiu ya mwaka huu 2024, yaani "Kuelimisha Afrika inayofaa kwa karne ya 21: kujenga mifumo ya elimu inayoweza kustahimili utoaji wa elimu bora na endelevu, kipindi chote cha uhai na inayolingana na mahitaji ya Afrika".

Kwa kweli, Mpango wa Miaka Kumi wa utekelezaji wa Mfumo wa Bara la Afrika kuhusu Vijana, Amani na Usalama (YPS) 2020-2029 una sehemu tano za kushughulikia zinazojumuisha shughuli ishirini na tatu muhimu zenye malengo na viashiria vya utendaji vilivyowekwa vizuri kwa kipindi cha katikati (mwaka 2024) na kufikia mwaka 2029. Mwaka huu unawakilisha mwaka wa tathmini ya katikati ya utekelezaji wa mpango wa miaka kumi na tunashuhudia kwamba kwa ujumla, licha ya juhudi zilizofanywa na wadau mbalimbali katika kutekeleza Ajenda ya Vijana, Amani na Usalama, utendaji kazi kulingana na malengo yaliyowekwa katikati bado ni dhaifu sana.

Utendaji hafifu ulioonekana unahusiana haswa na upungufu wa rasilimali watu wenye ujuzi wa kutosha katika masuala ya Vijana, Amani na Usalama haswa katika ngazi ya Nchi wanachama; upungufu wa fedha zilizotengwa kwaajili ya Programu ya Vijana ya Amani; kutokuwepo kwa mfumo endelevu wa ufadhili wa mipango inayohusiana na Ajenda ya Vijana, Amani na Usalama katika ngazi ya kitaifa, kikanda na bara; dhamira dhaifu ya Nchi wanachama katika kuendeleza Mipango Kazi ya Kitaifa kuhusu ajenda ya Vijana, Amani na Usalama, kwa kutumia Mfumo wa Bara la Afrika; pamoja na kutokuwepo kwa mfumo wa Mipanga ya kila mwaka na Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Ajenda ya Vijana, Amani na Usalama katika ngazi ya bara la Afrika.

Ni muhimu kuzidisha juhudi katika ngazi zote na kwa pande zote zinazohusika ili, mwishoni mwa mwaka 2024, tuweze kufikia malengo yote ya kati yaliyowekwa. Kamisheni ya Umoja wa Afrika inapaswa kuongeza juhudi zake ili kusaidia Nchi Wanachama pamoja na Jumuiya za Kikanda katika kuratibu jitihada zao na kuongeza kasi ya utekelezaji wa mipango katika ngazi ya kitaifa na kikanda, haswa kupitia uundaji wa Mipango ya Kitaifa ya Ajenda ya Vijana, Amani na Usalama, yenye kufuata Mfumo wa Bara la Afrika, na utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na elimu ya amani, kwa kuzingatia kauli mbiu ya mwaka 2024, ambayo ni "Kuelimisha Afrika ya Karne ya 21: kujenga mifumo imara ya upatikanaji mpana wa elimu na ujifunzaji jumuishi, wenye ubora, siku zote za uhai, na unaofaa kwa Afrika".

## 16. MHESHIMIWA MATAMELA CYRIL RAMAPHOSA, RAIS WA JAMHURI YA AFRIKA YA KUSINI NA KINARA WA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU UVIKO-

**Ripoti ya Kinara wa UVIKO-19** kwenye Mkutano wa 37 wa Kawaida wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali inawasilishwa na Mheshimiwa Rais Matamela Cyril Ramaphosa kuhusu jukumu lake alilopewa kuwa kiongozi wa mkakati wa kukabiliana na UVIKO-19 wa bara Afrika na Umoja wa Afrika (AU) kupitia Maamuzi ya Mkutano Mkuu /AU/Dec.797(XXXIV) ya Februari 2021, Mkutano Mkuu /AU/Dec.816(XXXV) ya Februari 2022, pamoja na Mkutano Mkuu /AU/Dec. 839-865(XXXVI) ya Februari 2023, ambayo yalieleza kuwa AU inapaswa kuendelea kushughulikia suala la UVIKO-19.

Ripoti hiyo imejikita katika kubadilisha jukumu la Kinara na kujumuisha Magonjwa ya Kuambukiza, Kinga, Maandalizi na Majibu (PPPR), pamoja na kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika (CAP) kuhusu Kinga, Maandalizi, Majibu na Uokoaji kutokana Magonjwa ya Kuambukiza(PPPRR). Kuhusu hilo, Mchakato wa Johannesburg utatoa jukwaa lisilo rasmi la kujadili upatikanaji sawa wa tiba, pamoja na msaada wa ushauri, kiufundi, vifaa tiba, ikijumuisha msaada wa kifedha kwenye mikutano ya majadiliano na wadau kuhusu Magonjwa ya Kuambukiza, Kinga, Maandalizi na Majibu, na Msimamo wa pamoja wa Afrika (PPPR na CAP).

Mkakati ulioboreshwa wa Kinara unazingatia maeneo muhimu yafuatayo kwa ajili ya uponyaji baada ya athari za Uviko-19 na kwa maandalizi ya baadaye ya Magonjwa ya Kuambukiza, Kinga, Maandalizi na Majibu (PPPR): i) Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu PPPR; ii) Kuongeza Michango kweny Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika; iii) Mchakato wa Johannesburg; iv) Ununuzi wa 30% wa Bidhaa za Kiafrika na Wanunuzi Wakubwa; v) Kanuni za Upendeleo kwenye sheria za Manunuzi; vi) Sera ya Maendeleo na Kuwabakisha Kazini Wafanyakazi wa Afya; vii) Kuimarisha Mifumo ya Afya (ikiwa ni pamoja na kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa PPPR); viii) Mfumo wa Uwajibikaji kwaajili ya Ajenda ya Lusaka (Mpango wa Baadaye wa Afya ya Kimataifa); ix) Uungwaji mkono Kisiasa wa Mpango wa Dharura wa Pamoja wa Afrika CDC/WHO; na x) Uwiano wa Kijinsia katika majibu ya PPPR. Kulingana na maeneo muhimu yaliyotajwa hapo juu, Kinara anawasilisha mapendekezo kumi yafuatayo:

1. Kuidhinisha Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Kinga, Maandalizi na Majibu ya Magonjwa ya Kuambukiza (ukihakikisha kwamba masuala ya kurejesha hali ya kawaida yanafafanuliwa vizuri pia);
2. Kuhimiza vyombo vya sera vya Umoja wa Afrika kukamilisha kwa haraka uanzishwaji wa Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika na Kinara kuanza kuendesha kampeni ya kurejesha upya. Nchi zote lazima ziwe tayari kuchangia;
3. Wakati tukisherehekea uzinduzi wa GAVI wa Kasi ya Watengenezaji wa Chanjo wa Kiafrika, kuendelea kushiriki katika utetezi imara ili kushawishi wanunuzi wote wakubwa wa dawa kununua 30% ya bidhaa zilizokusudiwa kwa ajili ya Afrika kutoka kwa Watengenezaji wa Kiafrika;

4. Kuendelea kusaidia Mchakato wa Johannesburg na kuhamasisha nchi wanachama wa AU kutumia jukwaa lisilo rasmi kama fursa ya mazungumzo imara na kujenga makubaliano tayari kwa mazungumzo rasmi;
5. Kuhimiza vyombo vya sera vya AU kukamilisha uandishi wa kanuni za kisheria za Manunuzi ya Upendeleo (wa Bidhaa za Dawa za Kiafrika) kwa haraka kati ya nchi wanachama;
6. Kuendelea kutoa uungwaji mkono wa kisiasa kwa Timu ya Msingi ya Wafanyakazi wa Afya na kuhimiza nchi wanachama kupunguza changamoto ya waatalamu wa afya wa Kiafrika kuhamia ughaibuni kwaajili ya kujipatia fursa bora zaidi;
7. Kuweka mazingira wezeshi na kutumia uwezo wote muhimu wa serikali kusaidia Juhudi za Kuimarisha Mifumo ya Afya;
8. Kusaidia uanzishwaji wa mfumo wa uwajibikaji ndani ya muundo wa AU ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi wa Ajenda ya Lusaka Barani Afrika;
9. Kusaidia jitihada za uwekezaji kwenye Mpango wa Dharura wa Pamoja wa Africa CDC na Shirika la Afya Duniani; na
10. Kuhakikisha kwamba juhudi zote za kukabiliana na janga zinaaksi Uwiano wa Kijinsia.

**AFRICAN UNION UNION AFRICAINE**

**African Union Common Repository** **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

# Annual Report of the Activities of the African Union and its Organs

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10555

*Downloaded from African Union Common Repository*